لا إله إلا الله محمد رسول الله

# SAFINA YA NUHU

**Kimeandikwa na:**

**Seyyidna wa Maulana Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as)
Masihi Aliyeahidiwa na Mjumbe wa Mungu kwa siku
hizi za mwisho – Qadian Bara Hindi**

**Kimeenezwa na;**

**Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya – Tanzania**

**S.L.P 376, Simu:+255222111031; Fax +255222121744**

**Dar es Salaam**

Chapa ya mara ya kwanza 1944 ……….. Nakala 2,000

Chapa pili 1957 ………………...............…. Nakala 3,000

Chapa ya tatu 1963 ……………......……… Nakala 5,000


Chapa ya nne 1987 ……….........…………. Nakala 10,000

Chapa ya tano 2018 …….........………….. Nakala 3000

وَاصْنَعِ الْفُلْكَ بِاَعْيُنِنَا

*(Quran Tukufu)*

# SAFINA YA NUHU



**Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as)**

**Masihi Aliyeahidiwa**

# Kashti-i-Nooh

## (The Ark of Noah)

The Kashti-i-Nooh was also given two other titles; Dawatul Iman (The Invitation to Faith) and Taqwiyatul Iman (The Strengthening of the Faith) and it was published on 5th October 1902. The title page in addition to the three titles of the book also has the writing which means 'A booklet to be meant as a heavenly inoculation for the Jamaat against bubonic plague'. The title page also carries two couplets which mean 'This bubonic plague has broken the heart of the people; this plague is not just a plague, it is a great flood (deluge). Hurry up and come to my Ark, for this Ark has been prepared under the Divine Command'.

Hazrat Ahmad (as) had a vision on 6th February, 1898 that the Angels were planting some plants of blac colour in various parts of the Punjab; these plants, as he saw them, were very ugly, black and terrifying and of small stature. He says that he asked some of those who were planting the plants as to what those trees were and he was told that they were the trees of bubonic plague which was going to break out in the country very soon. He further says that it did not become clear to him whether this plague was to break out in the next winter or the winter after that but what he saw was something very terrible and he had also received a revelation which pointed to the breaking out of the bubonic plague.

Hazrat Mirza Ghulam Ahmad (as) explains the position of Hadith and the Sunna (the practice of the Holy Prophet, peace and blessings of Allah be upon him) and also tells his readers what significance these two things have got in conjunction with

the Holy Qur'an. He advises his followers to take heed of the Hadith, for a number of people, he says, are ignoring it. Of course, only such Hadith has to be considered valid as tallies with the teachings of the Holy Qur'an.

He makes mention of the death of Jesus Christ and reproduces a Hebrew writing bearing testimony to the fact that the tomb of Jesus Christ which Hazrat Ahmad pointed out to be in Srinagar is rally and truly a tomb like that of the elders of the Israelites.

As the epilogue to the book, Hazrat Ahmad calls upon his Jamaat to improve their spirituality so that the wrath of God that was raging in the world might subside.

بسم الله الرحمن الرحيم

## NENO LA MBELE

Kitabu hiki 'SAFINA YA NUHU' kilichoandikwa na Seyidna wa Maulana Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad, Mjumbe wa Mungu kwa siku hizi na kimefasiriwa kwa lugha ya Kiswahili na Maulana Sheikh Mubarak Ahmad, H.A, kilipigwa chapa mara ya kwanza mnamo mwaka 1944. Watu wengi wamepata faida kwa kukisoma na kujua mambo ya Dini ya Kiislam. Kwa Baraka ya Mwenyezi Mungu tumepata nafasi kukipiga chapa mara ya tatu. Twamwomba Mwenyezi Mungu Atie Baraka Zaidi katika kitabu hiki, na Awabariki sana na Awafunulie haki wale wanaokisoma, ili wapate nuru ile ilioteremshwa siku hizi, Amin.

**Ahmadiyya Masjid,**
**Fort Hall Road,**
**Nairobi, Kenya.**
**08th November, 1963**

**Sheikh Nur-El-Haq Anwar,**
**Mubashir wa Islam.**

## MANENO YA MFASIRI.

### 1. Shukrani:

Mwenyezi Mungu Anao uwezo wa kila namna na mwanadamu, ingawa ni mdhaifu na mnyonge kabisa, lakini anapopewa na Mwenyezi Mungu uwezo na nafasi njema, anaweza kufanya lolote. Mimi niliyefasiri kitabu hiki, ijapokuwa ni Mhindi, lakini juu ya hayo nilipopewa na Mwenyezi Mungu uwezo na nguvu nikamaliza kazi ya kukifasiri kitabu hiki ninachokiweka mbele yenu sasa. Kwa hiyo, ni wajibu wangu nimshukuru Yule Mwenyezi Mungu aliyenipa uwezo huo. Tena naomba kwake kwa unyenyekevu kwa jinsi alivyonisaidia kufasiri kitabu hiki Awasaidie ndugu zangu wasomaji waweze kukisoma kitabu hiki na kupata neema ile tuliyopata sisi.

### 2. Mtungaji wa Kitabu:

Kitabu hiki kilichofasiriwa kwa lugha ya Kiswahili kimetungwa na Seyidna wa Maulana Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian, Bara Hindi. Mtungaji wa kitabu hiki ni mtu maarufu na anayejulikana sana katika kila nchi kwa sababu ya utakatifu na kazi aliyoifanya kwa kuijadidisha dini ya Kiislam na kwa kuisimamisha sharia ya Quran. Yeye ndiye aliyekuwa Masih-ul-Mau'ud na ndiye yeye Imam Mahdi katika siku hizi za mwisho na cheo hiki kapewa na Mwenyezi Mungu. Alizaliwa katika mwaka 1835 siku ya Ijumaa tarehe 13 mwezi wa Februari, na akaishi miaka 75 baada ya kumaliza kazi yake kwa kufanikiwa, na akafariki tarehe 26 Mei, 1908.

### 3. Kusudi la kutunga kitabu hiki:

Kitabu hiki kilitungwa katika lugha ya Kiurdu alipopata ufunuo mara nyingi kutoka kwa Mwenyezi Mungu ya kwamba ugonjwa wa tauni hivi karibuni utaenea sana nao kwa hakika utakuwa ni adhabu itokayo kwa Mwenyezi Mungu ili kuwaangamiza

wakadhibishao Ishara za Mungu na wanaomkataa Mjumbe wa Mungu wa siku hizi. Pia aliambiwa na Mwenyezi Mungu kwamba watakaomfuata Mjumbe huyu hawatashikwa na ugonjwa huo kabisa. Ijapokuwa maadui watapigwa sindano ya tauni lakini hawataokoka katika balaa hili na hii itakuwa ishara ya ukweli wa Mjumbe wa Mungu wa siku hizi. Kwa hiyo akaona ni afadhali aandike kitabu kimoja chenye maagizo ambayo kwa kuyashika watu bila shaka watasalimika katika ugonjwa wa tauni hata bila ya kupigwa sindano.

4. **Majina ya Kitabu hiki:**

Kwa ajili ya haya mtungaji mtakatifu wa kitabu amekiita kwa majina matatu.

(i) Kashtie Nuh – Safina ya Nuhu, yaani kwa kupanda safina mtu anaokoka katika taabu ya bahari na anafika salama barani; hivyo ndivyo watakaoshika sawasawa maagizo mema yaliyomo katika kitabu hiki watakavyosalimika katika ugonjwa wa tauni, maana wameingia katika safina iliyoundwa kwa amri ya Mungu.

(ii) Da'watul Iman – wito wa Imani, yaani kitabu hiki kinawaita watu katika siku hizi za upotevu kwenye Imani, na kujulisha ya kwamba kuamini Mwenyezi Mungu ndiyo njia hasa iwezayo kuwalinda katika adhabu ya tauni.

(iii) Tak-wiyatul Iman-Kuipa nguvu Imani, yaani katika kitabu hiki yameelezwa mambo ya Imani kwa namna iliyo nzuri ambayo kwa kuyasoma na kuyashika Imani inazidi, na inapozidi Imani mtu anajiepusha na maasi, na aachapo maasi anasalimika.

5. **Kazi ya Tafsiri:**

Nakumbuka katika mwaka 1937 niliambiwa na Nazarat Da'wat-o-Tabligh, Ofisi ya kupeleka wabashiri katika nchi za kigeni, kwamba nikitafsiri kitabu hiki chenye manufaa sana kwa kuwaongoza watu na kuwatoa katika giza la upotovu ili kuwapeleka kwenye nuru. Maana katika kitabu hiki zimeelezwa ishara za Mwenyezi Mungu zilizodhihirishwa siku hizi za mwisho, na imehakikishwa kwamba mafundisho ya Kiislamu ni bora kuliko mafundisho ya Kikristo na hakuna njia nyingine ya wokofu isipokuwa njia ile iliyoelezwa na Mtume Muhammad, Amani ya Mungu juu yake. Tena kitabu hiki kitawafaa wale wanaoleta mara kwa mara upinzani juu ya Waahmadiyya watakaposoma maneno hasa ya mwanzishaji mtakatifu wa Jamaat ya Ahmadiyya, maana mtu kujisomea si sawa na kusikia. Basi, kwa makusudio haya, kwa Baraka za Mwenyezi Mungu katika mwaka 1938 nikamaliza tafsiri ya kitabu hiki.

6. **Kazi ya kusahihisha:**

Lakini sasa lilipokuwa karibu kumalizika jengo la Ahmadiyya Masjid-ul-Fadhl mjini Tabora niliona ni heri watu wa nchi hii watakapopata nyumba ya Mwenyezi Mungu pia wapate safina iliyoundwa kwa amri ya Mwenyezi Mungu ili kwamba sio waokoke katika balaa tu, bali pia wapate Baraka na neema za Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo tafsiri hii imesomwa tena, na imesahihishwa katika siku hizi chache zilizopita ikapangwa katika mafungu madogo –madogo.

Katika kazi ya kusahihisha mahali pengi nimesaidiwa na mpenzi Mwalimu K. Amri Abedi, anayefanya kazi ya ubashiri sasa pamoja na mimi. Na pia kazi ya kupiga taipu karatasi za kitabu hiki imefanywa na yeye. Pia nimepewa mashauri mema na ndugu wengine, na ninawashukuru hawa wote nami namwomba Mwenyezi Mungu Awajaalie heri. Endapo

likionekana kosa lolote basi hilo limekuwa kwa ajili ya upungufu wangu katika kufasiri.

7. **Anwani na maelezo mengine:**

Ikumbukwe ya kwamba kitabu hasa kilichotungwa katika lugha ya Kiurdu hakina milango na fusuli, lakini kwa kupiga chapa katika Kiswahili nimeweka milango mbali-mbali ili watu wapate kufahamu mara moja.

Anwani za milango hii yote pia ni maneno yangu si ya mtungaji mtakatifu. Zaidi ya haya, yako baadhi ya maelezo yaliyoandikwa chini katika kurasa, ambayo yameandikwa nami na yanapambanuka kwa kuandikiwa mwishoni neno (Mfasiri) ndani ya mabano, lakini maneno mengine yote ndani ya kila mlango ni ya mtungaji mtakatifu.

8. **Neno la mwisho.**

Mwishoni, naomba Mwenyezi Mungu, kwa rehema zake hasa, apokee juhudi yangu hii ya kufasiri kitabu hiki cha Mjumbe Wake – Seyyidna Mirza Ghulam Ahmad a.s., na awape uwezo watu wa nchi hii wa kukisoma ili wapate nuru ile iliyoteremshwa siku hizi na wapate kumwamini Masihi-ul-Mau'ud ambaye Mtume Muhammad, amani ya Mungu juu yake, aliwaagiza Waislamu wamkubali. Mwenyezi Mungu Atie baraka katika tafsiri hii kama Anavyotia baraka katika vitabu vya wapenzi wake. Tena Afungue roho za watu ili wakipokee kwa nia safi na kiwe mwongozo kwa ajili yao; Amini. Na neno langu la mwisho ni; "Sifa zote njema zinamhusu Mwenyezi Mungu".

**Ahmadiyya Masjid Alfadhl,**
**Sheikh Mubarak Ahmad, (H.A)**
**Usagara Street,**
**24th July, 1944**
**Tabora, T.T**
**3 Shaaban, 1363 A.H**

## YALIYOMO

**Sura** **Ukurasa**


1. Kupiga Sindano ya Tauni ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 1

2. Mafundisho yaliyo bora kabisa ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 16

3. Malinganisho kati ya Quran na Injili ... ... ... ... ... ... ... 38

4. Bishara kuu iliyomo katika sura ya Alhamdu ... ... ... ... 62

5. Jinsi Masihi wa Muhammad alivyofanana na Masihi wa Musa ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 72

6. Njia zingine za Mwongozo ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 80

7. Mawaidha juu ya Yakini, Sala na Wokofu ... ... ... ... ... 89

8. Msishike mwendo wa Mayahudi ... ... ... ... ... ... ... ... ... 97

9. Maagizo mema machache kwa wanawake ... ... ... ... ... 105

10. Nasaha nzuri ya mwisho ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 108

بسم الله الرحمن الرحيم

*Kwa jina la Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na ukarimu.*

*Tunamhimidia na tunamsalia Mtume wake Mtukufu.*

# SURA YA KWANZA

## Kupiga Sindano ya Tauni

*Lan yuswiybana illa ma kataba llahu lana huwa maulana wa'alallahi falyatawakkalil mu'minuuna* – Hautufiki msiba wowote ila Aliotuandikia Mwenyezi Mungu; Yeye ndiye Mola wetu; basi waaminio wamtegemee Mwenyezi Mungu tu[1].

Mahali pa kuishukuru Serikali ya Kiingereza kwa sababu ya kuwatakia wema na kuwarehemu raia zake, na kuwavusha katika ugonjwa wa Tauni, ilitoa amri ya kupiga sindano. Na kwa hivi serikali yetu imebeba mzigo wa maelfu na maelfu ya rupia kwa ajili ya kuwahurumia na kuwatakia wema viumbe vya Mwenyezi Mungu. Bila shaka hiyo ndiyo kazi inayotakiwa kupokewa na raia wenye busara kwa kushukuru.

Na ni mjinga kabisa tena adui wa nafsi yake mwenyewe anayeliona shauri hilo la kupiga sindano ya Tauni kwa dhana mbaya. Maana imekwisha hakikishwa, baada ya majaribio mengi ya kwamba, dola yetu haikubali kabisa kuwaambia watu watumie shauri au dawa fulani yenye hatari mpaka ithibitishwe na kuonekana kuwa inafaa. Basi kusema kuwa serikali, inayotoa laki na laki za rupia kwa sababu ya kuwafanyia wema raia, ina makusudio yake hasa kwa kuyabeba mashaka haya, ni mbali na utu na tabia njema. Hakika raia wenye kudhani vibaya kwa namna hiyo ni wenye bahati mbaya.

1 Sura 9, aya 51

Bila shaka shauri jema lililokuja mikononi mwa Serikali yetu mpaka sasa ni dawa ya kupiga sindano kwa ugonjwa wa Tauni. Na shauri hilo haliwezi kukataliwa kwamba si lenye manufaa. Na ni wajibu kwa watu wote raia kulishika na kulifuata shauri hili la kupiga sindano, waiondoe huzuni ya Serikali iliyo nayo kwa ajili yao. Lakini tunasihi na kuomba kwa adabu nyingi kwa Serikali yenye hisani kuwa, kama tusingalikatazwa na kizuio cha mbingu, tungalikuwa wa kwanza katika raia kukubali shauri hilo la kupiga sindano ya Tauni.

Na makatazo yale ya mbinguni ni kuwa Mwenyezi Mungu Ametaka kuwaonyesha watu wa siku hizi ishara katika ishara Zake za rehema. Kwa hiyo Aliniambia Mwenyezi Mungu, Akanena:

"Wewe na wa nyumbani mwako na mwenye kuwa nawe kwa kukufuata sana na kukutii kwa roho safi, hao wote wataepushwa na ugonjwa wa Tauni. Na hii itakuwa ishara ya Mwenyezi Mungu siku hizi za mwisho ili kupambanua baina ya mataifa. Lakini asiyekufuata sawasawa huyu si katika wafuasi wako; na kwa ajili yake usihuzunike".

Hii ni amri ya Mwenyezi Mungu. Basi kwa sababu ya amri hii sisi hatuna haja, wala wanaokaa nyumbani mwetu hawana haja, ya kushika shauri hilo la kupiga sindano ya Tauni.

Maana kama nilivyobainisha sasa hivi muda kidogo kabla ya leo, nimefunuliwa na Mwenyezi Mungu, ambaye ni Bwana wa mbingu na ardhi na anayo elimu na uwezo wa kila kitu; alinifunulia akasema; "Mimi nitamlinda mtu yeyote katika kifo cha Tauni atakayekuwa katika boma la nyumba hii, kwa sharti aache kila mambo ya uasi na aingie katika silsila (ya Ahmadiyya) kwa nia safi na kwa utii kamili na unyenyekevu.

Na asiwe mbele ya amri za Mwenyezi Mungu na Mtume wake, mwenye kiburi na ushupavu na kujivuna na kujipenda; bali awe mtendaji hasa wa mafundisho".

Na zaidi ya haya pia aliniambia kwamba; "Hautatokea katika mji wa Qadian, ugonjwa wa Tauni wenye nguvu sana kuwaua watu wengi kabisa na kuleta maangamizo hata wahilikishwe kama mbwa, na wawe wenye kuchanganyikiwa kwa sababu ya huzuni na mahangaiko".

Na watu wote wa Jamaat ya Ahmadiyya, kadiri itakavyokuwa hesabu yao, watasalimika kwa Tauni kuliko maadui zao, isipokuwa wale wasiotimiza ahadi zao, au kwa sababu nyingine ya siri Anayoijua Mwenyezi Mungu, wanaweza kushikwa na Tauni. Lakini mwishoni watu watakiri kwa kustaajabu kwamba, kweli msaada wa Mungu upo pamoja na Jamaat ya Ahmadiyya bali si kwa mataifa mengine, na Amewalinda Waahmadiyya kwa rehema Zake hasa kwa ulinzi usio mfano.

Juu ya jambo hili baadhi ya wapumbavu watashtuka, wengine watacheka na baadhi yao wataniona mwenye wazimu, na pengine kuliona jambo hili watashangaa sana kama huko kuna Mungu mwenye kuweza kuteremsha rehema bila sababu yoyote? Jibu lake ni kweli huko kuna Mungu Mwenye uwezo wa namna hiyo. Lau kama kusingalikuwa Mungu wa namna hii wapenzi wake wanaoungana na Yeye wangalikufa kabla ya siku zao za maisha. Bila shaka Yeye ni wa ajabu na pia uwezo wake ni wa ajabu! Upande mmoja anawasalitisha maadui wajinga, juu ya marafiki wake kama majibwa, na upande mwingine anawaamuru malaika kuwatumikia. Hivyo ndivyo ghadhabu yake inaposhuka duniani na adhabu yake inapochemka juu ya wadhalimu ndipo hapo macho yake yanalinda wale walio watu wake hasa. Lau kama isingalikuwako desturi hii ya Mwenyezi

Mungu kazi ya wenye haki ingalivunjika, na kuchanganyika mambo mazuri na mambo mabaya; wala asingeweza yeyote kuwafahamu. Kweli, uwezo wake haumkini kuhesabika wala haumkini kukusanyika; ni mwingi mno lakini unawadhihirikia watu, kwa kiasi cha yakini yao, wale waliopewa yakini na shauku na waliojitupa kwa Mwenyezi Mungu na wakaondolewa katika matamanio ya kidunia; na hao ndio watakaoonyeshwa uwezo wake hasa kinyume cha desturi yake ya siku zote. Hakika Mwenyezi Mungu Hufanya Anavyopenda.

Lakini Hutaka Kudhihirisha uwezo wake hasa kinyume cha desturi ya siku zote kwa ajili ya wale wanaojitakasa na wanaacha ada zao. Lakini siku hizi watu wanaomfahamu na wanaoamini uwezo wake wa ajabu ni wachache tu. Bali wengi wale wasiomwamini Mungu Mwenyezi ambaye sauti Yake kila kitu husikia na ambaye hapana kitu cho chote kisichokuwa katika uwezo wake. Kumbukeni ya kwamba kutumia dawa kwa ugonjwa wa Tauni na kwa maradhi mengine si dhambi; bali imesemwa katika hadithi moja ya Mtume Mtakatifu, kuwa hapana ugonjwa wowote ila Mwenyezi Mungu Ameuumbia dawa yake. Lakini mimi naona ni hatia kubwa kuficha ishara ya Mwenyezi Mungu kwa kupiga sindano ya Tauni na kufedhehesha ishara ya kweli na ahadi ya haki, aliyotaka kuonyesha duniani kwa wazi wazi. Kwa hiyo, sipendi kuvunja heshima ya agano Lake la kweli, na lau kama nikilivunja, basi itakuwa ni kosa langu litakaloulizwa kwa sababu ya kutoamini ahadi Aliyoniahidi Mola wangu Mwenyezi Mungu. Na lau kama ni hivi basi juu yangu nimshukuru daktari aliyeivumbua dawa ya kupiga sindano ya Tauni wala nisimshukuru Mungu Aliyeniahidi na kusema; “Nitalinda kila aliyomo katika boma la nyumba hii, yako”.

Mimi nasema kwa busara na maarifa kwamba ahadi za

Mwenyezi Mungu ni kweli; na mimi naona siku zijazo kama zimekwisha fika.

Na pia ninafahamu kwamba kusudi hasa la dola yetu tukufu ni kuhifadhi watu katika Tauni na wapate kuokoka katika ugonjwa huu wa Tauni kwa njia yoyote. Na hata Serikali ipate shauri jingine bora kuliko kupiga sindano itakubali kwa furaha. Basi ni dhahiri kuwa njia hii Aliyonionyesha Mwenyezi Mungu na Kuniendesha juu yake haikushindana na kusudi la Serikali kabisa, bali inafanana na shauri lake. Na miaka ishirini iliyopita, toka leo, ufunuo utoao habari ya matokeo ya balaa kubwa hili la ugonjwa wa Tauni umo katika kitabu changu kiitwacho Barahiine Ahmadiyya, na pia imo Ahadi ya Mwenyezi Mungu ya baraka nyingi zitakazoteremshwa juu ya Silsila hii (ya Ahmadiyya). Tazameni kitabu changu Barahine Ahmadiyya ukurasa wa 518 na 519.

Zaidi ya hayo uko unabii kutoka kwa Mwenyezi Mungu utoao habari kwa wazi wazi ya kwamba Mwenyezi Mungu Atawalinda, watu waliohalisika katika boma la nyumba yangu na kuwaokoa wale wasiofanya kiburi mbele ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake, katika ugonjwa wa Tauni; na fadhili za Mungu zitaonekana nyingi juu ya Jamaat ya Ahmadiyya kuliko Jumuiya zote zingine. Na lau kama kwa sababu ya udhaifu katika imani yake au kwa upungufu wa vitendo vyake au kwa ajali yake iliyowekwa au kwa sababu nyingine anazozijua Mwenyezi Mungu, akifa mmoja katika Jamaa Ahmadiyya basi hukumu yake itakuwa isiyohesabika.

Maana yake, katika kushindana linatazamwa jambo liletalo faida nyingi kama vile serikali baada ya majaribio mengi imekwisha jua ya kuwa wanaopigwa sindano wanakufa wachache kuliko wasiopigwa sindano. Lakini kama uzuri wa dawa ya kupiga

sindano haukupungua kwa sababu ya mtu mmoja kufa, hivyo ndivyo kama ikitokea Tauni hapa Qadian au akifa mmojawapo katika Jamia hii kwa kushikwa na Tauni haiwezekani kutenguka heshima ya ishara hii ya Mwenyezi Mungu.

Unabii huu umeandikwa kwa kufuata matamko yanayodhihirika katika usemi mtukufu wa Mwenyezi Mungu. Si desturi ya mtu mwenye akili kuyacheka maneno ya mbinguni kabla ya kutokea kwake. Hayo ni maneno ya Mwenyezi Mungu si maneno ya mpiga ramli, mwongo; tena ni katika macho ya nuru si katika giza la ovyo. Haya ni maneno ya yule Aliyeteremsha Tauni na Awezaye kuiondoa. Bila shaka serikali yetu itafahamu ubora wa unabii huu wa kweli itakapoona matokeo yake ya ajabu na itashangaa sana ndipo itasema ya kuwa, imekuwaje hivi? Kumbe! Watu hawa wasiopigwa sindano ni wenye afya sana tena salama kuliko wale waliopigwa sindano!

Nawaambieni kweli kweli, kama haikutokea ishara hii sawasawa na unabii unaotangazwa tangu miaka 20 au 22, basi sitakuwa mwenye kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Kwa yakini ishara hii, yaani watu waliohalisika wakaao katika boma la nyumba yangu watalindwa na kuepushwa na ugonjwa wa Tauni, itakuwa dalili kubwa ya kutoka kwangu kwa Mwenyezi Mungu. Na wafuasi wangu wote watahifadhiwa katika madhara ya shambulio la Tauni kuliko watu wa madhehebu na mataifa mengine; na salama watayokuwa nayo haitaonekana mfano wake katika watu wengine. Na katika mji wa Qadian hayatatokea maangamizo ya ugonjwa wa Tauni kwa nguvu na shida, isipokuwa kidogo yatakayokuwa yasiyohesabika.

Laiti watu hawa wangalikuwa wenye mioyo safi na kumwogopa Mwenyezi Mungu wangalilindwa kabisa, sababu kwa udhuru wa hitilafu ya dini haiteremki adhabu, kosa hili litahukumiwa

siku ya kiyama. Bali adhabu inakuja duniani kwa sababu ya shari na ufasiki na kwa wingi wa madhambi.

Na pia kumbukeni kuwa habari za kutokea Tauni si katika Quran Tukufu tu, bali vile vile zimo katika baadhi ya vitabu vya Torati[2], kwamba katika siku za kufika kwake Masih-ul-Mau'ud, Mjumbe aliyeahidiwa, ugonjwa wa Tauni utatokea duniani. Na Nabii Isa, amani ya Mungu juu yake, vile vile ametoa habari hii ya Tauni katika Injili[3], na haiwezekani kupotea bure unabii na ubashiri wa Manabii.

Na mwakumbuka ya kwamba ni wajibu wetu tujiepushe na mashauri mengineyo ya kibinadamu ili adui yeyote asipate kusema kwamba ishara hii ya Mwenyezi Mungu imetokea kwa sababu nyingine. Lakini kama Mungu Mwenyewe Afahamishe dawa au shauri lolote kwa ufunuo wake, basi haiwezi kupunguka heshima ya ishara ya Mwenyezi Mungu kwa kutumia dawa na kushika shauri hilo litokalo kwa Mwenyezi Mungu, maana limetoka kwa Mungu ambaye Ametoa ishara ile.

Wala msidhani kuwa mmojawapo akifa katika jamaa yetu kwa ugonjwa huu wa Tauni waweza kuondoa heshima ya ishara hii ya Kiungu. Sababu zamani Nabii Musa na Yoshua na mwishoni Mtume wetu Muhammad, amani ya Mungu juu yake, wote wameamrishwa ya kwamba wawaue wale waliokuwa wakichukua panga zao na kuwaua watu mamia miongoni mwa waaminio; na hii ilikuwa ishara ya Mwenyezi Mungu iliyoonyeshwa na Manabii, ambayo baadaye ukaja ufaulu mkuu upande wa Manabii. Lakini juu ya hayo katika mapigano waaminio wenye haki nao pia walikuwa kwa kushindana na

2 Zakaryia 14:12

3 Mathayo 34:8, Ufunuo 18:8 (Seyidna Ahmad aliandika hapa maneno ya Injili ya Matayo 24:8; lakini katika tafsiri mpya ya Injili ya Luka 21:11. Labda mara nyingine wataliondoa hili pia. Mfasiri).

makafiri wakiuawa kwa panga zao ingawa wachache tu. Basi hesabu kidogo ya namna hii haivunji heshima ya ishara hii ya Mungu. Vivi hivi wakipata Tauni watu wachache kabisa katika jamaa yetu kwa sababu zile tulizotaja juu, basi matokeo ya Tauni ya namna hii hayawezi kabisa kupunguza heshima ya ishara ya Mungu.

Jee! Hii si ishara kubwa kuwa mimi nasema mara kwa mara kila mwenye kutaka haki hatakuwa na shaka yoyote; naye atafahamu ya kuwa Mwenyezi Mungu Amewafanyia wema hawa jamaa Waahmadiyya kwa njia ya kimwujiza. Na kwa sababu ya haya watu wengi wataingia katika jamaa ya Ahmadiyya na watazidi sana kwa hesabu yao, tena wataendelea mbele khilafu ya desturi ya siku zote; na mwendeleo wao utatazamwa kwa kustaajabu, na hii pia itakuwa ishara ya Mwenyezi Mungu. Kama nilivyoandika katika kitabu changu kiitwacho "Nuzulul Masih", ikiwa Mwenyezi Mungu hakupambanua baina ya jamaa Ahmadiyya na mataifa mengine sawasawa na unabii huu, maadui wanaoshindwa kila pahali itakuwa haki yao kunikadhibisha. Ijapokuwa kwa sababu ya kunikadhibisha mpaka sasa wamepata laana moja.

Mathalan, wamepiga makelele mengi mara kwa mara kwamba Atham[4], hakufa katika miezi kumi na tano. Lakini hawaoni ya kwamba ubashiri na unabii ulieleza kwa wazi wazi; "Kama yeye akielekea kwenye haki basi hatakufa kwa muda wa miezi kumi na tano". Ni dhahiri yeye amekwishatubu katika usemi wake aliosema kwamba Mtume wetu Mtakatifu ni Dajjal, mbele ya watu 70 wenye heshima katika mjadala; na akaelekea.

4 Huyu alikuwa ni Padre wa Kikristo aliyeshindana na Seyidna Ahmad (as) kwa siku 15. Siku ya mwisho Seyidna Ahmad alitoa unabii juu ya hali yake (Mfasiri)

Tena si haya tu, bali pia amethibitisha maelekeo yake kwa kunyamaza kwake na kuogopa kwake kwa muda wa miezi kumi na tano. Na sababu hasa ya ubashiri na unabii huu ilikuwa ni kumwita Mtume Muhammad amani ya Mungu juu yake, Dajjal. Kwa hiyo, yeye amepata faida katika kurejea na kuelekea kwake na akafa baada ya miezi kumi na tano. Maana, pia ilisemwa katika ubashiri niliotoa ya kwamba; "Atakayekuwa mwenye imani ya uwongo miongoni mwa hawa mahasimu wawili atakufa mbele", na kwa hivi amekufa kabla yangu.

Hivi ndivyo ulivyo ubashiri na mambo ya ghaibu Aliyoniambia Mwenyezi Mungu nayo yametimia kwa wakati wake; haiwezi kuwa hesabu yao chache kuliko elfu kumi. Lakini katika kitabu changu 'Nuzulul Masih', kinachochapwa, mmeandikwa kwa mfano, bishara 150 tu pamoja na dalili na mashahidi wao. Wala haiwezekani kuonekana katika bishara zangu ubashiri usiokamilika au nusu ya sehemu moja katika sehemu zake mbili. Hata mtu akifa katika kutafuta hawezi kupata bishara iliyotoka katika kinywa changu kwa idhini ya Mwenyezi Mungu isiyotimia; isipokuwa atasema kwa ujinga na ushupavu jinsi anavyotaka. Ninasema kwa yakini kuwa maelfu na maelfu katika bishara zangu zilizotimia sawasawa na zina watu mashahidi maelfu na maelfu na ukitafutwa mfano wake katika Manabii waliotangulia haupatikani ila katika Mtume wetu Muhammad, amani ya Mungu juu yake. Lau kama maadui wangu wangalihukumu kwa njia hii macho yao yangalifumbuka zamani!

Na nilikuwa nimejiweka tayari kuwapa zawadi kubwa lau kama wangalionyesha mfano wa bishara zangu duniani. Lakini kusema kwa shari na upumbavu kuwa bishara fulani haikutimia, tusemeje juu ya jambo hili? Isipokuwa usemi wao ni kwa sababu ya kutudhania vibaya na kwa uchafu wa roho

zao. Lau kama wangalizungumza kwa nia ya kuhakikisha katika mkutano wa watu bila shaka wangalitubu katika kauli yao, au wangalifedheheka. Utimilizo wa maelfu ya bishara za wazi wazi, tena wapo mashahidi walio hai maelfu na maelfu, si jambo dogo bali ni kwa hakika kuwaonyesha Mwenyezi Mungu kwa wazi wazi. Je, alipata kuona mmojawapo zamani pasipo zama za Mtume Mtakatifu, kuwa imetolewa bishara na unabii maelfu na maelfu kisha ukatimia kama mwangaza wa mchana; na maelfu ya watu wakashuhudia juu ya utimizo wao? Mimi najua kwa yakini jinsi Mungu siku hizi anavyodhihiri kwa karibu, na kuyadhihirisha mambo mamia kwa mamia kwa kumfunulia mtumishi wake; hautakuwako mfano wa siku hizi katika siku za kale ila kidogo tu.

Hivi karibuni watu wataona kwamba Uso wa Mwenyezi Mungu Utadhihirika kama Aliyekwisha teremka kutoka mbinguni. Kweli, Yeye Amejificha kwa siku nyingi na Amekataliwa na Akayanyamazia; lakini sasa Yeye Hajifichi. Na dunia itaona uwezo Wake usioonwa na babu zao na wazee wao. Haya yote yatatokea kwa sababu ardhi imeharibika na imani ya watu juu ya Mwumbaji wa mbingu na ardhi imeondoka. Anakumbukwa na kutajwa midomoni tu, lakini mioyo imekuwa mbali naye.

Kwa sababu ya haya Mwenyezi Mungu Amesema katika ufunuo wake kuniambia hivi; “Sasa Mimi nitaumba mbingu mpya na ardhi mpya”. Na maana yake ni kuwa ardhi imekufa; yaani watu wa dunia na mioyo yao imekuwa migumu kama imekwisha kufa. Sababu Uso wa Mwenyezi Mungu umefichama, na ishara Zake zote za zamani zimekuwa kama visa. Kwa hiyo, Mwenyezi Mungu Ameazimia kuumba nchi mpya na mbingu mpya. Mbingu mpya na ardhi mpya ni nini? Fahamuni, ardhi mpya ni mioyo safi anayoifanya Mwenyezi Mungu kwa mkono wake hasa – mioyo ilidhihirika kwa Mungu na Mungu Atadhihirika

kwao. Na mbingu mpya ni ishara zinazodhihiri kwa idhini yake katika mkono wangu mimi niliye mtumishi wake.

Lakini nasikitika kwamba watu wa dunia wamefanya uadui kwa maonyesho haya mapya ya Mwenyezi Mungu. Na mikononi mwao hamna chochote ila visa na hadithi tu. Tena Mungu wao ni matamanio yao na fikara zao tu. Mioyo yao imepotoka na bidii zao zimechoka na macho yao yana vifuniko. Watu wa mataifa mengine, msiwaulize hali yao, maana wao wamemwachilia mbali Mola wao na wakawafanya wanadamu waungu wao; hata na Waislam pia tazameni hali yao jinsi walivyojitenga mbali na Mwenyezi Mungu na wamekuwa maadui hasa wa ukweli na wahalifu wa njia iliyonyoka kama maadui wauaji. Mathalani, watu wa '*Nad'watul-Ulamaa*' wanaojidai kuutetea Uislam na pia watu wa chama cha '*Himayatul Islam*' wa Lahore wanaopokea mali za Waislam kwa jina la Uislam, je, hao wanayo huruma juu ya Uislam? Au je, watu hawa ni wahifadhi wa njia iliyonyooka? Hapana! Hata hawajui Uislam umesagwa chini ya msiba gani na hawafahamu ni desturi gani ya Mwenyezi Mungu kwa Kujadidisha na Kuhuisha dini Yake, Uislam.

Sikilizeni, nasema kweli kweli, lau kama nisingalikuja madai yao ya kuulinda Uislam yangaliwezakana kukubaliwa kidogo; lakini sasa watu hawa wako chini ya lawama ya Mwenyezi Mungu, maana ilipotoka nyota mbinguni hao waliojidai kuulinda Uislam wakawa ndio wao wa kwanza kukataa, basi sasa watajibuje kwa Mungu Aliyenituma kwa wakati hasa? Lakini hawajali kitu wala hawaangalii chochote. Eee, jua limekaribia wakati wa Adhuhuri lakini kwao bado ni usiku! Chemchem ya Mwenyezi Mungu imebubujika na wao bado wanalia jangwani!! Mto wa elimu ya kimbinguni umeporomoka lakini hawana habari nao kabisa!!! Tena si wenye kughafilika tu, bali wao ni maadui wa Jumuiyya ya Mwenyezi Mungu. Je, huu ndio ulinzi wa Uislam

na mafundisho ya Kiislam yanayotangazwa na mikono yao? Lakini je, watu hawa kwa sababu ya uzembe wao, watayazuia maazimio ya Mwenyezi Mungu ya haki, ambayo Manabii wote wameyashuhudia tangu kale? Hasha! Basi unabii na bishara hii iliyofunuliwa na Mungu; "*Kataballahu laaghlibanna anaa warusuliy*" – Amekwisha andika Mwenyezi Mungu kwamba Mimi na Mitume wangu bila shaka tutashinda[5], karibu kutimia.

Kama vile Mwenyezi Mungu alivyodhihirisha, miaka kabla ya leo, ili kumsadikisha mtumishi wake na ukweli wa madai yake, ishara mbili mbinguni kwa kupatwa mwezi[6], na kupatwa jua katika mwezi wa Ramadhani na kuvifanya king'arisha cha mchana na king'arisha cha usiku kuwa vishahidi vyangu. Hivi ndivyo pia alidhihirisha ishara mbili katika ardhi sawasawa na bishara ya Manabii. Na tena ishara moja mnayoisoma katika Quran Takatifu; "*Waidhal 'isharu 'uttilat*" – Na watakapoachwa ngamia[7]; na mnasoma katika Hadithi; "*Layutrakannal qilasu fala yus'aa 'alaiha*" – Na kwa yakini wataachwa ngamia wala hawataendewa juu yao[8]. Na hii ndiyo ishara ambayo kuikamilisha inatengenezwa njia ya reli katika nchi ya Hijaz baina ya Makka na Madina. Na ishara ya pili ni ugonjwa wa Tauni; kama Alivyosema Mungu; "*Wain min qaryatin illa nahnu muhlikuwha qabla yaumil qiyamat*" – hapana mji wowote ila sisi tutauhilikisha kabla ya siku ya Kiyama au tutauadhibu kwa adhabu kali[9]. Kwa hivi Mwenyezi Mungu Ameendesha reli

5 Sura 58 aya 21.

6 "Kwa kuthubutisha ukweli wa Imam Mahdi zitaonekana ishara mbili ambazo hazijatokea tangu kuumbwa mbingu na ardhi. Nazo ni; Mwezi utapatwa katika usiku wa kwanza wa kupatwa kwake katika mwezi wa Ramadhani (tarehe 13). Na jua litapatwa katika usiku wa katikati wa kupatwa kwake katika mwezi huo huo (tarehe 28) (Daru Kutni, uk 188). Haya yalitokea katika mwaka 1894 (Mfasiri)

7 Sura 81 aya 4.

8 Sahihi Muslim.

9 Sura 17, aya 58

katika nchi na akaangusha juu ya watu ugonjwa wa Tauni ili na ardhi iwe shahidi kama mbingu ilivyokuwa shahidi.

Basi msipigane na Mwenyezi Mungu, maana kupigana naye ni upumbavu. Zamani Alipotaka Mwenyezi Mungu kumfanya Adam kuwa '*Khalifa*', malaika walijaribu kumzuia Mungu. Lakini jee, Mungu Aliacha nia yake kwa sababu ya upinzani wao? Sasa pia Mwenyezi Mungu wakati wa kuumba Adamu mwingine amesema; "*Aradtu an astakhlifa fakhalaqtu Adama*"- Nimependa kufanya Khalifa nikamuumba Adamu huyu. Niambieni, je, mnaweza kuzuia azimio la Mwenyezi Mungu? Kwa nini mnatanguliza mambo ya mazoea na kudhani, wala hamchungui njia yenye yakini? Msijitupe majaribioni. Na jueni kwa yakini kuwa hapana mwenye kuzuia maazimio ya Mwenyezi Mungu. Mapigano ya namna hii si njia ya utawa na uadilifu!

Mkiwa na shaka kwa haya ninayoyasema yumkini kushika njia hii. Yaani wapatieni watu wa madhehebu yenu bishara, kwa Mungu, ya kuwaokoa katika ugonjwa wa Tauni; ikiwa ninyi mnawatakia wema na huruma kama mimi nilivyofanya kwa jamii ya watu wanaotii na kufuata amri yangu, na nimepata bishara ya kuwaokoa katika adhabu ya Tauni na nimetangaza kwa magazeti yaliyochapwa; nanyi wabashirieni watu habari njema ya kuwa wao wataepushwa na adhabu ya Mungu ili watu wajue kwamba Mwenyezi Mungu Yu pamoja nanyi. Tena nafasi nzuri pia kwa Wakristo. Sababu wao kila mara wanasema kuwa wokofu ni kwa Yesu. Basi ni faradhi juu yao kuwaokoa Wakristo katika ugonjwa wa Tauni katika siku hizi za msiba.

Na atakayesikilizwa kwa wingi miongoni mwa mataifa haya, huyu ndiye aliyekubaliwa na Mwenyezi Mungu. Basi kila mmoja wao amepewa na Mwenyezi Mungu nafasi ya

kudhihirisha kukubaliwa kwake kwa Mungu, na asigombane bure katika dunia, ili watu wao wahifadhiwe katika Tauni na pia udhihirike ukweli wao. Na hasa ni mapadri wanaofahamu na kusema kwamba Yesu Kristo, mwana wa Mariamu, ni mwokozi wa walimwengu wote, basi kama wao wana yakini mioyoni mwao na kumfahamu mwana wa Mariamu, bwana wa hapa duniani na huko akhera, ni haki juu yao kuonyesha katika kuamini kwao kafara namna ya wokofu. Wakifanya hivi itakuwa wepesi kwa Serikali tukufu pia.

Kama mataifa mbalimbali yanayokaa Bara Hindi, ikiwa wao wana yakini juu ya ukweli wao na ukweli wa madhehebu zao, basi wafanye shauri, ili wakomboe jamaa zao na kuwaokoa katika Tauni; yaani waombe kwa Mola wao wanayemwamini au kwa mwingine wanayemfahamu mungu badala ya Mwenyezi Mungu, awaondoe waliomo katika msiba. Na wachukue kwake ahadi ya kweli kweli na itangazwe katika matangazo kama sisi tulivyotangaza matangazo haya. Na kwa kushika jambo hili itakuwa faida kwa watu na pia itakuwa dalili ya ukweli wa dini yao, tena itakuwa msaada kwa Serikali. Maana Serikali haitaki ila raia zake waokolewe katika balaa na msiba wa ugonjwa wa Tauni kwa njia yoyote.

Mwishoni mkumbuke ya kwamba sisi hatuwakatazi watu wa jamia yetu, wanaokaa katika sehemu mbalimbali ya nchi ya Panjabi na Bara Hindi, kupiga sindano ya Tauni; bali ni wajibu kwa wale waliolazimishwa na Serikali kwa amri ya nguvu; basi ni juu yao kutii amri ya Serikali. Lakini wasiolazimishwa, bali wamo katika hiyari yao na kuachiliwa kufanya kama wanavyotaka, ikiwa wao wamo katika hao wasiofuata mafundisho sawasawa, basi wapigwe sindano vilevile; ili wasiteleze wala wasidanganye watu juu ya ahadi ya Mwenyezi Mungu, Aliyofanya kwa ajili ya wafuasi wangu wafuatao

sawasawa mafundisho, kutokana na hali zao za uharibifu.

Na kama iulizwe kwamba mafundisho gani ambayo yakifuatwa sawasawa yanaweza kumlinda mtu katika machafuko ya ugonjwa wa Tauni? Basi ni haya ninayoyaandika kwa ufupi katika mistari hii michache ifuatayo.

# SURA YA PILI

## Mafundisho yaliyo Bora kabisa.

Jueni kuwa kukiri kwa ulimi tu si kitu mpaka kufuatane pamoja na vitendo kwa nia ya moyo wote. Basi mwenye kutenda vitendo sawasawa na mafundisho yangu anaingia katika nyumba yangu iliyoahidiwa na maneno ya Mungu; "*Inniy uhaafidhu kulla man fi-ddari*" – Mimi Nitamlinda kila aliyomo katika boma la nyumba yako. Isifahamiwe hapa kwamba waliyomo katika nyumba yangu, wao ndio wakaao peke yao katika nyumba yangu ya matofali na udongo; la, bali na wale pia wanaonifuata kwa kweli vile vile wamo katika nyumba yangu ya rohoni. Mambo yawapasayo kufuata ni haya:-

Wakiri kwa yakini kuwa wana Mungu Mmoja, Mwenye Enzi, Aliye imara na Mwumbaji wa kila kitu, ambaye katika sifa zake ni tangu na dawamu wala hazibadiliki. Hakuzaliwa wala Hakuzaa. Naye Ameepukana na kuumwa na kuwambwa msalabani na kufa. Tena Yu karibu juu ya umbali wake, na Yu mbali juu ya ukaribu wake. Ijapokuwa ni Mmoja tu lakini namna za maonyesho Yake ni mbalimbali.

Yanapotokea mabadiliko mageni kwa mwanadamu ndipo Mwenyezi Mungu pia Anakuwa kwa ajili yake mpya, na Anamtendea mema kwa maonyesho yake mapya. Na mtu anaona kwa Mungu mabadiliko vile vile kwa kiasi cha kubadilika kwake. Lakini si muradi wake kuwa yanatokea mabadiliko katika Mwenyezi Mungu; la, bali Yeye tangu kale dhati yake haibadiliki naye yu Mkamilifu kabisa. Lakini wakati anapobadilika mtu kwenye kheri, Mwenyezi Mungu pia Anajidhihirisha kwake kwa maonyesho mapya. Na mwanadamu anapoendelea kwenye wema zaidi Mwenyezi

Mungu pia Humzidishia kumwonyesha maonyesho yake ya Kudra. Mwenyezi Mungu Huonyesha uwezo ulio kinyume cha desturi Yake ya siku zote yanapoonekana mabadiliko makuu katika mwanadamu kinyume cha desturi yake ya siku zote. Na huu ndio msingi wa ishara na uwezo Wake wa namna hii. Mungu huyu ni sharti ya Silsila yetu.

Basi mwaminini na mtangulizeni juu ya mioyo yenu, na juu ya raha yenu, na juu ya kufungamana kwenu kote. Na onyesheni katika njia yake ukweli na kutekeleza kwa vitendo vyenu na ushujaa. Watu wa dunia hawamtangulizi Mungu juu ya jamaa zao na vitu vyao; lakini ninyi mtangulizeni Mungu ili muandikwe mbinguni Jamaa Yake. Kuonyesha ishara za rehema ni desturi ya Mungu toka zamani. Lakini ninyi hamtapata sehemu yenu katika desturi yake hii ila mpaka isibakie umbali baina yenu na Yeye, na kuwa radhi yenu ni radhi Yake, na kupenda kwenu ni kupenda Kwake. Na vichwa vyenu kila wakati na kila hali ya ustawi na kukosa, viwe juu ya kizingiti chake, ili Mungu Atende Atakavyo. Kama ninyi mkifanya hivi Atadhihiri kwenu Mungu yule Aliyeficha uso wake toka zamani. Je! Yuko mmoja wenu mwenye kutenda hivi na awe mwombaji wa radhi yake wala asikasirikie hukumu na kadri yake? Basi baada ya kuona msiba endeleeni mbele kwani hii ni njia ya kukua kwenu. Na kwa kutangaza Umoja Wake duniani jitahidini kwa uwezo wenu wote.

Na rehemuni watu wake wala msiwadhulumu kwa ulimi au kwa njia ya mikono au kwa njia nyingineyo; na jitahidini kuwafanyia watu kheri. Wala msijivune kwa yeyote ijapokuwa ni watu wa chini yenu, wala msitukanane na yeyote hata akikutukaneni, na kuweni wanyonge na wapole na wenye nia nzuri na watakieni wema viumbe ili mkubaliwe.

Ni wengi wanaodhihirisha upole, lakini undani wao ni kama mbwa mwitu, ni wengi walio safi juu lakini ndani yao ni kama nyoka. Basi jilindeni! Hamtokubaliwa na Mungu ikiwa wema wa ndani si sawa. Wakubwa wawarehemu wadogo wala wasiwafedheheshe. Na baada ya kuwa mmekuwa matajiri, watumikieni maskini wala msitakabari juu yao kwa kujipenda. Jiepusheni na njia za maangamio, mwogopeni Mungu siku zote, na mcheni wala msiabudu kiumbe, na jitupeni kwa Mola wenu. Na chukieni dunia siku zote, na kuweni wa Mungu na ishini kwa ajili yake tu. Na kirihikeni, kwa ajili ya radhi yake kila ubaya na dhambi kwa sababu Yeye ni Mtukufu. Inafaa kila asubuhi ishuhudie kuwa mmelala usiku kwa kumuogopa Mungu na kila usiku ushuhudie kuwa ninyi mmeshinda mchana kwa kumcha Mungu.

Msiogope laana ya dunia kwani hiyo inapotea mara moja kama moshi, wala haiwezi kubadilisha mchana uwe usiku. Bali ogopeni laana ya Mungu inayoteremka mbinguni na kuangamiza kila inayemteremkia katika dunia na akhera. Ninyi hamuwezi kujilinda nafsi zenu kwa kujionesha; sababu Mungu ambaye ni Mungu wenu Anaona hata kilicho chini ya mtu. Je, mnaweza kumdanganya? Hapana! Basi ni juu yenu mnyooke, na jitakaseni, na jikuzeni, na tiini. Sikilizeni! Kikibaki kwenu chembe cha giza, basi hicho kitapoteza nuru yenu yote. Na ikiwa katika ubavu wenu wowote kuna kiburi au majisifu au kujipendelea au uvivu, basi ninyi si kitu kinachopasa kukubaliwa. Jihadharini na kujidanganya kwa hayo kidogo mliyo nayo na kufahamu kuwa mmefanya vilivyo vya lazima kuvifanya. Kwani Mungu Anataka yatokee mabadiliko makuu katika nafsi zenu. Na anawatakieni kifo kimoja ambacho baadae Awahuisheni.

Fanyeni suluhu upesi ninyi kwa ninyi na sameheni makosa

ya ndugu zenu, kwani ni mtu wa shari asiyekuwa radhi kufanya suluhu na ndugu yake; yeye atakatwa kwa sababu ya kuachanisha watu. Acheni kabisa matamanio yenu kwa yeyote na acheni hasira zenu mlizo nazo. Nyenyekeeni kama muongo anavyonyenyekea ijapokuwa ninyi ni wakweli, ili mghofiriwe. Na wacheni unene wa mioyo kwani mlango mlikoitwa ndani yake hawezi kuingia aliyekuwa mnene kwa sababu ya makosa yake. Bahati mbaya namna gani kwa mtu asiyeamini maneno yaliyotoka kinywani mwa Mungu nami nimeyabainisha!

Mkitaka Mwenyezi Mungu Awe radhi juu yenu mbinguni, basi kuweni kama ndugu wawili waliozaliwa katika tumbo moja. Mbora wenu ni yule mwenye kusamehe sana makosa ya nduguze, na mwenye bahati mbaya ni yule mshupavu asiyesamehe; basi huyu hana ufungamano nami.

Siku zote ogopeni laana ya Mungu, kwani Yeye ni Mtukufu tena mwenye ari. Muovu hawezi kupata ukaribu kwa Mungu. Mwenye kiburi hawezi kumkaribia. Mdhalimu hawezi kumkaribia. Haini hawezi kumkaribia. Na kila asiye na ghera kwa jina lake hawezi kumkaribia, na wale wanaoangukia dunia kama mbwa na sisimizi na mbesi na wanafurahia dunia hawawezi kumkaribia. Kila jicho baya liko mbali naye, na kila moyo mchafu hauna habari naye. Atakayekuwa katika moto kwa ajili ya Mungu ataokolewa katika moto. Mwenye kulia kwa sababu ya Mungu atakuja cheka. Na mwenye kuacha dunia atakutana Naye. Kuweni wapenzi wa Mungu kwa ukweli wa mioyo yenu, na kwa shauku sana, na kwa hamu nyingi ili Mungu pia Awe mpenzi wenu. Rehemuni walio chini yenu na wake zenu na walio maskini katika ndugu zenu, nanyi mtarehemiwa mbinguni vilevile. Kuweni wa Mungu ki kwelikweli Naye Atakuwa wa kwenu. Dunia ni mahali pa maelfu ya mabalaa; pia Tauni ni moja kati ya hayo, basi mshikeni Mwenyezi Mungu

sawasawa ili Yeye Ayatenge mbali mabalaa haya. Halitokei balaa lolote ardhini mpaka kwa amri Yake ya mbinguni. Wala balaa haliondoki mpaka iteremke rehema kutoka mbinguni. Kwa hivyo, akili zenu ziwe katika kukamata shina wala siyo matawi. Hamkukatazwa kutumia dawa, bali mmekatazwa kutawakali juu ya dawa. Na mwishoni yatatokea Anayotaka Mwenyezi Mungu. Lakini kama mmoja wapo anaweza kushika jambo la kutawakali ni bora kuliko mambo yote.

Na mafundisho mengine yaliyo wajibu kwenu ni kuwa msiiache Quran Tukufu ovyo, kwani katika Quran tu umo uzima wenu. Watakaoiheshimu watapata heshima mbinguni. Na watakaotanguliza Quran Tukufu kuliko hadithi zote na maneno yote, wao watatangulizwa mbinguni. Sikilizeni! Na sasa hapana kitabu chochote kitakachoweza kuongoza mwanadamu juu ya ardhi ila Quran Tukufu. Na hapana Mtume wala Muombezi mwingine wa mwanadamu ila Mtume Muhammad, amani ya Mungu juu yake, kwa hiyo jitahidini mumpende kwa mapenzi kweli kweli Mtume huyu, Mtume wa heshima na utukufu. Na wala msimuheshimu mtu yeyote kuliko yeye ili muandikwe mbinguni pamoja na waliookoka. Na jueni kuwa kuokoka si kitu kinachoonekana baada ya kufariki; bali kuokoka hasa ni kule kunakoonyesha nuru yake hapa duniani.

Ni nani aliyeokolewa? Aliyeokolewa ni yule mwenye yakini kuwa Mwenyezi Mungu kweli yupo na Mtume Muhammad, amani ya Mungu juu yake, ni muombezi katikati ya Mungu na viumbe vyote. Na kuwa hapana Nabii yeyote aliye sawasawa na Mtume Muhammad, amani ya Mungu juu yake; na kuwa hapana kitabu chochote sawa na Quran Tukufu chini ya mbingu. Na Mungu Hakupenda kwa yeyote awe mzima wa milele ila kwa Mtume huyu Mtukufu aliye ni mzima wa milele. Yaani Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kumuweka mzima wa

milele Amefungua chemchem ya sheria yake na mibaraka ya utukufu wake kuendelea mpaka siku ya Kiyama. Na mwisho kwa baraka ya utukufu wake Amemtuma duniani *Almasih-il-Mau'ud* (Masihi Aliyeahidiwa), ambaye kuja kwake kulikuwa ni lazima kwa kukamilisha jengo la dini ya Kiislam. Maana ilikuwa ni lazima kwamba dunia hii isiishe mpaka aje Masihi mmoja, aliye kwa asili ya rohoni, mfano wa Nabii Isa (as), katika umati wa Muhammad, amani ya Mungu juu yake, kama ulivyopewa umati wa Musa (as).

Na aya hii ya Quran Tukufu; '*Ihdiinassiratal mustaqiym siratalladhiyna an'amta' alaihim*' – Utuongoze katika njia iliyonyooka, njia ya wale uliowapa neema, inadhihirisha jambo hili. Na Musa (as) alipata mambo yaliyopotezwa na watu wa zamani; na Muhammad, amani ya Mungu juu yake alipata mambo yaliyopotezwa na watu wa Nabii Musa (as). Na Silsila ya Muhammad, amani ya Mungu juu yake, ilishika pahala pa Silsila ya Mussa (as). Lakini Silsila ya Muhammad, amani ya Mungu juu yake, ilizidi kuwa na fadhila nyingi kuliko Silsila ya Musa (as). Mfano wa Musa, (Muhammad amani ya Mungu juu yake) ni bora kuliko Musa; na mfano wa Nabii Isa, (Seyidna Ahmad as) ni bora kuliko Nabii Isa (as). Na yule Masihi Aliyeahidiwa si kwamba yeye alitumwa katika karne ya kumi na nne baada ya Mtume, amani ya Mungu juu yake[10] kama alivyotumwa Isa bin Mariamu katika karne ya kumi na nne baada ya Nabii Musa tu; bali amekuja wakati ule hali ya Waislam ilipokuwa kama hali ya Mayahudi wakati wa kutumwa kwake Isa bin Mariamu; na yule aliyeahidiwa kufika kwake katika siku hizi za mwisho ni mimi. Mungu Hufanya Apendavyo. Ni mpumbavu anayepigana na Mungu, na ni mjinga anayeleta hoja na kusema mbele yake;

10 Mayahudi wanakubali kwamba Nabii Isa amedai utume baada ya Nabii Musa zilipopita karne kumi na tatu na kuanza karne ya kumi na nne. Tazameni katika hisroria ya Mayahudi.

“Siyo hivi bali inafaa hivi”. Na Mwenyezi Mungu Amenituma pamoja na ishara zenye kung’aa zaidi ya elfu kumi. Na moja yao pia ni Tauni. Basi anayefungamana na mimi ki kweli kweli, na anakuwa mfuasi wangu kwa nia safi na kujiweka katika kunitii kwa moyo wote na kujiepusha na matamanio yake yote; huyu ndiye atakayeombewa na roho yangu katika siku hizo za mabalaa.

Basi enyi watu wote mnaojihesabu katika jamaa yangu! Hamtahesabiwa mbinguni katika jamaa yangu mpaka mtembee katika nyayo za utawa kweli kweli. Simamisheni sala zenu tano kwa unyenyekevu na upole wa moyo kama ni wenye kumuona Mwenyezi Mungu. Na kamilisheni sawasawa saumu zenu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Na kila anayewajibika kutoa Zaka na atoe. Na mwenye kuwajibika kuhiji, wala hakuna kinachomkataza, basi na ahiji kwenye Kaaba. Fanyeni wema kwa vizuri na acheni mabaya kwa kuyachukia. Jueni kwa yakini kuwa hakifai kabisa kitendo kisicho na utawa. Utawa ni shina la kila wema. Kitendo kisichopoteza shina hili hakitopotezwa. Ni wajibu kwenu kujaribiwa kama waaminio wa kwanza.

Kwa hiyo jitahadharini ili msiteleze. Ardhi haiwezi kuwadhuruni hata kidogo ikiwa mmefungamana sana na mbingu. Na kama ikiondolewa heshima yenu yote ya duniani, Mungu Atawapeni heshima ya milele mbinguni, basi kwa hiyo msimwache kabisa. Hapana budi kuwa mtaudhiwa na mtaepushwa na matumaini mengi, basi msiyahuzunikie hayo kabisa. Kwani Bwana wenu Mungu Anawajaribuni ili Ajue kuwa mmekazania njia Yake au hapana? Ikiwa mnapenda kusifiwa na malaika pia mbinguni, basi furahini mnapopigwa na shukuruni mnapotukanwa wala msikate kufungamana mnapoyakosa matumaini yenu kwa sababu ninyi ni katika Jumuiya ya Mwisho ya Mwenyezi Mungu; basi onyesheni vitendo vyema vitakavyokuwa bora sana. Jueni

kuwa katika ninyi kila atakayekuwa mvivu atatupwa nje ya Jamaat kama kitu kibaya na atakufa kwa huzuni wala hataweza kumdhuru Mungu chochote.

Tazameni mimi nawaambieni kwa furaha kubwa kuwa kweli Bwana wenu Mungu yupo! Na ingawa viumbe vyote ni viumbe vyake, lakini Mungu Anamchagua yule mwenye kumchagua Mungu. Na Anamkaribisha yule anayekwenda karibu Yake. Na mwenye kumheshimu Naye pia humpa heshima.

Njooni Kwake Mwenyezi Mungu baada ya kunyoosha mioyo yenu na baada ya kutakasa ndimi zenu na macho yenu na masikio yenu. Na Yeye Atawakubalini. Ama kwa shauri la imani ya Mwenyezi Mungu; Anawatakeni mwamini kuwa Mungu ni Mmoja na Muhammad, amani ya Mungu juu yake ni Mtume Wake. Tena ni '*Khatamul-Anbiya*' – Muhuri wa Manabii, na ni mbora kuliko wote. Wala hapana Nabii baada yake ila yule aliyevalishwa shuka la Muhammad, amani ya Mungu juu yake kwa njia ya mfano. Kwani mtumishi si mbali na bwana wake wala tawi haliko mbali na shina lake. Basi kwa hivyo mwenye kujitoa kwa kumfuata kweli kweli bwana wake anapata kwa Mungu jina la Nabii, na yeye havunji *U-Khatamun-Nubuwwat*. Kama vile mnapojitazama katika kioo hamuwezi kuwa wawili bali ni peke yako na ikionekana kwako wawili hapana tofauti baina yao ila tofauti ya kivuli na asili. Hivyo ndivyo Mwenyezi Mungu Alivyotaka kwa Masihi Aliyeahidiwa. Na kwa ajili ya siri hii amesema Mtume Mtukufu, amani ya Mungu juu yake; "Masihi Aliyeahidiwa atazikwa katika kaburi langu, yaani yeye ni kama mimi wala hayakumtokea mabadiliko kinyume cha nilio nayo.

Tena jueni kwa yakini kuwa Isa mwana wa Mariamu amekwishafariki na kaburi lake lipo katika mtaa uitwao

*Khaniyar*[11], katika Srinagar, Kashmir – bara Hindi. Na Mwenyezi Mungu Ameeleza kifo chake katika kitabu chake Kitukufu cha Quran. Someni aya hii; '*Falammaa tawaffaitaniy kunta antar –raqiba'alaihim*' Basi uliponifisha wewe ukawa mlinzi wao[12]. Na ikiwa maana yake aya hii ni nyingine, basi iwapi habari ya kufariki kwake katika Quran Tukufu? Ikiwa aya zilizoonyesha kifo chake zina maana nyingine kama wanavyofahamu maadui zetu basi maana yake Quran haikutaja kifo chake pahali popote kwamba yeye atakufa au hafi? Ni ajabu Mwenyezi Mungu Ameeleza habari za kufariki kwake Mtume wetu Muhammad, amani ya Mungu juu yake, lakini katika Quran nzima asieleze habari za kifo cha Nabii Isa bin Mariamu! Siri gani iliyomo ndani yake? Mkisema kuwa kifo cha Isa kimetajwa katika aya hii; "*Falammaa tawaffaitaniy kunta antar-raqiba'alaihim*" – Uliponifisha ukawa wewe ni mlinzi wao[13], aya hii inaonyesha kwa wazi wazi kuwa yeye amekufa kabla ya uharibifu wa Wakristo. Na kama maana ya aya hii ni kuwa Mungu Amemrufaisha Isa mbinguni mzima na kiwiliwili chake, basi kwa nini Mwenyezi Mungu Hakutaja kifo cha mtu ambaye uzima wake umewaangamiza watu maelfu na maelfu? Na Mwenyezi Mungu Amemweka mzima ili watu wawe mushrikina na wapotevu; ikiwa ni hivyo basi si makosa ya watu bali Mungu Mwenyewe Ameyafanya ili Awapoteze watu! Mkumbuke haiwezekani kuvunjika imani ya msalaba mpaka kihakikishwe kifo cha Masihi, mwana wa Mariamu.

---

11 Wanazuoni wa Kikristo wameonesha jambo hili, tazameni uk.522 katika kitabu "Super natural religion". Na mkitaka maelezo Zaidi tazameni uk.139 katika kitabu changu "Tohofa Golarwiya".

12 Sura 5, aya 118.

13 Sura 5, aya 118. Na inadhihirika katika ayah ii kuwa Nabii Isa haji duniani mara nyingine. Kwani lau kama angalirudi duniani jibu lake ya kuwa hajui upotevu wa Wakristo lingekuwa uwongo. Maana mtu aliyerudi duniani mara nyingine na kukaa miaka 40 na kuona maelfu na maelfu ya Wakristo wanamwita Mungu, na akavunja misalaba na kusilimisha Wakristo wote, anawezaje kusema mbele ya Mungu siku ya Kiyama kuwa yeye hajui uharibifu wa Wakristo?

Basi ni faida gani kudhania nabii Isa kuwa yu hai khilafu ya mafundisho ya Quran Tukufu? Acheni afe ili dini hii ya Kiislam ihuishwe. Mwenyezi Mungu amedhihirisha kifo cha nabii Isa kwa kauli yake. Na Mtume, amani ya Mungu juu yake, amemwona nabii Isa katika wafu usiku wa Miiraji. Pia bado hamjaamini? Imani hii ni imani gani? Je! Mnatanguliza masimulizi ya watu juu ya maneno ya Mungu? Dini hii ni dini gani[14]? Tena si kuwa Mtume wetu Muhammad, amani ya Mungu juu yake, ameshuhudia tu kwa kumwona nabii Isa katika wafu; bali amethibitisha kwa kufariki kwake mwenyewe kuwa hakuwa yeyote kabla yake aliyeishi milele. Basi maadui zetu kama wanavyoacha Quran wanaacha Sunna vile vile; kwani mauti ni sunna ya Mtume wetu. Ikiwa nabii Isa yu hai basi kifo cha Mtume wetu ni fedheha kwake! Hakika ninyi hamuwi Ahlu Sunnat wala Ahlul Quran mpaka mwamini kifo cha nabii Isa.

Na mimi sikatai utukufu wa nabii Isa. Ingawa nimeambiwa na Mwenyezi Mungu kuwa Masihi wa Muhammad, amani ya Mungu juu yake, ni bora kuliko Masihi wa Musa. Lakini pamoja na haya namheshimu sana Masihi bin Mariamu, kwani mimi ni *Khatamul Khulafa* wa Kiislamu kwa asili ya roho kama alivyokuwa Nabii Isa *Khatamul Khulafa* katika umati wa Israeli. Kama mimi nilivyo Masihi Aliyeahidiwa katika umati wa

---

14 Aya moja katika Quran imeonyesha kwa wazi wazi kuwa Masihi na mama yake walikwenda nchi ya Kashmiri baada ya kutoka msalabani. Kama alivyosema Mungu; "Wa-aawainaahumaa ilaa rab'watin dhati qaraarin wamai'yn" – Sisi tumempa Isa na mama yake pahali pa raha palipoinuka na maji safi. Yaani maji ya chem chem (a). Katika aya hii Mwenyezi Mungu Ameeleza namna ilivyo nchi ya Kashmir. Na tamko la 'Aawaa' linatumika kwa Kiarabu kwa maana ya kujiponya katika msiba na taabu, na hazikupita zama za taabu na msiba kwa nabii Isa na mama yake kabla ya kusulubiwa, jambo lililotakiwa kuponywa. Basi hakika ni hii kuwa Mwenyezi Mungu Amewapeleka Isa na mama yake baada ya kusulubiwa kwenye kilima hiki yaani kilima cha Kashmiri.

(a) Sura 23 aya 51

Muhammad, amani ya Mungu juu yake, vivi hivi mwana wa Mariamu alikuwa Masihi Aliyeahidiwa katika umati wa Musa. Kwa hivi mimi namheshimu yule aliye ni wa jina langu. Na ni mfisadi na mwongo anayesema kuwa simheshimu. Acheni Masihi hata ndugu zake wanne nawaheshimu kwa sababu wote watano walitoka tumbo moja. Na zaidi ya haya nawaheshimu dada zake wawili kwa sababu hawa wote ni watakatifu wametoka katika tumbo la Mariamu bikira[15]. Na utukufu wa Mariamu aliyejizuia nafsi yake wala hakuolewa mpaka muda mrefu, na baadaye kwa sababu ya kulazimishwa na wakubwa wa jamaa zake kwa ajili ya mimba, akaolewa.

Kweli, ingawa, watu wanabishana kwa kusema kwa nini Mariamu kuolewa alipokuwa na mimba hilafu ya mafundisho ya Torati, na kuvunja ahadi ya ubikira, na kwa nini ikawekwa desturi ya kuoa zaidi ya mwanamke mmoja? Yaani ilipokuwa kwa Yusufu Seremala alipokuwa tayari ana mkewe wa kwanza, kwa nini Mariamu akakubali kuolewa na Yusufu. Lakini mimi nasema haya yote yalikuwa kwa shida iliyompata, na kwa hiyo anatakiwa kuhurumiwa sio kulaumiwa.

Baada ya maneno yote haya nasema mara nyingine, msidhani kuwa mmekiri dhahiri, kwani kukiri dhahiri si kitu. Mwenyezi Mungu Anatazama mioyo yenu na roho zenu, na Atawatendeeni sawa na hali ya mioyo yenu.

Tazameni! Mimi natimiza faradhi ya kubashiri baada ya kusema haya kuwa; “Dhambi ni sumu msiile. Kumwasi Mwenyezi Mungu ni kifo kibaya, kiogopeni. Ombeni ili mpewe nguvu.

15 Yesu Masihi alikuwa na ndugu zake wanaume wanne na dada zake wawili; wote hao ni watoto wa Yusuf na Mariamu. Majina ya ndugu zake ni haya: 1. Yahuda, 2. Yaakub, 3. Shamuun, 4. Yuzus. Na majina ya dada zake wawili ni haya: 1. Asiya, 2. Lediya. Tazameni kitabu kiitwacho ‘Apostolic Records’ ukurasa 159, 166. Kimeandikwa na Padri Jan Elen Gailz, kimechapwa London katika mwaka 1886.

Sikilizeni, mtu asiyemfahamu Mwenyezi Mungu kuwa ana uwezo juu ya kila kitu wakati wa kuomba kwake hayumo katika jamaa yangu. Yule mtu asiyeacha uongo na udanganyifu, huyo hayumo ndani ya jumuiya yangu. Mtu asiyetanguliza dini, juu ya dunia, kweli kweli hayumo katika jamaa yangu. Mtu asiyeacha kila kitendo kibaya kama kunywa pombe na kucheza kamari na kutazama wanawake na kuzini na hiyana na rushwa, na kila jambo lisilojuzu kutenda na asiyetubia kutubu kwa kweli, hayumo katika jamaa yangu.

Mtu asiyedumu katika kusali sala tano siku zote hayumo katika jamaa yangu. Mtu asiyeshughulika katika kuomba kwa daima, wala hamkumbuki Mwenyezi Mungu siku zote kwa unyenyekevu, hayumo katika jamaa yangu. Mtu asiyeacha rafiki mbaya mwenye kumwingiza mambo mabaya moyoni mwake hayumo katika jamaa yangu. Mtu asiyewaheshimu wazazi wake wala asiyezitii amri zao maarufu, zisizo kinyume cha Quran Tukufu, wala hawatumikii kwa haki, hayumo katika jamaa yangu. Mtu asiyemfanyia wema mke wake na jamaa za mke wake kwa upole na ihsani hayumo katika jamaa yangu. Mtu mwenye kumnyima jirani yake hata kheri kidogo, hayumo katika jamaa yangu. Mtu asiyetaka kumsamehe mwenye kumkosea na mwenye kumbughudhi hayumo katika jamaa yangu. Kila mume mwenye kufanya hiyana kwa mke wake na kila mke mwenye kufanya hiyana kwa mume wake, hayumo katika jamaa yangu.

Mtu avunjaye ahadi aliyoahidi wakati wa kukiri na kuingia katika jamaa Ahmadiyya, kwa sababu yoyote, hayumo katika jamaa yangu. Mtu asiyeamini kwa kweli kuwa "*mimi ni Masihi na Mahdi Aliyeahidiwa*", hayumo katika jamaa yangu. Mtu asiyejiweka tayari kunitii katika mambo maarufu, hayumo katika jamaa yangu. Mtu anayekaa pamoja na watu walionikataa

na kukubali maneno yao ya upinzani hayumo katika jamaa yangu. Na kila mzinzi, fasiki, mlevi, mwuaji, mwizi, mcheza kamari, haini, mla rushwa, mnyang'anyi, mdhalimu, mwongo, mhadaa na mwenye kukaa na watu hawa wote, na mwenye kuwasingizia ndugu zake na dada zake na asiyeacha vitendo vyake vibaya, wala asiyeacha kukaa na watu wabaya, hayumo katika jamaa yangu.

Kumbukeni kuwa haya yote ni sumu na baada ya kuzila sumu hizi hamuwezi kusalimika. Nuru na giza haiwezekani kukusanyika pahali pamoja. Kila mtu mwenye tabia yenye kujikunja, wala si safi kwa Mwenyezi Mungu, hawezi kupewa baraka inayopewa wenye mioyo safi. Bahati gani nzuri ya wale wanaosafisha mioyo yao na kutakasa roho zao na kila uchafu na kufunga na Bwana wao Mwenyezi Mungu ahadi ya uaminifu! Hawatapotezwa kabisa!! Haiwezekani Mungu Kuwafedhehesha sababu wao ni wa Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu ni wa kwao. Nao wataepushwa na kila balaa. Ni mpumbavu adui yule ambaye awakusudia ubaya, kwa sababu wao wanabebwa na Mungu, yaani wamo katika ulinzi Wake.

Ni nani aliyemwamini Mwenyezi Mungu? Ni wale tu watakaokuwa kama hawa; Na vile vile ni mpumbavu yule anayefikiri kumtia udhia mtu mjeuri, mwenye dhambi, mbaya wa roho na mwenye nafsi ya shari; kwani yeye mwenyewe ataangamia. Tokea Mwenyezi Mungu Kuumba mbingu na ardhi hata siku moja Hajawaangamiza watu wema na Kuwahilikisha au kuwafuta kabisa. Bali tangu zamani Huonyesha ishara Zake hata sasa. Yeye Mungu ni Mungu Mwaminifu na zinadhihirika ishara za ajabu kwa waaminifu wake. Watu wa dunia wanataka kuwaangamiza na kila adui anataka kuwahilikisha. Lakini aliye ni rafiki yao Anawalinda katika kila pahali pa maangamizo na Anawapa ustawi na ufaulu katika kila matokeo.

Bahati gani nzuri ya yule asiyeacha kamba ya Mwenyezi Mungu! Tumemwamini na tumemjua. Hakika Yeye ni Mungu wa walimwengu wote ambaye Amenifunulia na Ameonyesha kwa ajili yangu, ishara zilizo kubwa, Naye Ndiye Aliyenituma siku hizi niwe Masihi Aliyeahidiwa. Wala hapana Mungu mwingine ardhini wala mbinguni isipokuwa Yeye. Asiyemwamini amenyang'anywa bahati njema na ameshikwa na udhaifu. Tulipata ufunuo wa Bwana wetu Mwenyezi Mungu unaong'aa kama jua. Na tumeona ya kuwa Yeye ndiye Mungu wa dunia yote wala hapana Mungu mwingine ila Yeye tu. Nguvu zilioje za Yule tuliyemkuta na Mmiliki wa uwezo ulioje tuliyemwona! Kweli ni hii kuwa; hapana kitu kisichokuwa katika uwezo Wake; ila kile kilicho khilafu ya Kitabu Chake na khilafu ya ahadi Yake.

Basi mwombapo msiombe kama watu wategemeao vitu vya duniani na wanakuwa wajinga na uwezo wa Mungu, wao wametengeneza kanuni ya viumbe wenyewe ambayo haikusadikishwa na kitabu cha Mungu. Hakika wao wamekasirikiwa, na dua yao haikubaliwi. Wao ni vipofu si wenye macho, wafu si wazima. Wanaweka mbele ya Mwenyezi Mungu kanuni waliyoifanya wenyewe na wanapima kwa kiasi chao uwezo wa Mungu usioweza kuhesabika wala kukusanywa; na wanafahamu kuwa Mwenyezi Mungu ni dhaifu. Basi wanatendewa na Mungu kama hali yao. Lakini unaposimama wewe kusali na kuomba ni wajibu kwako kumfahamu Mungu wako Ana uwezo juu ya kila kitu; ukifanya hivi dua yako itakubaliwa na wewe utaona ajabu ya uwezo wa Mungu kama sisi tulivyoona. Na kushuhudia kwetu ni kwa kuona si namna ya masimulizi. Itakubaliwaje dua ya yule mtu, na itakuwaje moyo wake kupata ushujaa wa kuomba dua wakati taabu kubwa inapomfikia, anayeifahamu kuwa ni kinyume cha kawaida na

asiyeamini kuwa Mungu ana uwezo juu ya kila kitu?

Lakini ewe mtu mwema! Wewe usifanye hivi, maana Mola wako ni Yule Aliyezitundika nyota zisizohesabika bila nguzo na Aliyeumba mbingu na ardhi bila chochote. Je, wewe unamdhania vibaya kuwa Yeye Atashindwa na haja yako?[16] Hasha! Bali utakosa kupata bahati yako kwa sababu ya dhana yako mbaya. Ajabu za Mungu wetu ni nyingi wala hazihesabiki, lakini wanaweza kuziona wale waliojitoa kwa Mwenyezi Mungu kwa ukweli na uaminifu. Yeye Hazionyeshi ajabu Zake kwa watu wasioamini uwezo Wake, wala watu wasio waaminifu wa kweli. Bahati gani mbaya ya mtu yule asiyejua kuwa ana Mungu Mmoja Mwenye uwezo juu ya kila kitu! Hakika pepo yetu ni Mungu wetu na ladha yetu yote ni kwa Mola wetu. Sababu sisi tumemwona na tumeukuta kila uzuri ndani Yake. Inafaa kujipatia hazina kama hii hata kwa kutoa roho. Na inafaa kununua almasi hii hata kwa kutoa uzima wote. Enyi wenye bahati ndogo! Kimbilieni upesi kwenye chemchem hii ambayo itawanyweshení! Ndiyo chemchem ya uzima itakayowalindeni! Nifanye nini na niingize namna gani mioyoni mwenu maneno haya ya furaha? Kwa ngoma gani ninadi katika masoko kuwa Mola wenu ni Huyu ili watu wasikie? Na niwape dawa gani ili masikio ya watu yafunguke na yasikie?

16 Mwenyezi Mungu hashindwi na kazi yoyote. Kweli kitabu cha Mwenyezi Mungu kimeeleza sharia juu ya dua; ya kwamba Mwenyezi Mungu anamtendea mtu mwema kwa huruma nyingi na urafiki. Yaani baadhi ya wakati huacha shauri lake na hupokea maombi ya mtumishi wake, kama alivyosema; "Ud'uwni astajib lakum" – Niombeni nitakupeni (a). Na baadhi ya wakati humtaka mtumishi wake alifuate shauri lake. Kama alivyosema; 'Walanabluwannakum bishai-in minal khauf waljuw-I' – Na tutawajaribuni kwa mambo ya hofu na njaa (b). Na amefanya haya ili amzidishe mtumishi wake katika yakini na maarifa, kwa kusikiliza maombi yake, na ili amzidishe mtumishi wake katika cheo na mwongozo na zawadi ya radhi yake kwa kumfanya alitii shauri lake.

(a) Sura 40 aya 61
(b) (b) Sura 2 aya 156

Kama ninyi mtakuwa wa Mungu, fahamuni kwa yakini kuwa Mwenyezi Mungu pia Atakuwa wa kwenu. Mkiwa mmelala, Mwenyezi Mungu Atawalindeni. Mkiwa mmeghafilika juu ya adui zenu Mwenyezi Mungu Atawaangalieni na Atavunja hila zao. Mpaka sasa hamjajua uwezo wa Mungu wenu, lau kama ninyi mngalijua haya isingetokea siku yoyote ninyi kuhuzunikia dunia yenu. Mtu mwenye hazina akipoteza pesa moja analia au anapiga kelele au anajiangamiza? Basi lau kama mngalijua habari za hazina hii, ya kwamba Mungu wenu Anaweza Kuwasaidieni katika kila wakati wa haja, msingalihangaika kuipenda dunia. Mwenyezi Mungu ni hazina ipendwayo, iheshimuni. Yeye ndiye Msaidizi wenu katika kila mahali. Ninyi si kitu pasipokuwa Yeye, wala vitu vyenu wala hila zenu.

Msifuate mataifa yaliyoangukia na kutawakali juu ya vitu na hila zao. Wao wamekula udongo wa vitu vya dunia kama nyoka anavyokula udongo. Na kama mbwa na mbesi wanavyokula nyamafu, hivi ndivyo wao wameuma nyamafu. Wamekuwa mbali sana na Mwenyezi Mungu! Wamewaabudu watu na wamekula nguruwe na wametumia pombe kama maji. Na wamehilikishwa kwa sababu ya kuangukia kwao kwenye vitu na kuacha kuomba nguvu kwa Mungu.

Na roho ya mbinguni imeruka kutoka kwao kama njiwa anavyoruka kutoka katika kiota. Katika mioyo yao mna ukoma wa kuipenda dunia, uliovikata viungo vya ndani yao vyote. Basi jihadharini na ugonjwa huu! Mimi siwakatazeni kutumia vitu, bali nawakatazeni msiwe kama mataifa mengine waliokuwa watumwa wa vitu tu, na kumsahau anayeumba vitu kama anavyoumba viumbe vingine. Lau kama mnayo macho mngaliona kuwa hapana kitu chochote ila Mwenyezi Mungu tu. Wala hamwezi kunyosha mikono yenu wala hamwezi kuikunja

ila kwa idhini Yake. Mfu wa roho atalicheka, laiti angalikufa ingalikuwa bora kuliko kucheka kwake!

Jihadharini! Msifuate mataifa mengine baada ya kuona hali yao kwamba wao wameendelea mbele katika hila yao ya dunia, kwa hiyo na sisi pia tuwafuate nyayo zao, hapana! Sikilizeni na fahamuni, kwamba wao hawamfahamu Mwenyezi Mungu Yule Anayewaiteni kwake, maana wamemsahau. Je, mnajua Mungu wao ni nani? Hakuwa ila ni mtu dhaifu! Kwa hivi wametumbukizwa katika kughafilika. Mimi siwakatazeni kuchuma na kutafuta manufaa ya dunia; lakini ninawaambieni kuwa msiwafuate wale wanaofahamu kuwa dunia ni peke yake. Bali ni lazima juu yenu kumwomba Mungu Mwenyezi ili Awapeni nguvu siku zote katika kila kitendo, kama ni kitendo cha dunia au kitendo cha dini. Mwombeni uwezo na nguvu siku zote, si kwa midomo tu, bali inafaa kwenu kuamini kwa yakini kwamba, baraka zote zinatoka mbinguni tu. Mtakuwa wakweli mtakaposhika njia hii, yaani katika kila kitendo na kila taabu, kabla ya kushika shauri lolote, fungeni mlango wenu na kiangukieni kizingiti cha Mwenyezi Mungu na ombeni kwake kwa unyenyekevu; Ee Mola wetu, tumepata taabu hii, kwa fadhili zako tuondolee. Ndipo roho takatifu itateremka kwenu kuwasaidieni na wakati ule mtafunguliwa njia ya msaada kwa siri. Jirehemuni nafsi zenu wala msiwafuate wale waliokataa kufungamana na Mungu na kuangukia vitu vya dunia hata hawasemi *Inshallah* (Mungu Akipenda) kwa kupata nguvu.

Mwenyezi Mungu Ayafumbue hasa macho yenu ili mjue kuwa Mungu wenu Ndiye nguzo za mashauri yenu yote; na kama nguzo zikianguka, jee paa linaweza kukaa? La, bali litaanguka mara moja, na inayumkinika kuwaua watu wengi. Hivi ndivyo haiwezekani kuendelea na mashauri yenu sawasawa bila msaada wa Mwenyezi Mungu. Na kama ninyi hamtaomba

msaada kwake, wala hamtafanya desturi zenu kuomba uwezo kwake, hamtapata ufaulu kabisa. Na mwishoni mtakufa kwa majuto makubwa.

Msidanganywe kuwa kwa nini mataifa mengine, wasiomjua Mungu ambaye ndiye Mungu wenu Mkamilifu na Mwenye uwezo, wanaendelea mbele na kustawi? Majibu yake ni haya; kuwa mataifa haya kwa sababu ya kumwacha Mwenyezi Mungu, wameingizwa katika mtihani wa dunia. Mtihani wa Mungu baadhi ya wakati unakuwa hivi; yaani anayemwacha Mungu na kupenda utamu na ladha ya dunia na matamanio yake, na anataka mali ya dunia; basi anafunguliwa milango ya mali ya dunia na anakuwa tajiri; lakini katika dini anakuwa maskini na mtupu kabisa, na mwisho wake anakufa katika mazoea ya dunia na kutupwa motoni. Lakini wakati mwingine mtihani unakuwa hivi ya kuwa, ananyang'anywa katika dunia pia na hapati chochote. Lakini mtihani wa namna hii hauna maumivu sana kama mtihani wa kwanza, kwani mwenye mtihani wa kwanza anakuwa na kiburi sana kuliko mwenye mtihani wa pili. Lakini pamoja na haya, hawa wote wawili wanakasirikiwa na Mungu. Kwa sababu Mwenyezi Mungu ni chemchem ya hali ya furaha ya kweli kweli. Ikiwa wao wanamsahau Mungu, Aliye Mzima wa milele, na si haya tu, bali pia hawamjali na wanatengana Naye, itayumkinikaje kwao kupata hali ya furaha ya kweli? Hubarikiwa anayeifahamu siri hii na huangamizwa asiyeifahamu siri hii.

Vile vile mnatakiwa msishike njia ya wanafalsafa (philosophers) wa kidunia wala msiwatazame mtazamo wa heshima, kwani dhana zao zote ni za kipumbavu. Hekima ya kweli ni ile Aliyowafundisheni Mwenyezi Mungu katika maneno yake. Wamekwishaangamia wale wenye kupenda hekima ya kidunia na wamestawi wale wenye kutafuta elimu ya kweli na

hekima katika kitabu cha Mungu. Kwa nini mnachagua njia za upumbavu? Je, mnamfundisha Mungu Asiyoyajua? Lakini hekima ya kweli mlioahidiwa inapatikana kwa roho takatifu. Ninyi kwa msaada wa roho takatifu, mtafikishwa kwenye elimu yenye kuchipusha moyo na kuuhuisha na kuufikisha kwenye mnara wa yakini. Anayekula nyamafu atawaleteeni wapi chakula chema? Na mwenye kuwa kipofu atawezaje kuwaongozeni? Kila hekima tukufu inatoka mbinguni, basi mnatafuta nini kwa hao watu wa ardhini? Hakika hao waendao na roho zao mbinguni wamekuwa warithi wa hekima. Unatakiwa utakasifu wa moyo, na ukweli na kujitakasa – baada ya haya yote, hekima ya kweli na elimu tukufu na utulivu mtapata.

Sikilizeni! Msidhani kuwa ufunuo wa Mwenyezi Mungu umekwisha zamani na hautakuja[17]. Wala msiseme kwamba roho takatifu (Jibril) hatateremka tena bali aliteremka zamani tu. Kweli kweli nawaambieni; milango yote inafungwa, lakini mlango wa kuteremkia roho takatifu haufungwi kabisa. Fungueni milango ya roho zenu ili aingie roho takatifu. Hakika ninyi mnajitupa mbali na jua mnapofunga dirisha la kuingilia nuru yake. Ewe mwenye akili ndogo! Simama, ufungue dirisha ili jua liingie ndani yako. Ikiwa kama Mungu Hakuwafungieni njia za baraka za dunia siku hizi, bali Amewazidishieni, jee, mnadhani kuwa Amewafungieni njia za baraka za mbinguni ambazo siku hizi mnazo haja nazo sana? Hasha! Bali umefunguliwa mlango ule wazi kabisa. Sasa kama Mungu Amewafungulieni mlango wa neema na baraka zote za kwanza kwa kufuatisha mafundisho yake Aliyofundisha katika sura ya Alhamdu, kwa nini mnakataa kuzipokea neema na baraka hizi? Kuweni wenye kiu

---

17 Sharia imekwisha timizwa katika Quran lakini ufunuo (Wahyi) haujaisha sababu ufunuo ni roho ya dini ya kweli. Dini isiyo na ufunuo wa Mungu ndani yake basi ndio dini iliyokufa na Mungu si pamoja nayo.

kwa sababu ya chemchem hii na maji yatakuja yenyewe kwenu. Lilieni maziwa, kama mtoto anavyolilia maziwa ya mama yake, na maziwa yatachuruzika yenyewe. Wezeni kurehemu, ili mrehemiwe. Onyesheni mahangaiko, ili mpate utulivu.

Lilieni mara kwa mara ili mshikwe na mkono mmoja. Ni njia yenye taabu namna gani, iliyo njia ya Mungu! Lakini njia hii hufanywa nyepesi kwa wale wanaojitupa katika shimo la taabu kwa nia ya kufa. Hao wanaohukumu katika mioyo yao kuwa 'tunakubali moto na tutaungua kwa ajili ya Mpenzi wetu Mwenyezi Mungu', kisha wao hujitumbukiza katika moto kumbe moto ule ni pepo. Na hivi ndivyo Alivyosema Mungu katika Quran Tukufu; *'Wain minkum illa waariduha kana 'alaa Rabbika hatman maqadhiyya'*[18] - Enyi watu wabaya na wazuri, hapana yeyote kwenu asiyepita kwenye moto wa jahannam, lakini hao wanaounguzwa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu wataokolewa katika moto. Lakini yule mwenye kuunguzwa kwa ajili ya nafsi yake yenye kumwamrisha kutenda mabaya, basi moto utamwunguza.

Amebarikiwa yule mwenye kupigana na nafsi yake kwa ajili ya Mungu. Na bahati mbaya kwa yule anayepigana na Mungu kwa ajili ya nafsi yake, wala asipatane Naye. Mwenye kuvunja amri ya Mungu kwa ajili ya nafsi yake haingii katika ufalme wa mbinguni kabisa. Kwa hiyo jitahidini ninyi msishuhudiwe hata na herufi au nukta moja ya Quran khilafu zenu (dhidi yenu) ili msikamatwe kwa sababu yake. Maana, hata shari kidogo inaleta adhabu. Wakati ni mdogo na mwendo ni mrefu, nyanyueni upesi upesi nyayo zenu, maana usiku umekaribia. Na kile mnachotaka kumpelekea, kitazameni mara kwa mara ili kisipunguke kitu cho chote na kupunguka huku kusije kuwa sababu ya hasara yenu; au visije kuwa vitu vyote vibaya au

18 Sura 19 aya 72

vibovu ambavyo havifai kupelekwa zawadi katika baraza la Mfalme wa Wafalme.

Nimesikia ya kuwa wako baadhi yenu hawasadiki *Hadithi* za Mtume Mtukufu kabisa. Ikiwa ni hivi basi hao wanakosa sana. Nami sijawafundisheni mafundisho haya kabisa, wala sijawaambieni ya kuwa msishike *Hadithi.* Bali madhehebu yangu ni kuwa Mwenyezi Mungu amewapeni vitu vitatu kuwaongozeni. Kitu cha kwanza katika vitu hivi vitatu ni Quran Tukufu[19], ambayo ndani yake umebainishwa Umoja wa Mungu, na utukufu Wake na heshima Yake. Na ndani yake zimehukumiwa hitilafu zilizokuwa baina ya Wakristo na Wayahudi. Kama hitilafu na kosa la kwamba Isa bin Mariamu ameuawa juu ya msalaba na amelaaniwa wala hakurufaishwa kama Manabii wengine. Vile vile imekatazwa katika Quran kukiabudu kitu kingine isipokuwa Mungu. Wala msimwabudu mwanadamu wala mnyama, wala msiabudu jua wala mwezi wala nyota nyingine; wala vitu vingine, wala nafsi zenu.

Basi jihadharini wala msiende hata hatua moja kinyume na mafundisho ya Mungu na mwongozo wa Quran Tukufu. Nakuambieni kweli kweli kuwa, mwenye kuvunja hata amri moja ndogo katika amri mia saba za Quran Tukufu, basi yeye, kwa mikono yake, anafunga mlango wake wa wokofu. Hakika Quran ndiyo iliyofungua njia za wokofu wa kweli, uliokamilika; na baki yote ni kama vivuli vyake. Kwa hiyo, someni Quran

19 Kitu cha pili cha kuongoza ni Sunna, yaani desturi njema na mfano mzuri wa Mtume, Amani ya Mungu juu yake, alioonyesha kwa vitendo vyake. Mathalani, alisali sala na alituonyesha kwa mfano wake kuwa tusali hivi, na akatuongoza tufunge saumu hivi. Basi hii ndiyo Sunna – yaani mwendo wa Mtume au desturi yake kwa kufuata kauli ya Mungu ambayo alionyesha kwa vitendo vyake. Na kitu cha tatu cha kuongoza ni Hadithi. Hadithi ni maneno ya Mtume yaliyokusanywa baada ya kufariki kwake na daraja ya Hadithi ni chini ya Quran na Sunna. Sababu Hadithi nyingi ni za kudhania tu. Na Hadithi inafikia daraja ya yakini inapowafikiana na Sunna. (Maelezo zaidimtasoma katika sura ya 6).

kwa kufikiri na ipendeni sana, kupenda ambako hamjakipenda chochote. Sababu ni kama alivyoniambia Mwenyezi Mungu; "*Alkhairu kulluhu fil Qur'an*" – Heri zote zimo katika Quran tu. Na haya ndiyo kweli. Ole kwa wale watu wanaotanguliza juu yake vitu vingine! Hakika Quran Tukufu ni chemchem ya kufaulu kwenu na wokofu wenu wote. Hapana haja yoyote katika haja za dini yenu ila mtaipata katika Quran Tukufu. Quran Tukufu ndiyo itakayosadikisha au kukadhibisha Imani yenu siku ya Kiyama. Minghairi ya Quran hapana kitabu kingine chini ya mbingu kinachoweza kuwaongozeni bila ya njia ya Quran Tukufu. Mwenyezi Mungu Amewafanyieni hisani kubwa kuwapeni kitabu kama Quran.

Nawaambieni kweli kweli ya kuwa kitabu mnachosomewa lau kama wangalisomewa Wakristo wasingaliangamia, na neema hii na mwongozo huu mliopewa lau kama wangalipewa Mayahudi badala ya Torati, baadhi ya mataifa yao wasingaliikataa siku ya Kiyama. Basi heshimuni neema hii mliyopewa. Hii ni neema ipendwayo sana na ni hazina kubwa! Lau kama isingekuja Quran, dunia yote ingalikuwa sawa na kipande kichafu cha nyama. Quran Tukufu ni kitabu cha mwongozo ambacho mbele yake mwongozo mwingine si kitu.

# SURA YA TATU

## Malinganisho kati ya Quran Tukufu na Injili.

Mletaji wa Injili alikuwa Roho Mtakatifu aliyedhihirika kwa sura ya njiwa ambaye ni ndege mnyonge na dhaifu, hata paka anaweza kumkamata. Kwa hiyo Wakristo wakaendelea, siku baada ya siku, kuanguka katika shimo la upotevu. Wala hawakubakiwa na wema wa rohoni. Maana, msingi wa Imani yao ulikuwa juu ya njiwa. Lakini Roho Mtakatifu wa Quran amedhihirika katika sura yenye cheo kikubwa kilichojaza mbingu na ardhi kwa nuru yake. Basi yule njiwa anawezaje kufanana na maonyesho makubwa haya (ya Roho Mtakatifu wa Quran), ambayo yametajwa katika Quran pia? Quran inaweza kumtakasa mwanadamu katika juma moja tu, kama ifuatwe sawasawa kwa dhahiri na kwa siri. Na inaweza kuwafanyeni kama manabii kama hamwikimbii.

Kitabu kipi isipokuwa Quran, kilichowafundisha wasomaji wake katika mwanzo wake dua hii, na kimewatumainisha kuwa; *'Ihdinas Siratal mustaqiyma siratal ladhiyna an-'amta 'alaihim'* – Tuongoze katika njia za neema zile zilizoonyeshwa kwa watu wa kwanza, waliokuwa manabii na mitume na masiddik na mashahidi na masalih. Basi jiimarisheni maazimio yenu wala msikatae mwito wa Quran, kwani Quran inataka kuwapeni neema zile zilizopewa watu wema wa zamani. Je, Mwenyezi Mungu Hakuwapeni nchi ya wana wa Israeli na Baitul Mukaddas, nyumba Tukufu ya Waisraeli, ambayo mpaka sasa imo mikononi mwenu? Enyi wenye Imani kidogo na wenye nia dhaifu! Je, mnadhani kuwa Mungu Amewarithisheni mamlaka yao (Waisraeli) ya kidunia lakini hakuweza kuwapeni mamlaka yao ya kiroho! Hasha, bali Mwenyezi Mungu Ana

nia ya Kuwafikishieni neema zilizo bora kuliko walizozipata Waisraeli. Mwenyezi Mungu Amewarithisheni mamlaka yao ya kiroho na kidunia, lakini hawatakuwako warithi wenu wengine wowote mpaka ifike siku ya Kiyama. Mwenyezi Mungu Hatawanyimeni katika neema ya Wahyi na ufunuo au kusemezana naye. Atatimiza kwenu neema zote zilizopewa watu waliotangulia.

Lakini mwenye kuzua kwa Mungu uwongo kwa ushupavu na kuwaambia watu ya kuwa umefunuliwa wahyi wa Mungu kwangu na hali hakufunuliwa; au kama atasema ya kuwa; Mungu Amenitukuza kwa maneno yake na usemi wake na hali yeye hakutukuzwa wala hakupata chochote katika neema ya namna hii, nasema kwa shahada ya Mwenyezi Mungu na Malaika wake, ya kwamba mtu huyo atahilikishwa. Sababu amezua uwongo juu ya Mwumba wake na kudanganya na kudhihirisha ushupavu na uasi. Basi jihadharini na mambo haya. Ni laana ya Mungu juu ya wale wajioteshao ndoto na kujidai kwamba wanapata katika hali yao ufunuo wa Mungu na usemi wake. Inajulikana kuwa wanadhani rohoni mwao Mungu hayupo; lakini watakamatwa na adhabu ya Mungu iliyo kali; wala haiwezi kuondoka kwao siku yao mbaya. Basi ninyi zidini katika ukweli na utawa na katika haki na kumpenda Mungu, na fahamuni hiyo ndiyo kazi yenu siku zote mpaka mwisho wa uzima wenu. Kisha Mwenyezi Mungu Atamtukuza Amtakaye katika ninyi kwa kusema naye na Kuzungumza naye vile vile. Lakini jihadharini hata kutamani hivi ili usianze ufunuo wa shetani, kwa sababu ni kutamani kwa nafsi, kunakowaangamiza watu wengi. Kwa hiyo, endeleeni kutumika na kumwabudu, toeni jitihada yenu yote kwa haya ili muwe wenye kutii sana amri za Mungu. Na endeleeni kuzidi katika yakini kwa kuokoka si kwa sababu ya kupata ufunuo.

Mmeandikiwa katika Quran Tukufu hukumu nzuri sana. Na katika hukumu zile iko mojawapo ya kwamba jiepusheni kabisa kumshirikisha Mungu. Sababu mushiriki amenyimwa chemchem ya wokofu. Wala msiseme uwongo, sababu uwongo pia ni sehemu moja ya ushirikina.

Quran Tukufu haisemi kama Injili kuwa; Msitazame wanawake wasio jamaa zenu kwa mtazamo mbaya na kuwatamani. Bali Quran inasema; Msitazame wanawake wasio jamaa zenu kwa mtazamo mbaya au mzuri, maana haya yote ni pahali pa kuteleza na hatari. Bali inafaa kuinamisha macho yako unapokutana na wanawake wasio jamaa zenu wala usiwe na habari ya sura zao isipokuwa anavyoona mtu katika hali ya kusinzia.

Wala Quran haiwaambieni kama Injili kuwa msinywe pombe kiasi cha kuwalevyesheni. Bali inasema kuwa msinywe pombe kabisa na ukinywa pombe huwezi kupata njia ya Mwenyezi Mungu wala Mwenyezi Mungu Hatasema nawe wala Hatakutakasa katika uchafu. Nayo inasema kuwa pombe ni uvumbuzi wa shetani, jiepusheni nayo.

Quran haiwaambieni kama Injili kuwa; usimkasirikie ndugu yako bila sababu; bali inasema, zuieni ghadhabu zenu, hata mshike aya hii ya Mungu; "*Tawaaswau bil marhama*"[20] – Usieni watu kurehemu; na kuwausia watu wafanye hivi pia, wala usirehemu wewe tu, bali wahimize nduguzo wote warehemu.

Wala Quran haiwafundisheni kama Injili kuwa subirini, stahamilini juu ya kila uchafu wa wake zenu, isipokuwa wafanyapo zinaa; wala msiwape talaka. Bali Quran inasema; "*Attwayyibaatu littwayyibiina*[21]" – wanawake wazuri kwa

20 Sura 90 aya 18
21 Sura 24 aya 27

wanaume wazuri. Quran inataka kuwa mtu mwovu asikae na mzuri. Basi kama mke wako hazini, lakini anawatazama wanaume wengine kwa tamanio baya na kukumbatiana nao na kudhihirisha mambo yanayofanana na zinaa, ingawa bado hajazini, na kuonyesha uchi wake kwa mwingine na kuwa mshiriki na mfisadi na kuwa mbali na yule Mungu Mtukufu ambaye unamwamini, na kama hakuacha mambo haya basi ni jaizi kwako kumpa talaka. Sababu kwa vitendo vyake ameachana nawe, na sasa si kiungo cha mwili wako, na sasa si jaizi kwako kukaa naye, kwani si mnofu wa mwili wako, bali amekuwa kama kiungo kichafu chenye kuchukiza kifaacho kukatwa, isije kikaharibu viungo vingine nawe ukafa.

Wala Quran haisemi kama Injili kuwa; Usiape kabisa, bali inawakatazeni kuapa ovyo. Kwani nyakati zingine kiapo kinakuwa sababu ya kukatia hukumu. Na Mwenyezi Mungu Hataki kuvunja sababu katika sababu za kukata hukumu, kwani kwa kukataza inabatilika hekima yake. Jambo hili ni wazi kuwa ikiwa mmojawapo ana ugomvi wala hana shahidi anayeshuhudia basi katika hukumu unahitajiwa ushahidi wa Mwenyezi Mungu.

Wala Quran haiwaambieni kama Injili kuwa: Msishindane na mtu mdhalimu popote. Bali inasema: "*Jazaau sayyiatin sayyiatun mithluhaa faman 'afaa wa aslaha fa ajiruhu 'ala llahi*[22]" – Malipo ya uovu ni uovu sawasawa na ule aliofanyiwa, lakini anayesamehe, na kama kwa msamaha mtu mdhalimu anaweza kupata faida ya kujisahihisha na kutotokea uharibifu, basi Mwenyezi Mungu Yu radhi katika msamaha wa namna hii na Atampa ujira wake. Basi kwa maneno ya Quran, si vizuri kujilipiza kila mara, wala haipendezi kutoa msamaha kila wakati, bali inafaa kutazama hali ya kila mara na inafaa kushindana na kusameheana kwa

22 Sura 42 aya 41

kufuatisha faida ya kusahihisha. Haya ni makusudi ya Quran Tukufu.

Wala Quran haisemi kama Injili kuwa; wapendeni maadui zenu, bali inasema kuwa usifanye uadui na yeyote kwa sababu ya nafsi yako; na huruma yako iwe kwa viumbe vyote. Lakini aliye adui wa Mola wako, adui wa Mtume wako na adui wa kitabu cha Mungu, basi huyu awe adui yako. Hata hao usiwanyime kuwabashiria na kuwaambia. Na inafaa uwe adui wa vitendo vyao wala si wa nafsi zao, na wafanyizie jitihada mpaka wawe marafiki. Na Mwenyezi Mungu anasema juu ya jambo hili; '*Innallaha ya'muru bil'adli wal ihsani waiytaai dhil qurbaa*[23]' – Unajua Mwenyezi Mungu analotaka kwako? Basi hayo tu ya kwamba muwatendee watu kwa uadilifu, na zaidi ya haya mfanye ihisani kwa wale wasiokufanyieni ihisani, na zaidi ya haya yote fanyeni huruma kwa viumbe vya Mungu kama kwamba wao ni jamaa zenu hasa au kama mama anavyowafanyia huruma watoto wake. Kwani katika hisani kimo chembe kilichofichwa cha kujipendeza na baadhi ya nyakati mwenye hisani anadhihirisha hisani yake kwa kujipendeza na kujifakharisha. Lakini mwenye kufanya hisani na huruma kama mama, kwa mapenzi ya moyo, yeye hawezi kujifakharisha au kujisifu. Basi daraja ya mwisho ya wema ni ile inayotendwa kwa shauku na mapenzi ya rohoni.

Tena aya hii haihusu viumbe tu bali na Mwenyezi Mungu pia. Ama *'adli* kwa Mungu ni kukumbuka mema Yake na kumtii; na *ihsani* kwa Mungu ni kumwamini kana kwamba unamwona. Ama *kufanya huruma kama* mtu *anavyofanya kwa jamaa zake,* kwa Mwenyezi Mungu ni kumwabudu kwa ajili ya kumpenda si kwa sababu ya kutamani pepo au kuogopa moto. Hata kama ukifahamu kwamba hapana pepo wala jahannamu usipunguze kumpenda Mwenyezi Mungu wala usiache kumtii.

---

23 Sura ya 16 aya 91

Na yameandikwa katika Injili kuwa waombeeni baraka wale wanaokulaanini. Lakini Quran inasema msifanye cho chote kwa nafsi zenu, bali ulizeni mioyo yenu, ambayo ni nyumba ya maonyesho ya Mwenyezi Mungu, mtu wa namna hii afanyweje? Basi kama Mungu Akiwafunulieni kuwa mwenye kulaani huyu inafaa kurehemiwa na hakulaaniwa mbinguni, basi msimlaani, ili msiwe wahalifu wa Mwenyezi Mungu. Lakini kama mioyo yenu haimfahamu kuwa ana udhuru na kuingizwa katika mioyo yenu ya kwamba mtu huyu amelaaniwa mbinguni pia, basi msimwombee baraka, kama vile Mitume, hata mmoja wao hakumwombea shetani baraka wala hawakumwachilia katika laana. Lakini msifanye haraka kumlaani mtu, sababu kudhani kwingi kumekuwa uwongo na kulaani kunamrudia mwenye kulaani. Nendeni kwa fikra sana na juu yenu kuugua sana kabla hamjaanza kitendo na ombeni msaada kwa Mwenyezi Mungu sababu ninyi ni vipofu. Msije kumfahamu mwenye uadilifu kuwa ni mdhalimu na kumdhani mkweli kuwa ni mwongo, na kumghadhibisha Mungu wenu kwa njia hii na kupoteza wema wenu wote.

Vile vile ilisemwa katika Injili, "Msifanye vitendo vyenu vyema mbele ya watu ili mpate kuvionyesha". Lakini Quran inasema, msifiche vitendo vyenu vyema vyote kwa watu, bali fanyeni baadhi ya vitendo vyenu vyema kwa siri mnapofahamu kuwa katika kuficha ni faida kwa nafsi zenu; na dhihirisheni baadhi ya vitendo vyenu vizuri mnapofahamu kuwa kudhihirisha vitendo hivi kuna faida kwa watu, ili mpate thawabu mara mbili na ili watu wadhaifu wasioweza kufanya wema nao vile vile kwa kuwafuateni wafanye wema. Na Aliyosema Mungu katika kitabu Chake ni: '*Sirran, wa'alaaniyatan*[24]' - toeni sadaka kwa siri na kwa dhahiri. Na hekima ya hukumu hizi Amebainisha Mwenyewe ya kwamba wafahamishe watu kwa maneno na

24 Sura 2 aya 275

vitendo, kwani maneno tu hayawi na faida kila mahali, mara nyingi mifano mizuri inakuwa na faida sana.

Tena imo katika Injili ya kwamba: Unapoomba nenda chumbani kwako! Lakini Quran inafundisha kuwa usifiche dua zako kila wakati. Omba mbele ya watu na pamoja na jamaa zako, ili ikikubaliwa dua inakuwa sababu ya kuzidisha imani kwa jamaa na ili watu wengine wapende kushughulika katika dua vile vile.

Vile vile imeandikwa katika Injili: Ombeni hivi: "Baba yetu uliye mbinguni, jina lako litukuzwe, ufalme wako uje. Uyatakayo yatimizwe chini yanavyotimizwa mbinguni! Tupe chakula chetu cha kila siku. Utusamehe deni zetu kama sisi tunavyowasamehe wadeni wetu. Usituingize majaribuni, bali utuokoe na yule mwovu, kwani wako ni ufalme na nguvu na utukufu hata milele.[25]"

Lakini Quran inasema kuwa: Si hivi kuwa ardhi haina utukufu, bali katika ardhi utukufu wa Mungu unasimama pia kama unavyosimama mbinguni. Mwenyezi Mungu Anasema: '*Wain min shai·in illa yusabbihu bihamdihi*' – yaani, kila kitu kilichopatikana katika ardhi au mbinguni kinamtukuza Mungu na kinamhimidia[26]. '*Yusabbihu lillahi ma fis samaawati wa ma fil ardhi*' – Na kila kitu katika ardhi au mbinguni kinashughulika katika kumkumbuka[27]'. Na mito inashughulika katika kumkumbuka. Na miti pia inashughulika katika kumkumbuka. Na wengi wanaosadiki, wenye roho safi, wanashughulika katika kumkumbuka. Na yule asiyeshughulika katika kumkumbuka Mungu, moyoni mwake na ulimini mwake, wala haonyeshi unyenyekevu mbele ya Mungu, yeye pia anaonyesha

25 Matayo, 6: 9 - 14
26 Sura 17 aya 45
27 Sura 62 aya 2

unyenyekevu kwa sababu adhabu na taabu zilizomfikia kwa kadri na hukumu ya Mwenyezi Mungu zinamtiisha.

Na yaliyoandikwa katika kitabu cha Mungu (Quran) juu ya Malaika kuwa, wao wanamtii Mwenyezi Mungu sana, hivi hivi imeandikwa katika Quran Tukufu kuwa kila jani katika ardhi na kila chembe, hata kila kitu kinashughulika katika kumtii Mwenyezi Mungu. Hata jani moja bila amri yake haliwezi kuanguka wala dawa haiwezi kuponyesha bila hukumu yake. Wala chakula hakifai ila kwa amri yake. Kila kitu kinaporomoka kumsujudia kwa unyenyekevu na kinashughulika katika kumtii. Changarawe za milima na chembe za ardhini na matone ya baharini na mito, na majani ya miti yoyote, na kila sehemu zake na kila kiungo cha mtu na mnyama kinamjua Mwenyezi Mungu na kinamtii na kinashughulika katika kumhimidia na kumtukuza Mwenyezi Mungu. Kwa hivi Mwenyezi Mungu amesema; '*Yusabbihu lillahi ma fis samaawaati wa ma fil ardhi*' – yaani kama vile kila kitu kilichomo mbinguni kinamsabihi na kumtukuza Mwenyezi Mungu hivi ndivyo kila kitu kilichomo ardhini kinamtukuza na kumsabihi Yeye[28].

Basi jee! Mmeona kwamba Mwenyezi Mungu hakutukuzwa katika ardhi? Hasha! Haiwezekani kutoka neno la namna hii katika kinywa cha mtu mtukufu. Bali baadhi ya vitu vya duniani vinatii hukumu za sharia na baadhi yake vinanyenyekea amri za kadri ya Mungu na vingine vinashughulika katika hukumu zote mbili za sharia na hukumu za kadri ya Mungu. Na kila kitu ikiwa mawingu au hewa au moto au ardhi, vyote vinashughulika kumtii Mwenyezi Mungu. Ikiwa mmoja wapo katika watu anaasi hukumu za sharia ya Mungu, yeye anafuata hukumu za kadri ya Mungu. Hapana kitu kisichokuwamo katika falme zake hizi mbili, kila mtu anafuata ufalme mmojawapo katika

28 Sura 62 aya 2

falme hizi mbili za mbinguni.

Naam kwa kiasi cha kuongoka mioyo na kupotoka, baadhi ya nyakati ufisadi na uvivu vinashinda katika ardhi, na nyakati zingine ukumbusho wa Mwenyezi Mungu unashinda duniani. Lakini kupungua na kujaa huko hakuwi kwenyewe bali kunakuwa kwa hekima za Mungu. Mwenyezi Mungu Amependa kwamba iwe hivi duniani na ikawa hivi. Basi zamu ya mwongozo na upotevu inazunguka kama mzunguko wa usiku na mchana na kwa amri ya Mungu na idhini Yake si yenyewe. Pamoja na haya kila kitu kinasikia sauti Yake na kinakumbuka utukufu Wake. Lakini Injili inasema kuwa ardhi ni tupu haina utukufu wa Mungu! Na imebainishwa sababu yake katika neno hili la dua ya Injili; "*Ufalme wako uje duniani*"; yaani mpaka sasa ufalme wa Mungu haujaja duniani. Kwa ukosefu wa ufalme wa Mungu duniani, si kwa sababu nyingine, hayawezi kuendelea mapenzi ya Mwenyezi Mungu duniani kama yanavyoendelea mbinguni. Lakini mafundisho ya Quran Tukufu ni kinyume cha mafundisho ya Injili.

Quran inasema kwa maneno wazi wazi kuwa, hapana mwizi aibaye, au mwuaji auaye, au mfidhuli aziniye, au kafiri akufuruye au fasiki akataaye, au mshupavu, hapana mmoja wapo katika hawa awezaye kufanya kitendo kibaya mpaka apewe hiyari kutoka mbinguni. Basi inamkinikaje kusema kwamba ufalme wa Mungu haumo duniani? Je! Yupo mwingine badala ya Mungu akatazaye kuendelea hukumu za Mungu duniani? Hasha! Haya hayawezekani kabisa.

Bali Mwenyezi Mungu Ametengeneza mwenyewe kanuni zingine kwa Malaika wa mbinguni na kanuni zingine kwa watu wa duniani. Wala Mwenyezi Mungu Hakuwapa Malaika hiyari katika ufalme wa mbinguni. Bali aliweka katika tabia zao

kutii tu, hawawezi kuasi wala hawawezi kusahau. Lakini roho ya mwanadamu imepewa hiyari ya kukubali au kukataa. Na kwa sababu ya kuhiarishwa hivi, hatuwezi kusema kwa ajili ya kuwapo mtu mbaya ya kwamba ufalme wa Mungu umeondoka duniani. Hasha! Bali ufalme wa Mungu kwa hali yoyote umo duniani.

Naam zipo kanuni mbili; Ya kwanza ni kanuni ya hukumu na kadri ya Mungu kwa ajili ya Malaika wa mbinguni na kwa hiyo hawawezi kuasi kabisa. Na kanuni ya pili ni hukumu na kadri ya Mungu inayohusiana na wanadamu duniani ambayo wamepewa hiyari kufanya maovu. Lakini wanapoomba msaada na uwezo kwa Mungu na kutubia kwake sana, udhaifu wao unaweza kuondoka kwa msaada wa roho takatifu na wakiweza kujiepusha na kufanya madhambi kama wanavyojiepusha manabii wa Mungu na mitume Wake. Ama watu hawa waliokuwa wenye dhambi, basi kuomba kwao msamaha kutawafaidisha kwa kulindwa katika adhabu iliyo ni matokeo ya dhambi. Kwani kwa kufika nuru giza haliwezi kubakia. Lakini hao wakosefu wasioomba msamaha kwa dhambi zao, yaani hawataki uwezo kwa Mungu ili waepushwe na makosa yao, wao kila mara wanapata adhabu ya dhambi zao. Tazameni! Ugonjwa wa Tauni ulioteremka siku hizi duniani vile vile ni adhabu itokayo kwa Mungu. Na hao waasi wa Mwenyezi Mungu wanaangamizwa kwa Tauni. Basi inawezekanaje kusema kwamba ufalme wa Mungu haumo duniani?

Mkidhania, kama ufalme wa Mungu umo duniani basi mbona tena watu wanatenda dhambi? Naam, kwani dhambi pia ni chini ya kadri ya Mwenyezi Mungu. Hao wakosefu wanatoka katika kanuni ya sheria, lakini hawawezi kutoka katika kanuni ya kadri ya Mungu. Basi inasemwaje kwamba wakosefu hawana kamba ya ufalme wa Mungu shingoni mwao? Tazameni katika

nchi hii ambayo iko chini ya himaya ya dola ya Kiingereza, wapo wezi waibao, tena watu wauaji wanaua, na wazinifu na mahaini, na wanaokula rushwa na wakosefu wengineo pia hupatikana. Lakini haiwezekani kusemwa kuwa katika nchi hii hakuna ufalme wa Kiingereza. Kwani ufalme upo, lakini kwa makusudi serikali haikutoa sharia ya nguvu ili maisha yao yasiwe na dhiki kwa shindo lake.

Na lau kama ufalme ungalitaka kuwazuia wakosefu katika makosa yao kwa kuwafunga kwa dhiki na taabu, wangeweza kuacha makosa yao mara moja. Au kama ingewekwa katika kanuni ya serikali adhabu kubwa juu ya makosa fulani ingewezekana kuyakomesha makosa. Basi ninyi mnaweza kufahamu kuwa katika nchi hii pombe inanywewa sana, na wanawake wazinifu na wamalaya, wizi na matokeo ya uuaji vinazidi. Na hayo yote yanayotokea si kwa sababu ya kuwa hakuna ufalme wa Kiingereza katika nchi hii. Bali kwa ajili ya urahisi wa kanuni iliyowekwa, na kwa hivyo makosa yanazidi; si kwa kuwa ufalme wa Kiingereza umeondoka. Pamoja na haya ufalme una hiyari ya kutengeneza sharia kali na kuweka adhabu kubwa na kuzuia makosa.

Ikiwa hii ndio hali ya ufalme wa kibinadamu, ambayo si kitu mbele ya ufalme wa Mungu, basi itakuwaje hali ya hiyari na uwezo wa ufalme wa Mungu! Lau kama kanuni ya Mwenyezi Mungu ingefanywa kuwa ngumu sasa hivi na radi kumwangukia kila mzinifu, na mwizi apate ugonjwa wa ukoma, na baada ya kuvunda mikono na miguu vianguke. Na kila fasiki akataaye dini ya Mungu afe kwa ugonjwa wa Tauni, Basi kabla ya kwisha juma moja watu wa dunia nzima wangeweza kuvaa shuka ya ukweli na uongofu. Yaani watakuwa watenda mema na wataongoka.

Kweli ufalme wa Mungu umo duniani; lakini kwa sababu ya urahisi wa kanuni ya mbinguni, wakosefu hawakamatwi upesi. Naam, wanaadhibiwa mara kwa mara. Tetemeko la nchi hutokea, radi huanguka, milima ya volkano huangamiza maelfu na maelfu ya wazima, na meli zinazama, na pengine kwa sababu ya magari ya moshi mamia ya watu huangamizwa. Tufani huja na nyumba zinaanguka, na nyoka huuma, na wanyama wakali hurarua, na magonjwa hutokea mara kwa mara; tena si mlango mmoja, bali milango maelfu na maelfu iko wazi ya kuangamizia, ambayo imewekwa kwa ajili ya wakosefu kwa hukumu ya Mwenyezi Mungu.

Basi kwa nini inasemwa kuwa hakuna ufalme wa Mungu duniani? Lakini kwa kweli ufalme upo duniani, kila mwenye makosa anazo pingu zilizofungwa mikononi mwake na minyororo katika miguu yake, lakini hekima ya Mwenyezi Mungu imelainisha sheria ya adhabu yake, kwa hiyo minyororo na pingu havionyeshi alama zao upesi. Na mwisho, kama mtu hakuacha makosa yake basi pingu na minyororo vitamfikisha mpaka katika moto wa mileIe, na vitamtupa katika adhabu ambayo ndani yake mwenye dhambi hafi wala haishi.

Kwa neno zima, zipo kanuni mbili, ya kwanza ni kwa Malaika. Yaani, wao wameumbwa kwa kutii tu, na kutii kwao ni tabia ya roho zao zenye utukufu, hawawezi kuasi wala hawawezi kuzidi katika wema.

Na kanuni ya pili ni ile inayohusu wanadamu. Yaani, imewekwa katika roho za watu hiyari na uwezo wa kuasi, lakini wao wanaweza kuzidi katika wema pia. Na hizi kanuni mbili hazibadiliki. Na kama Malaika hawezi kubadilika kuwa binadamu, vilevile binadamu hawezi kugeuka kuwa Malaika. Hizi kanuni mbili hazibadiliki kabisa, ni za siku zote, tena ni za milele.

Kwa hiyo kanuni ya mbinguni haiwezekani kuhukumu duniani wala haiwezekani kanuni ya duniani kuwahukumu Malaika wa mbinguni. Kama yakiisha makosa ya mwanadamu kwa kutubu, yawezekana kumfanya mwanadamu awe bora kuliko Malaika. Kwani haupatikani katika Malaika uwezo wa kuzidi katika wema. Na dhambi za mtu zinasamehewa kwa kutubia. Na hekima ya Mwenyezi Mungu imebakiza katika baadhi ya watu mwendeleo wa dhambi, ili watambue udhaifu wao baada ya kukosa, kisha watubu na wasamehewe. Hii ndiyo kanuni iliyowekwa kwa ajili ya watu. Na hiyo ndiyo kanuni inayotakiwa kwa tabia za watu. Maana kusahau hasa ni tabia ya binadamu si tabia ya Malaika, Basi itawezekanaje kutumika kanuni inayohusiana na Malaika kwa wanadamu?

Ni jambo la hatia kusema kuwa Mungu ni Mdhaifu, na kusema kuwa Hana ufalme duniani bali yanayotokea duniani ni matokeo ya sheria ya asili na ya kawaida tu. Hasha! Je, Mwenyezi Mungu ni Mdhaifu, Ambaye hata ufalme Wake na utukufu Wake na uwezo Wake haumo duniani bali uko mbinguni tu? Au duniani kuna mungu mwingine aliye na mamlaka ya duniani, kinyume cha Mwenyezi Mungu? Hasha! Wala si vizuri kwa Wakristo kusema kuwa ufalme wa Mungu uko mbinguni tu na mpaka sasa haujaja duniani. Sababu Wakristo wanaamini kuwa mbingu si kitu. Basi ni dhahiri kama iwapo mbingu si kitu chenye ufalme wa Mungu, na duniani mpaka sasa ufalme wa Mungu haujaja, basi maana yake ni kuwa Mwenyezi Mungu Hana ufalme pahali po pote.

Hali, kinyume cha haya, sisi tunauona ufalme wa Mungu duniani kwa macho yetu wenyewe. Umri wetu unakwisha sawa na kanuni Yake. Na tunabadilika katika hali nyingine na tunaona namna nyingi za raha na za huzuni. Maelfu na maelfu ya dua zinakubaliwa na ishara zinadhihirika. Na inaota katika

ardhi maelfu ya namna za mimea na matunda na maua. Je, hivi vyote hutokea bila ufalme wa Mungu?

Lakini vitu vya mbinguni kama jua, mwezi na nyota vinaendelea mwendeleo mmoja tu. Wala haijulikani ndani yake kubadilika kunakoonyesha kuwa huko kuna mbadilishaji. Lakini katika ardhi kunakuwa kubadilika maelfu na maelfu; kila siku wanafariki maelfu na maelfu ya watu na wengine wanazaliwa. Kwa hivi, kila siku katika kila hali na kila namna, inajulikana ndani yake mwendeleo wa Mwenye uwezo, Mwumbaji. Je! ufalme wa Mwenyezi Mungu mpaka sasa haumo duniani?

Tena lnjili haikuonyesha dalili yoyote ili kuthibitisha kwa nini ufalme wa Mwenyezi Mungu haujaja duniani mpaka sasa. Inaweza kuwa, labda Masihi aliomba dua usiku wote katika bustani ili aokoke na dua yake ilikubaliwa kwa ajili ya unyenyekevu wake kama ilivyoandikwa katika Waebrania aya ya saba mlango wa tano, juu ya hayo Mungu hakuweza kumwokoa. Inawezekana matokeo haya kuwa dalili kwa hamu ya Wakristo, kwamba wakati ule ufalme wa Mungu haukuwa duniani. Lakini sisi tumeona taabu kubwa kuliko hii na tumeokoka. Tunawezaje kukataa ufalme wa Mungu haumo duniani?

Je! Kesi ile aliyonishtaki Padre Martin Clark katika korti ya Captain Douglas ili niuawe, ilikuwa ndogo kuliko kesi ile aliyoshtakiwa Yesu na Mayahudi katika korti ya Pilato? Waliyoshtaki kwa sababu ya hitilafu ya dini tu, si kwa sababu ya masingizio ya kuua mtu. Lakini Mungu ambaye ni Mfalme wa ardhini kama alivyo Yu Mfalme wa mbinguni, Alinipa habari ya kesi hii kabla haijaanza na pia Aliniambia Mwenyezi Mungu Akasema: "*Mimi nitakuachilia katika jambo uliloshtakiwa*". Na watu wengi walipewa habari hii kabla ya kutokea kesi

hii na mwisho nikashinda na kuachiliwa. Basi huu ni ufalme wa Mungu ulionilinda katika kesi hii niliyoshtakiwa baada ya kupatana Waislamu na Mabaniani na Wakristo, wote kwa umoja wao.

Na vile vile nikaona maonyesho ya ufalme wa Mungu duniani,si mara moja bali mara nyingi. Hata sina budi kuamini aya hii: *"Lahuu mulkus samaawaati wal ardhi"* – yaani, Anao ufalme ardhini na mbinguni vile vile[29].Tena aya hii;"*Innamaa amruhu idhaa araada shaian an yaquwla lahuu kun fayakuwn"* – yaani, ardhi na mbingu vyote hushughulika katika kumtii Mungu. Na anapotaka jambo lolote anasema kuwa na linakuwa pale pale[30]". Tena Anasema Mwenyezi Mungu; "*Wallahu ghalibun 'alaa amrihi walaakinna aktharan-nasi laa ya' lamuwna"* – yaani, Mungu Anao uwezo juu ya amri Yake, lakini wanadamu walio wengi hawajui uwezo Wake na nguvu Zake[31].

Basi hii ndiyo dua ya Injili: (ufalme wa Mungu uje duniani) iwafanyayo watu kukata tamaa na rehema za Mungu na inawaghafilisha Wakristo katika kulelewa na Mwenyezi Mungu na huruma Zake na malipo Yake. Wala dua hii haijulishi kuwa Mwenyezi Mungu Anaweza Kusaidia, mpaka ufalme wa Mungu uje duniani.

Lakini dua ile waliyofundishwa Waislamu na Mwenyezi Mungu katika Quran, inaonyesha kuwa Mwenyezi Mungu Hakunyang'anywa ufalme Wake duniani kama watu wanavyonyang'anywa ufalme. Lakini sifa zake katika kulea na kuwarehemu na kuwahurumia watu na ufalme wake vinaendelea duniani. Na Anao uwezo Kuwanusuru watumishi Wake, na kwa uwezo Wake Anaweza Kuwaangamiza

29 Sura 9 aya 116
30 Sura 36 aya 83
31 Sura 12 aya 22

wakosefu kwa ghadhabu Yake. Na dua yenyewe ni hii;

"*Alhamdu lillahi rabbil aalamina. Arrahmaanir rahimi. Maliki yaumiddin. Iyyaaka na'budu wa iyyaaka nasta'iynu. Ihdina-ssiratal mustaqiyma. Sirata lldhiyna an amta alaihim, ghairil maghdhuubi alaihim wala-d-dhaalliyna*" - Mwenyezi Mungu peke yake Ndiye Mwenye haki ya kusifiwa kwa kila sifa njema, yaani hapana aibu katika ufalme Wake wala hapana katika sifa Zake itakayokuja baadaye Asiyokuwa nayo sasa, Wala hapana kitu katika ufalme Wake kilichonyang'anywa. Na Hushughulika katika kulea viumbe vyake, viumbe vya duniani na viumbe vya mbinguni. Na Anawarehemu watu bila vitendo vyao kama Anavyowarehemu kwa sababu ya vitendo vyao vyema. Na Hutoa ujira na adhabu kwa wakati maalum. Sisi tunamwabudu Yeye tu na tunaomba msaada kwake tu. Na tunamwomba Atuonyeshe njia za neema zote na Kututenga mbali na njia za ghadhabu na upotevu.

Hii dua iliyomo katika sura ya ALHAMDU, ni mbali kabisa na dua ya Injili na hazipatani kabisa. Kwani katika dua ya Injili imekataliwa kuwapo ufalme wa Mungu duniani. Inadhihirika katika Injili kuwa kulea kwa Mungu hakutumiki duniani, wala rehema, wala huruma, wala uwezo wa malipo na adhabu; sababu ufalme wa Mungu haumo duniani. Lakini inadhihirika katika sura ya Alhamdu kuwa Ufalme wa Mungu umo duniani.

Kwa hivi kila jambo lenye kuhusu ufalme limebainishwa katika sura ya Alhamdu. Ni dhahiri kuwa mfalme lazima awe na sifa hizi: Sifa ya kwanza lazima awe na uwezo wa kulea watu, na sifa hii imethibitishwa katika sura ya Alhamdu, kwa neno la *Mleaji wa viumbe vyote.* Na sifa ya pili, lazima mfalme atoe kwa rehema zake hasa kwa raia zake vitu vyenye kuhitajiwa kuwahuisha bila vitendo vyao wala kutumika kwao. Na kwa

neno la *Mwenye huruma* imethibitishwa sifa hii ya Mungu. Na sifa ya tatu ya mfalme ni kuwa na rehema, yaani ni juu ya mfalme kuwasaidia raia zake katika mambo yao wasiyoweza kuyakamilisha wenyewe. Imethibitishwa sifa hii katika neno la *Mwenye rehema.* Na sifa ya nne ya mfalme ni lazima awe na uwezo wa kutoa malipo na adhabu. Imebainishwa katika neno la *Mmiliki wa Siku ya Malipo.*

Kwa kifupi sura ya Alhamdu imebainisha mambo ya muhimu yanayohusiana na ufalme. Inathibitika katika mambo haya kuwa Mwenyezi Mungu Ana ufalme ardhini na hukumu Zake zimo duniani. Yaani kulea Kwake vile vile kumo, na rehema Yake vile vile imo, na huruma Zake vile vile zimo,na mwendeleo wa adhabu vile vile umo duniani.Na mwisho wa maneno,sifa zote zinazohusu ufalme, Mwenyezi Mungu anazo katika ardhi. Wala hapana hata chembe isiyokuwamo katika hukumu yake. Kila malipo yamo mikononi Mwake. Kila namna ya rehema imo mikononi Mwake.

Lakini Injili inafundisha dua hii kuwa ufalme wa Mungu bado haujaja kwenu duniani, ombeni siku zote ili uje. Yaani mpaka sasa mungu wao bado hajawa na mamlaka ya ardhi wala hajawa mfalme. Basi ni nini mnachotazamia kupata kwa mungu wa namna hii? Sikilizeni na fahamuni kuwa maarifa makubwa ni haya tu kuwa, chembe chembe za ardhi vile vile zimo katika mamlaka Yake kama chembe za mbinguni zilivyomo katika boma la ufalme Wake. Na kama maonyesho makubwa ya ufalme Wake yalivyo huko mbinguni, pia katika ardhi Anayo maonyesho makubwa ya mamlaka Yake. Lakini maonyesho ya mbinguni ni mambo ya imani tu, maana hajapata kwenda huko mbinguni mtu yeyote na kuuona ufalme Wake, lakini maonyesho ya ufalme wa Mungu yanayoonekana katika ardhi ni ya wazi sana hata kila mtu anaweza kuona kwa macho yake.

Kila mtu, hata akiwa tajiri wa namna gani, anakunywa kikombe cha mauti bila hiyari yake.

Basi tazameni jinsi zinavyodhihirika hukumu za Mfalme wa kweli duniani. Inapokuja hukumu ya mauti hapana yeyote anayeweza kuzuia mauti yake au kuahirisha hata dakika moja. Yanapokuja maradhi mabaya yasiyokuwa na dawa yoyote, hata daktari na wala tabibu yeyote hawezi kuyaondoa. Fahamuni namna gani maonyesho ya Mungu yanayodhihirika duniani hata hukumu zake zisiweze kuondolewa. Basi kwa nini inasemwa kuwa Ufalme wa Mungu haumo duniani, bali utakuja baadae?[32]

Tazameni, siku hizi kwa hukumu ya Mungu, dunia imetetemeka mtetemeko mkubwa kwa sababu ya tauni, ili iwe ishara ya Masihi Wake Aliyeahidiwa. Basi nani awezaye kuondoa tauni bila idhini ya Mwenyezi Mungu? Kisha kwa nini inasemwa kuwa Ufalme wa Mungu mpaka sasa haujaja ardhini? Naam ni mfidhuli anayeishi kama wafungwa wabaya na anataka asife kabisa; lakini ufalme wa Mungu wa kweli utamwangamiza na mwishoni atakamatwa na kitanga cha Malaika wa mauti. Mbona inasemwa tena ya kuwa mpaka sasa ufalme wa Mungu haumo duniani? Tazameni kila siku duniani wanakufa watu maelfu na maelfu katika saa moja tu kwa amri ya Mwenyezi Mungu na maelfu ya maskini wanakuwa matajiri kwa idhini Yake, na maelfu na maelfu ya matajiri wanakuwa maskini kwa amri Yake. Basi inamkinikaje, kusema kuwa mpaka sasa ufalme wa Mungu haumo duniani?

---

32 Pia aya hii; *Fahamalahal insaanu* – akaibeba mtu amana ya mapenzi ya Mungu (a). aya hii inadhihirisha kuwa mwenye kumtii Mungu kabisa ni mtu anayefikisha kutii kwa mapenzi yake hata akawa ashiki kwa Mungu na huthibitisha ufalme wa Mungu katika ardhi kwa kubeba maelfu ya mabalaa kichwani kwake. Je! Inawezekana kwa Malaika wawe wenye kutii kama mwanadamu amtiiye Mungu kwa shauku ya moyo wake wote?

Huko mbinguni wanakaa malaika tu, lakini ardhini wanakaa watu na vile vile malaika, wenye kufanya kazi za Mungu na watumishi wa Ufalme Wake, na wamewekwa duniani ili kuhifadhi vitendo vya watu. Na wanamtii Mungu kila wakati na wanapeleka ripoti zao. Basi inamkinikaje kusema kuwa Ufalme wa Mungu haumo duniani? Ama kwa hakika, Mwenyezi Mungu Amejulikana zaidi kwa Ufalme Wake wa duniani kuliko ufalme Wake wa mbinguni. Kwani kila mtu anadhani kuwa siri za mbinguni zimefichwa hazionekani; hata Wakristo wote wa siku hizi na wenye hekima wao wanakataa ya kwamba hakuna mbingu ambayo imedhaniwa ni pahali pa Ufalme wa Mungu. Ama ardhi, kwa hakika, ni kitu hasa kimoja chini ya miguu yetu; na juu yake kunaonekana maelfu ya matokeo ya kudra za Mwenyezi Mungu.

Na inajulikana wazi wazi kuwa mabadiliko na matokeo na kuumba na kifo kinachotokea vinakuwa ni kwa amri ya Aliye Mfalme hasa. Basi inamkinikaje kusema mpaka sasa Ufalme wa Mungu haumo ardhini? Tena mafundisho ya namna hii hayafai siku hizi. Walipokataa Wakristo na kusema kuwa hakuna mbingu, kwani imekubaliwa katika dua ya Injili kuwa Ufalme wa Mungu haumo duniani. Tena upande mwingine Wakristo wenye elimu wote wamekwisha kubali jambo hili; yaani kwa kuvumbua habari mpya kusema kuwa mbingu si kitu. Mwishoni, kwa maneno ya hao, inajulikana kwamba Mungu Hana ufalme duniani wala mbinguni. Ama mbingu wameikataa Wakristo, na ufalme Wake wa duniani Injili imeukataa na imesema kuwa Mungu Hana ufalme ardhini. Kwa hiyo, kwa kufuata kauli yao Mwenyezi Mungu Amekuwa Hana ufalme ardhini na bila ufalme wa mbinguni.

Lakini Mungu wetu Mtukufu Hakutaja katika sura ya Alhamdu neno la mbingu wala la ardhi. Na kwa kusema

kwamba Yeye ni *Rabbil'aalamina* – Bwana wa viumbe vyote; ametueleza hakika ilivyo hasa. Yaani popote panapopatikana viumbe[33] vya namna yoyote, viwiliwili au roho, Mwumbaji na Mlezi wao ni Mwenyezi Mungu, Anayewalea kila wakati, na Anawatengenezea matengenezo ya kuwafaa hali yao. Na juu ya kila kiumbe, mwendeleo wa ulezi Wake na rehema Zake na huruma Zake na thawabu na adhabu Yake, yote yanaendelea kila wakati. Kumbukeni ya kuwa aya ya*'Maliki yaumiddin* - Mmiliki wa Siku ya Hukumu, iliyomo katika sura yaAlhamdu, si mradi wake kwamba adhabu na thawabu itakuwa siku ya Kiyama tu, la, bali imebainishwa katika Quran mara kwa mara na tena wazi wazi kuwa, Kiyama ni siku ya malipo makubwa; kwa hiyo katika dunia vile vile inaendelea namna ya adhabu na thawabu kama isemwavyo katika aya hii "*In tattaqu-llaha yaj'allakum furqaana*"[34], yaani kama mtamwogopa Mwenyezi Mungu Atawapeni alama ipambanuayo.

Sasa sikilizeni hadithi hii vile vile: Kimeombwa katika dua ya lnjili 'chakula cha leo' kama ilivyosemwa, "Utupe chakula chetu cha leo". Lakini hili ni jambo la ajabu, atawezaje kutoa chakula cha leo yule ambaye ufalme wake bado haujaja duniani? Mpaka sasa mimea na matunda havijaiva kwa amri yake, bali vinaiva vyenyewe, na mvua inanyesha yenyewe! Basi mwenye uwezo wa namna hii anawezaje kutoa chakula? Utakapokuja ufalme wake duniani ndipo anatakiwa kuombwa chakula. Lakini sasa

hana mamlaka juu ya vitu vya duniani, atakapopata mamlaka juu ya vitu hivi ndipo atapata uwezo wa kutoa chakula! Kwa hiyo kumwomba sasa hakuna maana!

33 Tazama namna gani neno la Rabbil'aalamina – Bwana wa viumbe vyote, lilivyo na wasaa na kukusanya kila kitu. Lau kama ithibitishwe kuwa mbinguni kuna kiumbe nacho pia kitakuja chini ya neno hili.

34 Sura ya 8 aya 30

Na baada ya haya: Kauli hii katika lnjili kuwa "utusamehe deni zetu, kama sisi tunavyowasamehe wadeni wetu"[35] pia si kweli; sababu hajapata mpaka sasa ufalme wa duniani na mpaka sasa Wakristo hawajala chakula kilichotoka katika mikono yake. Basi ni deni gani walilo nalo? Hapana haja kuomba msamaha wa deni kwa Mungu mwenye mikono mitupu. Wala hana haja ya kuogopwa, kwani Yeye mpaka sasa hajawa na ufalme ardhini wala mjeledi wa ufalme wake hauogopeshi. Ana uwezo gani kumuadhibu mwenye makosa au kuwaangamiza watu wenye madhambi kwa tauni kama wale walioangamizwa zama za nabii Musa na kuwanyeshelea mvua ya mawe watu wa nabii Lut au kuwafuta kabisa kwa tetemeko au kwa radi au kwa adhabu nyingine? Kwani ufalme wa Mungu mpaka sasa haujaja duniani. Basi mungu wa Wakristo ni dhaifu kama mtoto wake alivyokuwa dhaifu na ni mnyonge kama alivyokuwa mwana wake, kwa hiyo ni bure kumwomba dua kama hii "utusamehe deni zetu", aliwakopesheni lini ili sasa awasameheni? Maana, mpaka sasa ufalme wake haumo duniani! Na kama ufalme wake haujaja ardhini, basi mimea yote iliyomo ardhini na vitu vingine vya ardhi haviwi kwa amri yake, bali vimekuwa vyenyewe: maana hukumu yake haitumiki duniani. Na kama Yeye si hakimu ardhini wala Mfalme wa dunia wala haipatikani neema ya dunia kwa amri ya ufalme wake, basi hana hiyari wala hana haki kumwadhibu ye yote. Ni upumbavu kuamini mungu kama huyu dhaifu na kutumaini kwake, kwani ufalme wake mpaka sasa haumo duniani.

Lakini dua ya sura ya Alhamdu inatufundisha kuwa Mungu Anao ufalme ardhini kila wakati kama Alivyo na ufalme mahali popote. Na sura ya Alhamdu imetaja mwanzo wake kwa wazi wazi sifa njema zenye mamlaka ya Mungu ambazo hapana kitabu cho chote duniani kilichotaja kwa wazi wazi

35 Mathayo 6:12

sifa kama hizi. Kama Alivyosema Mwenyezi Mungu, kuwa Yeye ni Mwenye rehema, na Mwenye huruma, na ni *Mfalme* wa siku ya hukumu. Na baada ya sifa hizi Mwenyezi Mungu Ametufundisha kuomba dua. Na dua aliyotufundisha si kama dua aliyofundisha Yesu Kristo, "Utupe mkate wetu wa kila siku" tu, bali ni dua yenye kukusanya kila kitu kinachomhusu mtu, na dua yenyewe ni hii: *Ihdinasswiratal mustaqiyma. Swirata lladhiyna an-'amta 'alaihim* - yaani, Ewe Mwenye sifa kamili na Ewe Mtoaji Mwenye hisani Ambaye Unalea hata chembe na kikapata manufaa katika rehema Yako na huruma Yako, kila neema uliyowapa watakatifu wa zama, Utupe nasi vile vile; na Tuepushe na kukuasi ili tusiwe katika wale walio kasirikiwa, na Tuepushe tusinyimwe msaada Wako ili tusipotee katika njia iliyonyoka, Amin.

Sasa, kwa upelelezi huu, imekwisha dhihirika tofauti kati ya dua ya Injili na dua ya Quran. Ama Injili inaahidi kuwa ufalme wa Mungu utakuja, lakini Quran inasema kuwa ufalme wa Mungu upo pamoja nanyi kwa kusema tu, bali upo kwa ukweli pamoja nanyi kwa hukumu zake. Basi Quran haiahidi tu kama Injili, bali inadhihirisha ufalme wa Mungu uliomo duniani, na hukumu Zake. Katika haya umedhihirika ubora wa Quran kuliko Injili. Quran inamuonyesha Mungu Yule Ambaye katika uzima huu wa dunia ni Mwokozi wa waongofu na kuwastarehesha katika dunia. Wala hapana nafsi isiyokuwa na baraka Zake. Bali kila nafsi inapata baraka yake kwa kufuatisha kulea Kwake na rehema Zake na huruma Zake. Lakini Injili inaonyesha Mungu yule ambaye ufalme wake mpaka sasa haujaja duniani, bali unaahidiwa tu. Basi, fikirini, ni kitabu gani kifaacho kufuatwa katika vitabu hivi viwili. Mwanachuoni wa zamani *Hafidh Sherazi alisema kweli;* Ee Sheikh! Mimi namfuata bwana wa masheikh, usinikasirikie; kwani wewe unaahidi tu

na Yeye anatekeleza pia.

Tena wamesifiwa katika Injili wapole, wadhaifu na maskini na vile vile wamesifiwa wale wanaoudhiwa wala hawashindani. Lakini Quran haisemi kuwa kuweni maskini siku zote wala msishindane na waovu kabisa. Bali inasema kuwa upole na umaskini na udhaifu na kusamehe na kuacha kushindana, haya yote ni mema, lakini haya yote ni mabaya yanapotumika pasipo pahali pake. Kwa hivi, tendeni kila jema kwa kutazama pahali pake na wakati wake, kwa sababu jema lisilokuwa pahali pake na wakati wake ni baya. Kama mnavyoona mvua ni kitu kizuri na tena kinahitajiwa sana, lakini inapoteremka wakati usio wake inakuwa sababu ya kuharibu mimea. Na ninyi mnaona kuwa uzima wenu hauwezekani kudumu katika hali yake kwa kutumia chakula cha namna moja cha baridi au cha moto siku zote. Lakini uzima unaendelea kwa kubadilisha namna ya vyakula na kunywa na kufuatisha wakati na pahali. Hivi hivi inafaa kwenu kutumia kwa kubadilisha ujeuri na upole, kulipiza kisasi na kusamehe, dua na laana, na tabia zingine kwa kufuatisha wakati na pahali. Kuweni wapole na wenye tabia nzuri, lakini jihadharini kuwa hivyo pasipo wakati wake na pahali pake.

Pamoja na haya, kumbukeni ya kwamba tabia nzuri hasa, ni tabia isiyochanganyika na sumu ya matamanio ya nafsi, bali ni ile iteremkayo kutoka juu kwa mkono wa Jibril. Ninyi hamuwezi kupata tabia nzuri kwa jitihada yenu tu msipopewa tabia hizi nzuri kutoka juu. Na ni mwongo kila anayejidai ya kwamba yeye ni mwenye tabia nzuri ambaye hakupata tabia nzuri kutoka mbinguni kwa mkono wa Jibril. Chini ya maji yake ziko takataka nyingi na uchafu mwingi unaoonekana wakati wa mchafuko wa nafsi. Kwa hiyo, ombeni msaada kwa Mwenyezi Mungu kila wakati ili mwokoke katika takataka zile na uchafu

ule, na iIi Jibril azalishe katika roho zenu tohara ya kweli na utakatifu. Na jueni kuwa tabia nzuri zenye kutakasika ni miujiza ya waongofu, hapana anayeshirikiana nao ila wao peke yao. Sababu wale wasiojitupa kwa Mungu hawapati uwezo utokao juu, kwa hivi haimkiniki kwao kupata tabia nzuri.

Jifungamanisheni pamoja na Mwenyezi Mungu sawasawa. Na acheni maskhara na mzaha, ukorofi na kutukana, tamaa na uwongo, ufasiki na tazamo baya, nia mbaya na kupenda dunia, kiburi na ufahari, kujipendelea na shari, ufisadi na ubishi. Yaacheni haya yote mtapewa tabia nzuri na neema zote kutoka mbinguni. Ninyi ni wadhaifu sana mpaka mtakapopata uwezo utokao juu utakaowainueni na uzima ule unaotolewa na Roho Mtakatifu *(Jibril)* uingizwe mioyoni mwenu, si wadhaifu tu bali ni maiti msio na roho. Na katika hali ya namna hii ninyi hamuwezi kushindana na msiba wowote wala hamuwezi kujiepusha na kiburi na ufahari katika hali ya furaha na utajiri. Na kwa kila upande ninyi mmeshindwa na shetani na nafsi zenu. Wala hakuna dawa yoyote kwa ajili yenu ila ni moja tu, yaani ni uwezo mtakatifu unaoteremka hasa mikononi mwa Mwenyezi Mungu, ugeuzao nyuso zenu kwenye uongofu na wema. Kuweni wana wa mbinguni, msiwe wana wa duniani. Na kuweni warithi wa nuru, msiwe wapenzi wa giza, ili msalimike na mwendeleo wa shetani. Hakika shetani anafungamana na usiku, hana haja ya mchana, sababu yeye ndiye mwizi wa zamani apenyaye penye giza.

# SURA YA NNE

## Bishara kuu Iliyomo katika Sura ya Alhamdu.

Tena sura ya Alhamdu si mafundisho tu, bali ina bishara kuu vile vile. Nayo ni kuwa, Mwenyezi Mungu, baada ya kuzitaja sifa Zake nne za ulezi, na rehema na huruma na ufalme Wake wa siku ya hukumu, na kuonyesha uwezo Wake wa kuadhibu na kufariji, Amefundisha katika aya zifuatazo dua hii: *Ihdina-sswiraatal mustaqiyma. Swiarata lladhiyna an-'amta 'alaihim, ghairil maghdhuwbi 'alaihim wala-d-dhaallyn - Ee* Mola wetu, Mwenyezi Mungu, Utufanye tuwe warithi wa wale watawa Manabii na Mitume waliopita; na Tufungulie njia yao na tupewe neema zao Ulizowapa. Bwana wetu Tulinde tusiwe katika watu Uliowaadhibu duniani; yaani Mayahudi, waliokuwa zama za Nabii Isa na walioangamizwa kwa Tauni. Na tulinde, Bwana wetu, tusiwe katika watu wasioendelea kupata mwongozo wako na wakapotea njia iliyonyoka, yaani Wakristo.

Katika dua hii mna habari za siri za bishara hii; yaani baadhi ya Waislamu watakuwa warithi wa Manabii waliopita kwa sababu ya ukweli wao na utukufu wao na watapata neema za unabii na ujumbe. Na wengine baadhi yao watakuwa wenye sifa za Mayahudi, watakaopata adhabu duniani. Na wengine watakaobaki watavaa mavazi ya Kikristo, yaani watashika mila ya Wakristo.

Maana katika maneno ya Mwenyezi Mungu hiyo ndiyo desturi daima ya kwamba Anapowakataza watu wasitende jambo fulani, basi katika ujuzi Wake yafahamika wazi wazi kwamba baadhi yao watalitenda. Na wengine watapata uongofu na wema. Toka mwanzo wa dunia mpaka mwisho katika kadiri yoyote ya vitabu Alivyovileta, desturi Yake hii ya daima inapatikana ya

kwamba Anapowakataza watu wasifanye kitendo kimojawapo au kuwahimiza kufanya kitendo kimojawapo, katika ujuzi wake yafahamika kwamba baadhi yao watafanya na wengine hawatafanya.

Basi sura hii inatoa bishara ya kuwa, mmojawapo wa umati wa Muhammad, Amani ya Mungu juu yake, atadhihiri kwa ukamilifu wa sifa za Manabii, ili itimizwe kwa wazi wazi bishara iliyomo katika aya hii; *'Ihdina-sswiratal mustaqiym. Swirata lladhina an-'amta 'alaihim'* – Utuongoze katika njia iliyonyooka; njia ya wale Uliowaneemesha. Na kundi moja katika umati wa Muhammad, Amani ya Mungu juu yake, watadhihiri kwa sifa za Mayahudi, ambao aliwalaani Nabii lsa na walikamatwa na adhabu ya Mungu; ili idhihirike iliyotolewa katika kauli hii: *Ghairil maghdhuwbi'alaihim.* Na kundi moja jingine litakuwa kama Wakristo, yaani watakuwa Wakristo ambao kwa sababu ya ulevi wao na uhuru na ufasiki na uovu, wakakosa uongofu wa Mwenyezi Mungu, ili itimizwe iliyoelezwa katika kauli hii: *'Wala-d-dhwaalliyna.*

Na imo katika imani ya Waislam ya kwamba, katika siku za mwisho wa dunia, maelfu kwa maelfu miongoni mwao watakuwa wenye sifa za Mayahudi. Na katika Quran pia aya kadhaa wa kadhaa zimeeleza bishara hii, na mamia ya Waislamu wamekuwa Wakristo, na kuishi kwa wengine wao bila kushika sheria ya Kiislamu kama Wakristo kunadhihirika kwenyewe. Hata ni wengi katika Waislamu wanaopenda desturi na mila za Wakristo. Ingawa wanaitwa Waislam, lakini wanazichukia hukumu za sala na kufunga saumu na hukumu za halali na haramu. Na vikundi hivi viwili, yaani Waislamu wenye sifa za Wakristo na wenye sifa za Mayahudi, wanaonekana kuwa wametawanyika katika nchi hii.

Na mmekwisha kuona kuwa, habari hizi mbili za bishara iliyomo katika Sura ya Alhamdu, zimekwisha timia. Na mmekwisha ona kwa macho yenu kuwa, Waislam wangapi wamekuwa kama Mayahudi na wangapi wanaonekana katika mavazi ya Wakristo. Kwa hiyo hapana budi kukiri habari za bishara ya tatu vile vile. Yaani kama Waislamu, baada ya kufuata desturi za Mayahudi na Wakristo, wamepata sehemu ya ubaya wao, vivi hivi ni haki kwa Waislam ya kwamba baadhi yao wapate vyeo vya watakatifu waliotangulia katika wana wa Israeli.

Bila shaka ni kumdhania vibaya Mwenyezi Mungu kwamba Amewafanya Waislam washirika wa Mayahudi, lakini hakuwapa sehemu hata kidogo katika daraja ya Manabii na Mitume wao! Basi ilikuwaje umati huu kuwa bora kuliko nyimati zote? Bali umati huu wamekuwa wabaya kuliko nyimati zote. Maana wamepewa kila namna ya ubaya wao lakini hawakupewa hata sehemu moja ya wema wao. Je! Haina haja ya kuwa mmojawapo katika Waislam awe na sifa za Manabii na Mitume, ambaye awe mrithi wa Manabii wote wa Waisraeli na adhihirike katika tabia yao?

Naam, inahitajiwa! Maana ni mbali na rehema ya Mwenyezi Mungu kuwaumba katika umati huu siku hizi, maelfu na maelfu kama Mayahudi na kuwaingiza maelfu na maelfu katika dini ya Kikristo, lakini Asidhihirishe hata mtu mmoja atakayekuwa mrithi wa Manabii wa kwanza na kupata neema zao walizozipata, ili itimizwe bishara iliyomo katika aya hii; *Ihdinas-swiratwalmustaqiym. Swiratwa lladhiyna an-'amta 'alaihim,* kama ilivyotimizwa bishara ile ya kuwa Waislam watakuwa Mayahudi na Wakristo!

Na kama umati huu ulivyopewa maelfu ya majina mabaya na inathibitika katika Quran na hadithi za Mtume, amani ya

Mungu juu yake, pia ya kwamba kuwa Mayahudi ni katika ajali yao, basi katika hali ya namna hii inatakiwa katika fadhili za Mungu ya kwamba kama Waislam wamechukua kwa Wakristo vitu vibaya, vivi hivi wawe warithi wa mambo yao mema. Kwa hiyo, Mwenyezi Mungu ametoa habari njema katika aya hii ya Sura ya Alhamdu: *Ihdinas-swiratal mustaqiym*, kuwa baadhi ya watu wa umati huu watapata neema ya Manabii waliotangulia, wala hawatakuwa Mayahudi au Wakristo tu. Wala haitatokea ya kwamba wachukue ubaya wao tu wala wasipate wema wao.

Juu ya jambo hili, Mwenyezi Mungu Amebainisha katika sura ya *Tahrim* pia. Na Alisema kuwa baadhi ya watu wa umati huu watafanana na *Mariamu Swiddiqa,* aliyeshika utawa na utakatifu, ndipoakapuliziwatumbonimwakerohoyaIsanahumoakazaliwa Nabii Isa (amani ya Mungu juu yake). Vivi hivi ilikuwamo katika aya hii habari ya siri ya kwamba mmoja wa umati huu, kwanza atapata cheo cha Mariamu, kisha atapuliziwa roho ya Isa, halafu kwa Mariamu atatokea Isa, yaani yule mtu atahamishwa kutoka katika sifa za Mariamu kupelekwa katika sifa za Isa. Kama vile sifa zake (za) kuwa Mariamu zimekuwa sababu ya kuwa kwake Isa. Na kwa njia hii mtu yule ataitwa *Ibni Mariamu*.

Basi kwa hiyo, kama ilivyoandikwa katika kitabu changu *Barahiyne Ahmadiyya,* katika ukurasa 241, kwanza nimeitwa kwa jina la Mariamu katika ufunuo wa Mwenyezi Mungu; na ufunuo wenyewe ni huu: *Annaa laki hadha* -Yaani ewe Mariamu umepata wapi neema hii. Na vile vile limebainishwa jambo hili katika ufunuo mwingine ulioandikwa katika ukurasa wa 226: *Huzzi ilaiki bijidh'innakhlati* yaani 'Ewe Mariamu tikisa shina la mtende'. Na baada ya haya, katika ukurasa 496 wa *Barahine Ahmadiyya,* ufunuo huu umeandikwa: *Yaa Maryamu-skun anti wa zaujukil jannata nafakhtu fiyki minladunniy ruwhasswidqi,-Ewe* Mariamu ingia pamoja na wapenzi wako katika Janna (Pepo),

Nimekupulizia roho ya ukweli.

Mwenyezi Mungu katika maneno haya, Ameniita *Roho ya Ukweli.* Na haya ni sawa na aya hii; *Wa nafakhna fiyhi min ruwhinaa*-Tukampulizia roho yetu. Basi hapa, kwa njia ya mfano, roho ya Isa, ambayo huitwa kwa jina la *Roho* ya *Ukweli,* ilipuliziwa katika tumbo la Mariamu.

Tena mwishoni, katika *Barahini Ahmadiyya* ukurasa 556, habari ya kuzaliwa kwa Isa aliyekuwamo katika tumbo la Mariamu, ilikuja kwa ufunuo huu: *Ya Isa inniy mutawaffika wa rafiuka ilayya wajailu lladhina tabauka fauqa lladhina kafaruw ilaa yaumil qiyama,*yaani, 'Ewe Isa! hakika Mimi Nitakufisha na Nitakunyanyua kwangu, na Nitawaweka waliokufuata juu ya waliokukataa mpaka siku ya Kiyama. Katika ufunuo huu nimeitwa kwa jina la Isa. Na ufunuo huu umedhihirisha kuwa, yule Isa aliyetajwa kupuliziwa roho yake katika ufunuo ulioandikwa katika ukurasa 496 wa *Barahini Ahmadiyya,* amekwisha zaliwa. Kwa sababu hii nimeitwa Isa bin Mariamu. Kwani cheo changu cha Isa kilizaliwa katika cheo cha Mariamu kwa upulizio wa Mungu. Tazameni maneno haya ya ufunuo katika ukurasa 469 na 556 wa *Barahini Ahmadiyya*[36].

---

36 *Barahini Ahmadiyya* ndicho kitabu cha kwanza kilichoandikwa na Seyidna Ahmad (amani ya Mungu juu yake) kabla ya kudai kwake kuwa yeye ndiye Masihi Aliyeahidiwa. Kitabu hiki kina jalada tano kielezacho ukweli wa Mtume Muhammad, ubora wa Quran na ukamilifu wa mafundisho ya dini ya Kiislam. Mwanzoni mwa kitabu hiki ilitangazwa ya kwamba atakayevunja dalili zinazoeleza ukweli na ubora wa Uislam, hata sehemu kidogo tu, atapewa zawadi ya rupia elfu kumi. Ikumbukwe kwamba kitabu hiki kilipoandikwa, watu wa dini mbali mbali walikuwa wanashughulika kuhakikisha ya kwamba mafundisho ya Kiislam hayana maana na Mtume Muhammad s.a.w. ni mtu mwongo. Kwa mashambulio ya namna hii ilikuwa inaonekana kama ni fedheha kushika dini ya Islam.

Seyidna Ahmad, amani ya Mungu juu yake, alipoona hali ya namna hii, alihuzunika sana, na akasimama kama mwanamume na kwa nguvu za Mwenyezi

Na jambo hili limebainishwa katika sura *Tahrim* wazi wazi, kwa njia ya bishara. Yaani Isa bin Mariamu atazaliwa katika umati huu kwa njia hii kuwa, mtu mmoja katika umati huu atafanywa Mariamu kwa sifa na baadaye huyo Mariamu atapuliziwa roho ya Isa. Mwisho mtu huyo atazaliwa katika roho ya Isa baada ya kulelewa muda kidogo katika hali ya sifa za Mariamu. Hivyo ataitwa Isa bin Mariamu.

Hii ndiyo habari ya Masihi wa Muhammad s.a.w. iliyobainishwa katika sura ya *Tahrim* katika Quran tukufu kabla ya miaka elfu moja na mia tatu, ambayo Mwenyezi Mungu Aliieleza tafsiri yake kwa ufunuo wake uliomo katika kitabu kiitwacho *Barahine Ahmadiyya.* Quran ipo, isomeni na upande mwingine, isomeni *Barahine Ahmadiyya,* kisha fikirini kwa uadilifu na akili na kwa kumwogopa Mungu, kuwa bishara ile iliyomo katika sura ya *Tahrim:* yaani mtu mmoja katika umati huu vile vile ataitwa Mariamu, kisha katika Mariamu atafanywa Isa, ilionekanaje ukweli wake kwa ufunuo ule uliomo katika *Barahini Ahmadiyya?* Na je! Haya ni katika uwezo wa binadamu? Ni hiyari yangu? Na je, nilikuwapo wakati ilipoteremshwa Quran, ili niseme kuwa niteremshiwe aya moja itakayonifanya Ibn Mariamu? Au inawezekanaje kwangu kufanya hila kabla ya leo miaka

---

Mungu, akabatilisha kwa dalili madhubuti, mafundisho ya dini nyinginezo na kuhakikisha, katika kitabu chake hiki kuwa, Quran ndicho kitabu chenye mwongozo hasa. Na Muhammad ndiye Mtume hasa, ambaye kwa kumfuata, mtu anaweza kupata radhi ya Mungu. Waislam walipopata kitabu hiki katika mashindano yaliyokuwapo, wakafurahi na wakaona kuwa wamekuwa wenye nguvu sana. Hata mmoja wa masheikh wakubwa, aliyekuwa adui wa Seyidna Ahmad a,s. baada ya kujitangaza kwake kuwa yu Masihi Aliyeahidiwa, akaandika hivi baada ya kukisoma kitabu hiki: ”Hiki ndicho kitabu kisicho mfano kwa ubora wake katika karne kumi na tatu zilizopita, na mtungaji, bila shaka, amepigania Uislamu kwa nguvu na mali yake na kalamu yake na kwa ulimi wake; na uimara aliouonyesha katika mambo haya yote, hakuna mfano wake katika karne kumi na tatu zilizotangulia. Naye, kwa kutunga kitabu hiki, amefanya kazi kubwa ya dini ya Islam, naye kwa yakini atapata malipo mema kwa Mola wake”.
(Mfasiri).

ishirini au ishirini na mbili iliyopita au zaidi kuliko hii, na kuzua ufunuo na kujiita kwanza Mariamu na halafu baada ya muda mrefu nikazua ufunuo huu, kuwa kama Mariamu wa kwanza, nami vile vile nimepuliziwa roho ya Isa. Na mwishoni nikaandika katika *Barahini Ahmadiyya* Ukurasa 556, kuwa 'sasa mimi nimegeuka kuwa Isa!' Hasha!

Enyi wapenzi, fikirini na muogopeni Mwenyezi Mungu! Hiki si kitendo cha mwanadamu kabisa. Hakika hii ni hekima kubwa na ni maneno ya fumbo kabisa, ambayo hayafumbuliwi kwa upesi. Lau kama ingalikuwa ni hila yangu, nisingaliandika katika *Barahini Ahmadiyya,* ambacho sasa muda mrefu umepita toka kuandikwa kwake, kwamba Nabii Isa atashuka duniani mara ya pili kutoka mbinguni. Sababu Mwenyezi Mungu Alikuwa Anajua kuwa daIili hii itakuwa dhaifu baada ya kulijua jambo hili. Kwa hivyo, kama Yeye Aliniita Mariamu katika sehemu ya tatu ya *Barahine Ahmadiyya*, tena kama ilivyodhihirika katika *Barahini Ahmadiyya,* nililelewa kwa miaka miwili katika sifa za Mariamu na nilikuwa nikikua kwa siri. Baadaye, ilipokwisha miaka miwili, nilipuliziwa roho ya Isa. Na nilipata mimba kwa njia ya mfano, kama ilivyotajwa katika ukurasa 469 wa *Barahini Ahmadiyya,* sehemu ya nne. Na baada ya kupita miezi isiyozidi kumi, nilifanywa kuwa Isa kutoka Mariamu, kwa ufunuo wake ulioandikwa katika ukurasa 554 katika sehemu ya nne ya kitabu hiki cha *Barahine Ahmadiyya.*

Na pamoja na haya, wakati wa kuandika kitabu hiki cha *Barahine Ahmadiyya,* Mungu Hakunieleza siri hii iliyofichwa. Naam, niliteremshiwa ufunuo huu wote na Mungu, na umeandikwa katika *Barahine Ahmadiyya;* lakini sikuambiwa maana yake na utaratibu wake. Kwa sababu hii niliandika katika *Barahini Ahmadiyya,* imani iliyokuwa tu ya mila (iliyokuwa imeenea), iIi iwe ushahidi juu ya usafi wa nafsi yangu. Sikuandika haya kwa

ufunuo, kwa hivi maandishi yangu haya, ya kwamba Nabii Isa atashuka mbinguni, yasiyokuwa ya ufunuo, hayawezi kuwa ni hoja juu yangu ili wahalifu wapate kunilaumu. Kwani mimi sijadai kwamba najua siri mimi mwenyewe pasipo Mwenyezi Mungu kunifahamisha. Mpaka wakati ule Mwenyezi Mungu, kwa sababu ya hekima Yake, Alipenda kuwa nisifahamu baadhi ya siri za *Barahine Ahmadiyya* nilizofunuliwa. Lakini wakati maalumu ulipofika, nikafahamishwa na Mwenyezi Mungu nikajua siri zile; hapo ndipo nikafahamu kuwa si jambo jipya kudai kwangu kuwa mimi ni Masihi Aliyeahidiwa, bali ni lile lile lililoandikwa katika *Barahine Ahmadiyya* mara kwa mara, tena wazi wazi.

Na hapa vile vile mimi naeleza ufunuo mwingine. Nami sifahamu kuwa kama nimeutangaza ufunuo huu katika gazeti lolote kabla ya sasa au hapana, lakini nakumbuka ufunuo huu nimewaeleza watu wengi nao umeandikwa katika daftari yangu. Ufunuo huu nilifunuliwa wakati ule nilipoitwa na Mungu kwa jina la Mariamu. Na kisha nilipata ufunuo mwingine kwamba nimepuliziwa roho ya Isa. Na baadaye, nilifunuliwa ufunuo huu: *Fa ajaaahal makhadhu ilaa jidh-'in nakhlati qaalat yaa laitani mittu qabla hadha wa kuntu nasyam mansiyyaa.* "Basi"uchungu ukampeleka "Mariamu", yaani mimi, "penye shina la mtende", yaani nikapata bahati ya kuonana na masheikh wajinga na wapumbavu wasiokuwa na matunda ya imani walioniita kafiri kunitukana na kuniweka katika tufani la uhalifu wao. Ndipo wakati huu wa taabu, alisema Mariamu, yaani mimi: "Laiti ningalikufa kabla ya taabu hii na ningalikuwa mwenye kusahauliwa". Mradi katika haya ni kule kupiga makelele kwa wahalifu kulikoanzishwa na masheikh wote walipoona hawawezi kuyavumilia madai yangu. Na walitaka kuniangamiza kwa kila hila. Basi Mwenyezi

Mungu Amebainisha katika ufunuo huu hali yangu hii wakati nilipopata huzuni kubwa na uchungu mwingi nafsini mwangu kwa sababu ya uhalifu wa wapumbavu na makelele yao.

Na vile vile nilifunuliwa ufunuo mwingine juu ya jambo hili kama:

*Laqad ji'ti shai-an fariyya maa kaana abuwki mra-a sayyian wamaa kaanat ummuki baghiyya,* na pamoja na haya vile vile nilifunuliwa kuwa: *Alaisallahu bikaafin 'abdahu walinaj 'alahu aayatallinnasi wa rahmatamminnaa wakaana amram maqdhiyyaa qaulal haqqi lladhiy fiyhi tamtaruwna.* Tazameni yaliyoandikwa katika *Barahini Ahmadiyya* ukurasa 516. Tafsiri: "Na watu walisema: Ewe Mariamu umelionyesha jambo la ubaya na chuki namna gani lisilotakasika; maana babaako[37] na mamaako hawakuwa watu wa namna hii! Lakini Mwenyezi Mungu Atamtukuza mtumishi Wake katika masingizio yote na Atamfanya awe ishara kwa watu. Na jambo hili lilikusudiwa toka zamani na lilikuwa la kutendwa. Huyu ndiye Isa bin Mariamu ambaye watu wanamtilia shaka! Lakini hiyo ndiyo kauli ya haki". Maneno haya yote yameandikwa katika *Barahini Ahmadiyya.*

Na funuo hizi zote kwa hakika ni aya za Quran tukufu, zinazohadithia habari za Nabii Isa na mama yake Mariamu. Na Alisema Mwenyezi Mungu katika aya hizi ya kwamba; "Sisi

Tutamfanya huyu mtu aliyesingiziwa na watu kuwa ni mwana

37 Ufunuo huu umenikumbusha kuwa alikuwapo sharifu mmoja katikamji wa Batala, jina lake lilikuwa *Fazal Shah* au *Mehr Shah.* Na alikuwa anampenda sana baba yangu. Alipoambiwa kudai kwangu kuwa Masihi Aliyeahidiwa, alilia sana akasema: Baba yake (baba yangu) alikuwa mtumwema sana, lakini huyu mtoto amekuwa namna gani? Baba yake alikuwa na tabia njema na alikuwa mbali na mambo ya kuzua, na alikuwa Mwislam kabisa mwenye roho safi. Vivi hivi na watu wengi wamesema kuwa 'wewe, kwa kufanya hivi, umeweka aibu juu ya jamaa zako wote'.

wa zina, awe ishara kwa watu na rehema itokayo Kwetu. Na ndiye Masihi aliyekuwa anangojewa”. Na katika maneno ya ufunuo, mradi wa Isa na Mariamu ni mimi. Na ilisemwa juu yangu, “Sisi tutamfanya ishara” na ilisemwa vile vile, “Huyu ndiye Isa bin Mariamu aliyekuwa anangojewa, na ambaye watu wanamtilia shaka; lakini kwa hakika, yeye ni yule anayengojewa na hii ndiyo kweli. Shaka ya watu wanayomtilia ni kwa sababu ya ujinga wao ambao hawafahamu siri za Mungu na wanapenda sura tu wala hawatazami hakika.”

# SURA YA TANO

## Jinsi Masihi wa Muhammad alivyofanana na Masihi wa Musa

Na ikumbukwe kwamba moja la makusudio makubwa ya Suratil- Faatiha ni dua hii: *'Ihdina-sswiraatwal mustaqiyma swiraatwal ladhiyna an'amta 'alaihim'* - Tuongoze katika njia iliyonyoka, njia ya wale Uliowapa neema. Na kama ulivyoombwa 'Mkate' katika dua za Injili, vivi hivi zimeombwa katika dua hii ya Quran: *neema* zile zote walizopewa Manabii na Mitume waliotangulia.

Na malinganisho haya baina ya dua hizi mbili ni ya ajabu na yanafaa kufikiriwa: Kama ilivyokubaliwa dua ya Nabii Isa a.s., Wakristo wakapata chakula kingi kwa dua hii, basi hivi ndivyo dua ya Quran imekubaliwa kwa mikono ya Mtume Muhammad, amani ya Mungu juu yake, na Waislamu waliohalisika na wenye utukufu hasa, waliokamilika katika uongofu, wakafanywa warithi wa Manabii wa Waisraeli.

Pia kwa sababu ya kukubaliwa dua hii, ametumwa Masihi Aliyeahidiwa katika umati huu. Ingawa wengi katika watu wema wa umati huu wamepata sehemu ya neema ya Manabii wa Waisraeli, lakini Masihi Aliyeahidiwa katika umati huu amesimamishwa pahali pa Nabii Isa, aliyekuwa Masihi wa Waisraeli, wazi wazi kwa hukumu ya Mungu na kwa idhini Yake, ili udhihirike mfano baina ya Silsila ya Musa na Silsila ya Muhammad, amani ya Mungu juu yake, Na kwa sababu hii Masihi huyu wa umati wa Muhammad amefananishwa kwa kila namna na mwana wa Mariamu. Hata amejaribiwa kwa taabu kama alivyojaribiwa Masihi wa Waisraeli.

Na kama Isa bin Mariamu alivyoumbwa kwa mpulizio wa Mungu, vivi hivi na Masihi wa umati wa Muhammad, kukua kwake katika tumbo la Mariamu kulikuwa kwa kupuliziwa na Mwenyezi Mungu tu, sawa na miadi iliyomo katika sura ya *Tahrim.* Na kama makelele ya maadui yalivyotokea sana wakati wa kuzaliwa Isa bin Mariamu; na maadui vipofu walimwambia Mariamu: *Laqad ji'ti shai'an fariyaa*[38] - Umeleta kitu cha kuchukiza. Vivihivi ilisemwa hapa na makelele mengi yamepigwa na maadui wetu. Na kama Mwenyezi Mungu Alivyowajibu maadui juu ya Isa alipozaliwa na Mariamu: *Walinaj'alahu aayata llinaasi wa rahmatam minnaa Wakaana amran makdhiyyaa - Sisi* Tutamfanya awe Ishara kwa watu na rehema itokayo Kwetu, na jambo hili lilikuwa limekusudiwa[39]. Jawabu hili Mwenyezi Mungu Amewajibu maadui zangu katika *Barahine Ahmadiyya* wakati Aliponizalisha kwa kiroho kwa njia ya istiara. Na Aliwaambia maadui zangu kuwa ninyi hamwezi kumwangamiza kwa hila zenu; nami Nitamfanya awe ishara ya rehema kwa watu na jambo hili lilikuwa limekusudiwa toka mwanzo.

Tena kama maulamaa na masheikh wa Mayahudi walivyomwita Masihi kuwa ni kafiri. Na mmoja wa Mayahudi aliyekuwa mwenye shari sana na aliyekuwa na elimu aliandika tangazo la Ukafiri wa Isa. Na jinsi maulamaa wengine wa Kiyahudi walivyosadikisha na kulitilia saini zao tangazo hilo, hata masheikh wa Baitul-Mukaddas ambao walikuwa wenye kushika sana *Hadithi* kuliko Taurati walilipiga tangazo hili mihuri ili kusadikisha ukafiri wa Nabii Isa[40]. Ndivyo hivyo

38 Sura 19 aya 28

39 Sura 19: 22

40 Wakati wa Nabii Isa, amani ya Mungu juu yalke, ingawa Mayahudi walikuwa na vikundi vingi, lakini wanaofahamiwa wenye haki walikuwa ni vikundi viwili. Cha kwanza ni wale waliokuwa wamekamata Taurati na walikuwa wanatoa mambo ya dini katika kitabu hiki tu. Cha pili walikuwa ni *Ahli-Hadith,* yaani wenye kutanguliza hadithi juu ya Taurati, na kuifahamu kuwa ni hakimu juu ya Taurati. Na watu wa hadithi walikuwa wamezagaa kwa

hayo yote yalivyonipata, yaani maadui wangu wamefanya hivi hivi. Na kama ilivyokuwa baada ya kumwita lsa kuwa kafiri, aliudhiwa sana na alitukanwa matusi mabaya na viliandikwa vitabu vya kumtukana; hivi ndivyo nami ilivyofanywa na maadui zangu. Kana kwamba baada ya miaka elfu na mia nne Masihi mwenyewe amefufuliwa na ni kana kwamba Mayahudi pia wamefufuliwa. Huu ndio mradi wa ubashiri ule Alioonyesha Mwenyezi Mungu zamani katika kauli yake: *Magh-dhuwbi 'alaihim* - Walioghadhibikiwa na Mungu. Lakini watu hawa (maadui zangu) hawakusubiri mpaka wasiwe wenye kukasirikiwa kama Mayahudi.

Aliweka Mwenyezi Mungu, kwa mikono yake, jiwe moja la kufananisha na amenifanya Masihi wa Waislamu na Amenituma katika karne ya kumi na nne baada ya Mtume Muhammad, amani ya Mungu juu yake; kama alivyotumwa Masihi wa Waisraeli katika karne ya kumi na nne baada ya

---

wingi katika miji ya Waisraeli. Hata walifuata hadithi zenye kuhalifu Taurati. Na walikuwa wanasema kuwa baadhi ya mambo ya sheria kama mambo ya ibada na desturi ya vitendo na kanuni za malipo, hazimo katika Taurati. Na mambo haya yanapatikana katika hadithi. Na jina la kitabu cha hadithi zao ni *Talmud.* Katika kitabu hiki mnapatikana hadithi za wakati wa kila Nabii, na hadithi hizi zilikuwa zinasemwa kwa vinywa tu, na baada ya muda mrefu ziliandikwa. Kwa hivi zimechanganyika na hadithi za uwongo. Na kwa sababu hii Mayahudi wametawanyika vikundi 73. Na kila kikundi kina hadithi zake mbali mbali. Na wale wenye kufuata hadithi walikuwa hawaangalii Taurati na wakafuata sana hadithi. Na Taurati ikawa kama kitu kilichoachwa; kama maneno ya Taurati yakiwa sawa na hadithi yanakubaliwa, na yakiwa si sawa na hadithi hukataliwa. Wakati ule alizaliwa Nabii Isa na yeye alieleza hasa kwa wale waliokuwa wakishika hadithi na kuiheshimu kuliko Taurati. Na ilielezwa katika vitabu vya Manabii zamani, kuwa Mayahudi watakapotawanyika vikundi na kuacha Kitabu cha Mungu na kufuata hadithi, atatumwa kwao hakimu mwenye uadilifu atakayeitwa Masihi na hawa hawatamkubali na mwisho wake watateremshiwa adhabu kali. Na adhabu hii ilikuwa Tauni. Mwenyezi Mungu Apishe mbali.

Nabii Musa. Na Mwenyezi Mungu Anawaonyesheni ishara kubwa kubwa kwa ajili yangu; wala chini ya mbingu hakuna yeyote awezaye katika maadui zangu, Waislamu au Wakristo au Mayahudi au wengine, kushindana na ishara zile. Na uwezo gani wa binadamu ambaye ni dhaifu na mnyonge kushindana na Mwenyezi Mungu? Hili jiwe la msingi limewekwa na Mungu. Kila mwenye kutaka kulivunja jiwe hili hawezi kulivunja. Lakini jiwe hili likimwangukia mtu linamponda kabisa. Kwani jiwe hili ni jiwe la Mungu na mkono ni mkono wa Mwenyezi Mungu. Na jiwe jingine limetengenezwa na maadui zangu na wameliweka. Yaani walifanya vitendo katika kushindana nami kama Mayahudi walivyofanya katika wakati ule.

Wamenishtaki hata kwenye kesi ya mauaji kwa kutaka kuniangamiza. Na Mwenyezi Mungu Alinieleza haya tangu zamani. Kesi niliyoshtakiwa ilikuwa kubwa kuliko kesi ya Nabii Isa bin Mariamu. Kwani kesi ya Nabii Isa ilikuwa kwa sababu ya hitilafu ya dini, na jambo hili kwa hakimu halikuwa kubwa, bali lilikuwa hafifu hata halikuwa kitu. Lakini kesi niliyoshtakiwa mimi ilikuwa ya kusingiziwa mauaji. Na kama masheikh wa Kiyahudi walivyotoa ushahidi dhidi ya Nabii Isa, vile vile ikawa hapana budi kwa baadhi ya masheikh miongoni mwa Waislamu kutoa ushahidi dhidi yangu katika kesi yangu. Kwa hiyo Mwenyezi Mungu Akamchagua kwa jambo hili Sheikh mmoja jina lake Maulawi Muhammad Hussein Batalwi. Alikuja kwa maringo hali amevaa joho refu ili kutoa ushahidi; na akahudhuria katika baraza la hakimu kama alivyohudhuria mkubwa wa makuhani katika baraza la hakimu kutoa ushahidi ili kumsulubu Masihi juu ya msalaba.

Hapakuwa na hitilafu, ila yule mkubwa wa makuhani alipewa kiti katika korti ya hakimu Pilato, kwa sababu wakubwa wa Mayahudi walikuwa wakipewa kiti katika hukumu ya ufalme

wa Rumi. Na baadhi ya Mayahudi walikuwa Mahakimu. Kuhani alipata kiti kwa kufuatisha kawaida ya ufalme; na Masihi alisimama mbele yake kama mwenye kosa. Lakini katika kesi yangu mambo yote hayakuwa sawa na haya. Yaani Captain Douglas, aliyekuwa hakimu kama vile Pilato, alinipa kiti kinyume cha matamanio ya maadui zangu. Na Pilato (Cap. Douglas) huyu alionyesha tabia nzuri zaidi kuliko zile za Pilato wa Nabii Isa. Sababu yeye, katika kesi hii yote, hakuacha kutazama uadilifu bali alifuata uadilifu kwa ushujaa na uimara, wala hakusikiliza maombi ya mahakimu wakubwa, wala hakubadilisha moyo wake kwa sababu ya kupendelea kabila na dini yake; bali aliendelea kwa uadilifu sawasawa. Na alionyesha namna ya ajabu kubwa katika uadilifu wake. Na alisimamisha mfano wa uadilifu na kwa hiyo amejiweka mfano kwa ajili ya mahakimu wengine. Hata aliwafanya watu wa kabila lake wajivune kwa sababu ya uadilifu wake ulioonyeshwa kwa ushujaa wakati ule. Uadilifu ni kazi ngumu; mtu hawezi kuutekeleza sawasawa mpaka akae kiti cha hukumu kwa kuacha mafungamano yoyote.

Hakika sisi tunashuhudia kushuhudia kwa kweli kuwa Pilato huyu, (Cap. Douglas), alitekeleza faradhi yake sawasawa ingawa Pilato wa zamani aliyekuwa Mrumi hakutekeleza faradhi yake sawasawa. Na kwa sababu ya woga wake Masihi alipata mashaka na taabu nyingi.

Tofauti hii inafaa ikumbukwe na wafuasi wetu mpaka mwisho wa dunia, kama vile wafuasi wetu watakavyozidi kwa mamilioni na mamilioni, hivi hivi hakimu huyu mwenye uadilifu na mwenye nia nzuri, atakumbukwa ukumbuko mzuri. Bahati yake ni nzuri mno Mwenyezi Mungu Kumchagua kwa kuhukumu kesi hii. Mtihani huu una ugumu ulioje kwa kujiwa kwake na watu wawili: mmoja akiwa ni mhubiri wa dini

yake na mwingine ni adui wa dini yake. Na vile vile baada ya kuambiwa hakimu kuwa huyu (yaani mimi) ni adui mkubwa wa dini yake! Lakini Pilato huyu (Cap. Douglas) ameweza kubeba mzigo wa mtihani huu kwa kukazana kabisa. Na alionyeshwa kurasa mbalimbali za vitabu vyangu mlimo na maneno yenye kufahamiwa kuwa ni yenye kuhitilafiana sana na dini yake ya Kikristo, lakini pamoja na haya yote hayakutokea mabadiliko usoni mwake. Kwani alikuwa amekwisha fahamu hakika ya kesi hii kwa ajili ya roho yake safi. Na Mwenyezi Mungu Alimsaidia kutafuta asili ya kesi hii kwa nia safi, na Alimfunulia ukweli rohoni mwake na Alifunguliwa mambo ya haki. Na alifurahi vikubwa mno kwa kuiona njia ya uadilifu, lakini aliyeshitaki hakupewa kiti. Na alipokuja Maulawi Muhammad Hussein, kama mkubwa wa Makuhani kutoa ushahidi dhidi yangu, aliniona nimekaa juu ya kiti na hakuniona katika hali mbaya kama alivyokuwa anataka sana kuniona, hapo alifahamu kuwa ni heri naye aombe kiti ili awe sawa, nami. Basi akaomba kiti kwa Pilato (Cap. Douglas). Lakini Pilato huyu alimtolea ukali na alisema kwa nguvu, "hukupewa wewe kiti wala baba yako, katika ofisi yetu hakuna maagizo ya kukupa kiti."

Na tofauti hii vile vile inafaa kutazamwa kwa fikara kuwa Pilato wa Mayahudi aliwaogopa Mayahudi na aliwapa baadhi ya mashahidi wao wenye heshima viti, na alimsimamisha Masihi mbele yake kama aliyekosa. Pamoja na kumwonea huruma moyoni hata akawa kama mwanafunzi wake. Na mke wake pia alikuwa ni katika wafuasi wake safi, hata alikuwa akiitwa mtawa. Lakini pamoja na haya yote Pilato alimtoa Yesu, asiyekuwa na kosa, akawapa Mayahudi bila haki kwa sababu ya kuwaogopa. Wala Yesu hakusingiziwa kama mimi nilivyosingiziwa kesi ya kuua, bali ilikuwa kesi ya hitilafu ya imani tu. Lakini yule Pilato wa Rumi moyo wake haukuwa na nguvu na aliogopa kushtakiwa kwa mfalme mkubwa Kaisari.

Na tena kuna mfano mwingine, inafaa kukumbukwa. Masihi alipopelekwa kwa Pilato wa kwanza katika korti; Pilato aliwaambia Mayahudi, ”Mtu huyu simwoni na makosa”. Hivi hivi Masihi wa pili, yaani, mimi, alipopelekwa katika korti ya Pilato wa pili (Cap. Douglas) na Masihi alimwambia Pilato (Cap. Douglas) akaomba kupewa ruhusa kwa siku chache kwa ajili ya kujibu shutuma, kwani alisingiziwa kuua. Pilato wa pili alijibu "Mimi sikusingizii hata kidogo". Kauli hizi mbili za Pilato wawili zimefanana.

Wala hapana hitilafu ila Pilato wa kwanza hakukamilisha neno lake alilosema, na alipoambiwa kuwa atashtakiwa kwa mfaIme Kaisari aliogopa na alimtoa Masihi akawapa Mayahudi wadhalimu. Ijapokuwa Pilato alihuzunika kwa kumtoa Yesu kwa Mayahudi, na mke wake vile vile alihuzunika, kwani walikuwa wanamwamini sana. Lakini alishindwa, kwa sababu ya woga wake, na makelele ya Mayahudi. Naam, aljitahidi kwa jitihada kubwa, kwa siri, kumwokoa Yesu asisulubiwe msalabani. Na alifuzu katika jitihada yake lakini baada ya Yesu kutundikwa msalabani na baada ya kuzimia kwa sababu ya maumivu sana alikuwa kama mwenye kufa. Na mwishoni kwa sababu ya jitihada ya Pilato wa Rumi, Masihi aliokoka katika kifo cha msalabani. Na ilikwisha sikilizwa dua ya Masihi aliyoomba kwa Mwenyezi Mungu[41] kuokolewa. Tazameni Waebrania mlango wa 5 aya 7.

Baadaye Masihi alikimbia kwa siri kuitoka nchi ile na kwenda

41 Na Masihi mwenyewe pia alibashiri kwa njia ya unabii kuwa "Wala hakitapewa ishara ila ishara ya Nabii Yunus" (Matt. 12: 39). Yesu alionyeshakatika kauIi hii kuwa kama, Nabii Yunus alivyoingia katika tumbo la nyangumi na hali yu mzima na kutoka hali yu mzima, hivi hivi naye ataingia katika kaburi akiwa hai na atatoka akiwa hai. Iliwezekanaje kutimia bishara hii ikiwa Masihi hakutoka mzima msalabani na kuingia mzima katika kaburi? Na kauli ya Yesu kuwa "Hakitapewa ishara nyingine ila ishara ya Nabii Yunus" inavunja maneno ya wale wanaofahamu kuwa yeye ameonyesha Ishara ya kuchukuliwa mbinguni.

Kashmiri Bara Hindi, halafu alifia huko. Na ninyi mmekwisha sikia kuwa kaburi lake liko katika mtaa wa Khan Yar. Na haya yote, kuokoka msalabani na kukimbilia Kashmir, yalitokea kwa juhudi ya Pilato. Lakini pamoja na haya, kitendo chake na jitihada yake vilichanganyika na woga. Lau kama Pilato angechunga kauli yake aliyosema kuwa "Mimi sioni juu yako makosa" na kumwachilia Yesu, isingekuwa ugumu juu yake, naye alikuwa anaweza kumwachilia, lakini aliogopa kushtakiwa kwa Kaisari.

Lakini Pilato wa pili, yaani Captain Douglas, hakuogopa makusanyiko ya Mapadre na hali ufalme ulikuwapo wa Ukaisari. Lakini Kaisari wa sasa, yaani Malkia Victoria alikuwa ni mwema sana kuliko Kaisari wa siku zile. Kwa hivi haikuwezekana kwa yeyote kumwogofya hakimu huyu kwa Malkia ili aogope na aache uadilifu. Walakini vitimbi vibaya vya wahalifu wa Masihi wa mwisho vilikuwa vikubwa kuliko vya Masihi wa kwanza na walikusanyika wahalifu wangu na wakubwa wa kila taifa ili kuniangamiza. Lakini Pilato wa pili (Cap. Douglas) alitekeleza kanuni ya uadilifu wala hakuwa na woga.

Tena siku ile nilipohukumiwa na kuachiliwa aliletwa mwizi mmoja wa jeshi la wokofu mbele ya hakimu: haya yote yalitokea ili kutimiza mfano, kwani pamoja na Yesu pia aliletwa mwizi. Lakini mwizi huyu hakuvunjwa mifupa yake, kama alivyovunjwa mwizi aliyeletwa pamoja na Yesu, na hakusulubiwa bali alipewa adhabu ya kufungwa miezi mitatu tu.

# SURA YA SITA

## Njia zingine za Mwongozo

**Njia iliyoelezwa na Quran.**

Sasa tunarudia maneno yale ya kwanza na tunaandika kuwa, sura ya Alhamdu imekusanya ndani yake, mambo ya hekima na mambo ya maarifa na mambo ya elimu ya kiroho kwa kiasi ambacho kikiandikwa chote, haiwezekani kukusanyika katika daftari moja. Tazameni dua hii ya hekima iliyofundishwa katika sura hii, yaani; *'Ihdinas swiraatwal mustaqiyma'* - tuongoze katika njia iliyonyooka, mmekusanyika mambo yote. Na bila shaka huu ni ufunguo wa makusudio yote ya dunia na ya dini. Ni dhahiri kuwa hatuwezi kujua hakika ya kitu, wala hatuwezi kupata faida na manufaa yake mpaka tujue njia iliyonyooka ya kupatia kitu kile.

Ni vigumu kabisa, hata haiwezekani yeyote kufuzu katika mambo magumu ya dunia ikiwa mambo ya ufalme au mambo ya kazi ya uwaziri au mambo ya kazi ya uaskari na kazi ya vita, au mambo ya elimu ya hekima ya dunia au njia za kupima ugonjwa na mambo ya elimu ya mimea; mpaka ajue njia iliyonyooka ya kuyapatia mambo haya yote, na ajue jinsi ya kuyaanzisha mambo haya. Na kila mtu mwenye akili anajilazimisha kufikiri kwa muda mrefu, usiku na mchana katika wakati wa taabu, ili aongoke katika njia iliyonyooka na atoke katika shida na taabu hiyo. Kila jambo jipya na kila chumo na kila kazi ngumu, kuyaendesha haya inatakiwa kwanza ipatikane njia iliyo sawa. Hivi hivi kwa kupata makusudi ya dini na dunia, dua hasa ni ile inayoonyesha njia.

Inapopatikana njia iliyo sawa kwa jambo lolote, basi hapana shaka na jambo hilo litapatikana kwa fadhili za Mungu. Uwezo wa Mwenyezi Mungu na hekima Yake imetengeneza njia ya kupatia kila haja. Mathalan haiwezekani kabisa kumponyesha

mgonjwa mpaka ijulikane njia ya kujua asili ya ugonjwa wake, na njia ya kupata kuutibu ambayo moyo ukielekeza kwamba, kwa njia hii kutapatikana kufaulu. Bali utaratibu wote wa dunia hauwezi kuendelea mpaka uwe na njia iliyo sawa. Basi kuomba njia ni lazima kwa yule anayetaka kupata kufaulu katika makusudio yake. Na kupata kustawi katika mwendeleo wa dunia, kwanza kunahitajiwa njia itakayofuatwa.Vivi hivi katika mwendeleo wa dini, na kuwa mpenzi wa Mungu na kupata mapenzi Yake na fadhili Zake, tangu zamani kumehitajiwa kuipata njia.

Kwa hivi ilisemwa mwanzo wa sura ya pili, sura ya Albaqarah, ambayo iko baada ya sura ya Alhamdu: *Huda llilmuttaqiyna* - Umo mwongozo kwa wamchao Mungu[42]. Yaani njia ya kupatikana neema ni hii[43] tunayoieleza Sisi.

Basi dua hii: *Ihdinas swiraatwal mustaqiyma* - tuongoze katika njia iliyonyooka ni dua inayokusanya mambo yote; nayo inamwelekeza mwanadamu katika wakati wa taabu ya dini na dunia, kuwa kitu cha kwanza ambacho ni lazima kwake kukitafuta ni njia iliyonyooka. Ili ayafikie makusudio yake kwa upesi, na aujaze moyo wake yakini na aokoke katika wasiwasi.

Lakini sawa na maagizo ya Injili, mwombaji wa mkate hatachagua njia ya kumpenda Mungu, sababu makusudio yake ni kupata mkate tu. Atakapopata mkate basi tena ana mahitaji gani kwa Mungu? Na kwa sababu hii Wakristo wameteleza katika njia iliyonyooka. Na imefungwa katika shingo zao imani ya ovyo ya kumwita binadamu kuwa mungu. Sisi hatuwezi kufahamu jambo gani linapatikana zaidi katika Yesu mwana wa Mariamu kuliko wengine, hata wakamdhania kuwa yeye ni Mungu. Manabii wengi waliokuwa kabla yake walikuwa

42 Iliombwa katika Suratul-Fatiha dua ya njia iliyonyooka; na katika sura ya pili baada ya kupokea dua hii ilionyeshwa njia ile iliyonyoka.

43 Sura 2 aya 3

wenye miujiza mingi, kama Musa, Alya's na Eliya.

Naapa kwa Mungu Ambaye nafsi yangu imo mikononi Mwake, lau kama Masihi angalikuwa katika zama zangu hizi, asingeweza kabisa kufanya ninayoweza kuyafanya. Wala hangeweza kuwaonyesheni zile ishara zinazodhihirika katika mikono yangu[44], na angeona fadhili za Mungu kwangu ni nyingi kuliko zile alizokuwa nazo. Basi kama hali yangu mimi ni namna hii, fikirini daraja gani ya yule Mtume Mtukufu ambaye mimi ni mtumishi wake. *Dhalika fadhlu llahi yu'tiyhi man yashaau-* Hizi ni fadhili za Mungu Humpa Amtakaye. Hapo kijicho na husuda havifai kitu. Mwenyezi Mungu Anafanya Atakavyo, na anayejitahidi kuvunja maazimio yake, hapati tu hasara katika makusudio yake, bali na baada ya kufa kwake atafuata njia ya jahannam vile vile. Wamekwisha angamia waliokifanya kiumbe dhaifu kuwa Mungu. Na wameangamia hao wasiomkubali Mtume Mtakatifu. Amebarikiwa yule aliyenifahamu. Mimi ni njia ya mwisho katika njia za Mwenyezi Mungu. Na ni nuru ya mwisho katika nuru Zake. Ana bahati mbaya mwenye kuniacha, kwani minghairi yangu sasa vyote ni giza.

**Njia ya pili - Sunna.**

Na njia ya pili waliyopewa Waislamu ili kuwaongoza ni *Sunna.* Yaani desturi, ya vitendo alivyoonyesha Mtume Mtakatifu kwa kueleza hukumu za Quran Tukufu. Mathalan, haionekani katika

---

44 Mtaona, kusadikisha yale ninayosema, katika kitabu changu *Nuzulu Masih* kinachochapwa; na sasa kimekwisha chapwa juzu kumi na kitatangazwa karibuni. Kitabu hiki kimeandikwa kuwa majibu ya kitabu cha Pir Mehr Ali Golarwi, *Tanbure-Chishtiai.* Na iIithibitishwa katika kitabu hiki kuwa Pir Mehr Ali, baada ya kuiba makala ya Muhammad Hussein aliyekufa, alifanya makosa mabaya sana. Hata atasikia uchungu sana baada ya kuyajua. Na yule Mohammad Hussein mwenye bahati mbaya nilivyosema katika I'jazul Masih. Na huyu mwingine mwenye bahati mbaya alikufa kama kutengeneza kitabu hiki ovyo akafedheheka kama nilivyosema kwa amri ya Mungu: *Inniy muhiynun man araada Ihaanataka - Mimi* nitamdhalilisha yule mwenye kutaka kuharibu heshima yako, Fikirini, enyi wenye busara.

Quran hesabu ya rakaa za sala tano ni ngapi; za sala ya asubuhi ni ngapi; za sala nyingine ni ngapi? Lakini Sunna - desturi ya Mtume, amani ya Mungu juu yake, ilionyesha wazi wazi kila kitu. Msidanganywe wala msidhani kuwa Sunna na Hadithi vyote ni kitu kimoja! Hapana! *Sunna* na *Hadithi* ni mbalimbali. Sababu *Hadithi* zilikusanywa baada ya kufariki Mtume Mtakatifu. Lakini *sunna* ilikuwapo pamoja na Quran. Baada ya Quran hisani ya *Sunna* ni kubwa sana juu ya Waislamu.

llikuwa kazi ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake, amani ya Mungu juu yake, kufanya mambo mawili. Kazi ya Mungu kwa kuteremsha Quran ilikuwa ni kuwaambia watu amri Zake kwa kauli Yake. Na kazi ya Mtume, amani ya Mungu juu yake, ilikuwa ni kuwafahamisha watu amri za Mungu kwa vitendo vyake. Kwa hiyo Mtume, amani ya Mungu juu yake, aliwaonyesha watu maneno yale kwa namna ya vitendo, na kwa Sunna, yaani kwa vitendo vyake, alifanya mambo magumu na elimu ngumu kuwa vyepesi. Na kusema kuwa mambo yenye mushkil kufumbuliwa kwake kulitegemea *Hadithi* sivyo. Kwani Uislamu ulikuwa umekwisha simama duniani kabla Hadithi hazijapatikana[45]. Jee, watu hawakuwa wanasali na kutoa zaka na kuhiji, na hawakuwa wanajua haramu na halali kabla hazijakusanywa *Hadithi?* Naam! Walikuwa wanatekeleza haya yote kabla hazijakusanywa *Hadithi* na hata kabla hazijaandikwa.

**Njia ya Tatu - Hadithi.**

Njia ya tatu ya, mwongozo ni *Hadithi.* Sababu *Hadithi* zinatuhadithia mambo mengi ya historia za Kiislam na mambo makuu ambayo imewapasa kuyatenda, elimu na mambo ya

45 *Ahlihadithi* (watu washikao sana mambo ya *hadithi)* wanaita kauli ya Mtume, amani ya Mungu juu yake, na vitendo vyake kuwa ni *Hadithi.* Kila mtu anaweza kuita kadri akili yake inavyomwelekeza. Sisi hatuingii katika shauri lao, lakini kwa hakika *Sunna* ni mbali ambayo Mtume, Amani ya Mungu juu yake, ameisimamisha mwenyewe katika maisha yake; na Hadithi ni mbali ambayo imekusanywa baada ya kufariki kwake Nabii, amani ya Mungu juu yake.

desturi za Kiislam, kwa wazi wazi. Na zaidi ya haya faida kubwa ya *Hadithi* ni kuwa ni mtumishi wa Quran na *Sunna.* Lakini sisi hatupatani na wale wasioiheshimu Quran, kama Mayahudi walivyosema kuwa hadithi zao ni hakimu wa Taurati. Bali sisi tunaona kuwa *Hadithi* ni mtumishi wa Quran na *Sunna.* Ni dhahiri kuwa heshima ya Bwana inazidi kwa kuwako watumishi. Quran ni kauli ya Mwenyezi Mungu, na *Sunna,* ni vitendo vya Mtume, amani ya Mungu juu yake, na desturi zake na *Hadithi* ni shahidi msaidizi wa *Sunna.* Ni makosa kusema kuwa *Hadithi* ni hakimu wa Quran. Hasha! ikiwa yuko hakimu wa Quran, basi Quran yenyewe ni hakimu. Haiwezekani kuwa *Hadithi* yenye daraja ya dhana kuihukumu Quran. Hazikuwa ila ni shahidi msaidizi tu. Kwa hakika Quran na *Sunna,* vimekwisha tekeleza kazi zote na *Hadithi* ni shahidi msaidizi. Basi itamkinikaje *Hadithi* kuihukumu Quran na *Hadithi* ilikuwa haijajulikana wakati ule Quran na *Sunna,* vilipokuwa vinaongoza watu.

Sikilizeni msiseme kuwa *Hadithi* ni hakimu wa Quran, bali semeni kuwa *Hadithi* ni shahidi mwenye kuisadikisha Quran na *Sunna.* Naam, *Sunna* ni jambo linalodhihirisha makusudio ya Quran. Na mradi wa *Sunna,* ni njia ile safi ya Mtume Mtukufu ambayo aliwaelekeza masahaba wake na wakaishika katika mwenendo wao. Jina la maneno yale yaliyoandikwa katika vitabu baada ya miaka mia au mia na hamsini si *Sunna,* bali jina la maneno hayo ni *Hadithi.* Na *Sunna* ni jina la desturi nzuri zinazoonekana katika vitendo vya Waislamu wema toka mwanzo. Na maelfu kwa maelfu ya Waislamu wameendeshwa juu yake.

Ama *Hadithi*, ijapokuwa nyingi ni za dhana, lakini vile vile inafaa kuzifuata kwa sharti zisihalifu Quran na *Sunna.* Hapana shaka kwamba ndani ya *Hadithi* mna hazina ya mambo mengi ya Kiislamu na kuacha kuziheshimu ni kama kukata kiungo

cha dini ya Kiislamu. Lakini ikiwa *Hadithi* haipatani na Quran na *Sunna,* au kuhalifu *Hadithi* yenye kuwa sawa na Quran au *Hadithi* yenye kuhalifu *Sahihi Bukhari,* haifai kuikubali. Sababu kuikubali *Hadithi* ya namna hii kunavunja Quran na *Hadithi* zote zilizo sawa na Quran. Pamoja na haya heshimuni *Hadithi* na pateni faida yake, kwani zimepokelewa kwa Mtume Mtakatifu, amani ya Mungu juu yake, wala msizikadhibishe kama Quran na *Sunna,* havizikadhibishi.

Bali inafaa kwenu kuzingatia *Hadithi* kwa nguvu, hata msitikisike wala msitulizane wala msifanye wala msiache kitendo cho chote ila mpaka iweko hadithi ya kusadikisha haya. Kama ikiwako hadithi yenye kuhalifu mambo ya Quran basi fikirini kwanza ili mpate usawa wake, labda kuhalifu kwake ni kwa sababu ya makosa yenu. Na kama kuhalifu hakukuondoka kwa kila njia, basi iacheni hadithi ya namna hii, sababu *Hadithi* ya namna hii si ya Mtume, amani ya Mungu juu yake. Ikiwa *Hadithi* ni dhaifu lakini inawiana na Quran basi ikubalini *Hadithi* hiyo, sababu Quran inaisadikisha.

Na kama ipo hadithi yenye kuwa na bishara yoyote, na hata iwe dhaifu kwa wenye elimu ya hadithi, lakini bishara ikitimia wakati wenu au kabla yenu, basi sadikini kuwa hadithi ile ni ya kweli. Na fahamuni kuwa hao wenye elimu ya hadithi na wabainishaji wamekosa, na ni waongo wale wenye kusema kuwa hadithi ile ni dhaifu. Na hadithi za namna hii ni mamia na mamia zenye bishara. Na hadithi nyingi za namna hii, wenye elimu ya hadithi wanasema kuwa ni dhaifu na zimeharibika, tena si sawa. Lakini ikitimia mojawapo katika hadithi hizi; na ninyi mkisema kuwa sisi hatukubali sababu hadithi hii ni dhaifu au mbainishaji wa hadithi hakuwa mtawa; jueni utakuwa ni upotevu wa nafsi zenu na kukufuru, endapo mkikataa hadithi ya namna hii Mwenyezi Mungu Aliyoidhihirisha ukweli wake.

Fikirini kama kuna hadithi elfu za namna hii, lakini wenye elimu ya hadithi wanasema kuwa ni dhaifu, halafu zikitimia bishara elfu zilizobainishwa katika hadithi hizo, je ninyi mtapoteza dalili hizi elfu nzima zihakikishazo ukweli wa Uislamu kwa sababu ya maneno yenu tu kuwa hadithi hii ni dhaifu? Basi ikiwa mtakataa, ninyi mtakuwa maadui wa Uislamu. Na Mwenyezi Mungu amesema: *Falaa yudh-hiru'alaa ghaibihiy ahadan illaa, manirtadhaa min rasuwlin* - Haonyeshi siri yake kwa yeyote ila kwa yule Aliyemchagua kuwa Mtume[46]. Minghairi ya Mtume wa kweli nani tena atakayeonyeshwa bishara ya kweli? Je, haitakuwa vizuri kwa kufuata mambo ya imani kusema hivi, kuwa mwenye elimu ya hadithi amekosa aliposema kuwa hadithi hizi ni dhaifu? Au mnafahamu kuwa ni vizuri kusema kuwa Mungu Amekosea kwa kuzisadikisha hadithi za uwongo?

Kwa hiyo nawausieni kuwa, fuateni hadithi hata kama ni dhaifu lakini kwa sharti ziwe sawa na Quran na zisiwe zenye kuhalifu hadithi zilizo sawa na Quran na *Sunna.*

Na tendeni kwa kufuatisha hadithi, lakini kwa kuangalia sana, kwani hadithi nyingi zimetengenezwa na watu, wala si za kweli, ambazo zimeleta fitina katika dini ya Kiislam. Kila taifa lina hadithi sawasawa na kuamini kwao. Hata sala ambayo ni faradhi ya yakini na ya mfululizo, hitilafu za hadithi zimeifanya faradhi hii katika namna nyingi na kwa sura mbalimbali. Wengine wanasema *Amin* kwa sauti kubwa na wengine kwa sauti ndogo. Wengine wanasoma sura ya Alhamdu nyuma ya imamu na wengine wanasema kusoma kwake kunaharibu sala. Na wengine wanafunga mikono yao juu ya vifua vyao na wengine wanafunga juu ya vitovu vyao, (Na wengine hawafungi mikono yao). Na asili ya sababu ya hitilafu hizi zote ni hitilafu ya hadith. *Kullu hizbin bimaa ladaihim farihuwna* - Kila

46 Sura 72 aya 27, 28

taifa linafurahia yale waliyo nayo.

Kwa kweli *Sunna* imeonyesha njia moja tu. Lakini kuchanganyika kwa hadithi hizi kumeitikisa njia hii. Na vivi hivi kutofahamu hadithi kumeangamiza watu wengi. Shia[47] pia wameangamia kwa sababu hii. Lau kama wangalifanya Quran kuwa hakimu baina yao, hata sura ya *Nuru* iliyomo katika Quran peke yake ingaliweza kuwatakasa. Lakini hadithi zimewaangamiza.

Hivi ndivyo wakati wa Nabii Isa wale Mayahudi wenye kufuata *Hadithi* walivyoangamia. Na waliacha Taurati na mpaka siku hizi wanaamini kuwa *hadithi* ni hakimu juu ya Taurati. Walikuwa na hadithi nyingi zenye kusema kuwa hawezi kuja Masihi Aliyeahidiwa mpaka ateremke *Ilyas* kutoka mbinguni kwa kiwiliwili chake. Hadithi hizi zimewatelezesha sana na wakaziinamia hata hawakuikubali hakika ya habari aliyoibainisha Masihi kuwa mradi katika kuja kwa *Ilyas* ni kuja kwa Yahya, aliyekuja kwa tabia za IIyas na kwa sifa zake na akawa wa mfano, Ilyas. Basi kuteleza kwao kulikuwa kwa sababu ya hadithi, na kwa sababu ya hadithi hizi mwishoni wakawa makafiri. Na vile vile inamkinika kuwa walikuwa wanakosa kutafsiri maana ya hadithi hizi au walichanganya maneno ya watu pamoja na hadithi hizi.

Labda Waislamu hawajui habari za matokeo haya kuwa Mayahudi waliomkataa Nabii Isa walikuwa watu wenye kufuata hadithi (Ahli-Hadithi), nao ndio waliompigia makelele

---

47 *Shia* ndio kundi moja katika makundi sabini na tatu ya Waislam, *Ithnaasharia, Bohora, Ismailia,* wote ni Shia ingawa wamehitilafiana kidogo kidogo tu. Imani yao ni mbali kabisa na mafundisho ya Islam. Mathalan: Wanaamini kuwa Seyidna Abubakar Siddik, Seyidna Umar, na Seyidna Athuman si Makhalifa wa haki wa Nabii Muhammad, amani ya Mungu juu yake, isipokuwa Seyidna Ali tu, na kwamba hawa watu watakatifu watatu walimnyang'anya Seyidna Ali haki yake ya Ukhalifa, hali hao wote, kama Waislamu wengine wanavyoyakini, walikuwa Makhalifa wa Nabii, amani ya Mungu juu yake, sawasawa, na ya kuwa Mungu Mwenyewe alisimamisha Ukhalifa wao (Mfasiri).

na kumwandikia tangazo kuwa yeye ni kafiri na walisema kuwa yeye haamini vitabu vya Mungu. Mwenyezi Mungu Ameeleza kuwa Nabii *Ilyas* atatumwa mara ya pili na huyu (Isa) ameeleza bishara hii kwa namna nyingine. Na anabadilisha maana yake kama anavyotaka bila kuwa na dalili za nguvu[48]. Tena Mayahudi hawakuona kuwa kumwita Nabii Isa kafiri kunatosha, bali vile vile walimwita *Mulhidi* - mshenzi hana dini, na walisema kama mtu huyu ni mkweli basi dini ya Musa ni batili. Wakati wao ulikuwa wakati wa uharibifu mkubwa, hadithi za uwongo ziliwadanganya.

Basi kwa neno zima inafaa kufikiri wakati wa kuisoma hadithi kuwa zamani walikuwapo watu waliofahamu kuwa hadithi ni hakimu juu ya Taurati wakaendelea hivi mpaka wakamkataa Nabii wa kweli, Isa, wakamwita kafiri na Dajjal (mwenye kudanganya).

Pamoja na haya *Sahihi Bukhari* ni kitabu chenye faida kubwa na baraka kwa Waislamu. Na hiki ndicho kitabu kilichoandikwa ndani yake kuwa Nabii Isa amekufa. Na vile vile katika *Sahihi Muslim na* vitabu vingine vya hadithi mna hazina ya mambo ya maarifa na mambo mengi ya dini. Na kutenda vitendo kwa kufuatisha hadithi hizi ni wajibu kwa sharti zisiwe zinahalifu Quran na *Sunna* na *Hadithi* zile zilizo sawa na Quran.

---

48 Walipoandika kuwa Yesu ni kafiri, wakati ule Paulo pia alikuwa katika watu wale waliomwita Yesu kafiri na baadaye alijitangaza kuwa yeye ni mjumbe wa Yesu! Mtu huyu Paulo alikuwa adui wa Yesu wakati wa uzima wake. Katika Injili zote zilizoandikwa mpaka sasa, haipatikani bishara isemayo kuwa Paulo atatubia na atakuwa Mtume. Hatuna haja kuandika juu ya hali yake ya kwanza, sababu Wakristo wanajua sana hali yake. Huyu ndiye aliyemwudhi sana Yesu alipokuwa katika mji wake. Na Yesu alipohamia Kashmiri baada ya kuokoka msalabani, Paulo alijiingiza katika wafuasi wa Yesu kwa ajili ya ndoto ya uwongo; na alianzisha imani ya utatu, na alihalalisha kwa Wakristo kula nguruwe ambayo ilikuwa imeharamishwa kabisa katika hukumu ya Taurati, na akatoa nafasi ya kunywa pombe na aliingiza imani ya utatu katika imani ya Injili ili wafurahike katika mambo haya mapya, Wagiriki waabuduo masanamu.

# SURA YA SABA

## Mawaidha juu ya Yakini, Sala, na Wokofu

**Baraka za Yakini.**

Enyi watu wamtakao Mwenyezi Mungu! Fungueni masikio na sikilizeni kuwa hapana kitu kama yakini. Yakini peke yake ndiyo yenye kumfungua mtu katika madhambi. Yakini ndiyo inayotoa uwezo wa kutenda mema. Na yakini ndiyo imfanyayo mtu ashiki na mpenzi hasa wa Mola Wake.

Je! Mnaweza kuacha dhambi bila ya yakini? Mnaweza kujikataza matamanio ya nafsi zenu bila nuru ya yakini? Au mnaweza kupata utulivu wa roho bila yakini? Au mnaweza kujibadilisha kweli kweli bila yakini? Je! Iko kafara au sadaka yoyote chini ya mbingu yenye kuweza kuwaondoleeni dhambi? Au je, damu isiyokuwa ya asili ya Isa mwana wa Mariamu, inaweza kuwaokoeni katika madhambi?

Enyi Wakristo! Msiseme uwongo ambao hupasua ardhi. Yesu Kristo mwenyewe alikuwa mhitaji wa yakini kwa kuokoka kwake, akayakini na akaokoka. Ole kwa hawa Wakristo wanaowadanganya watu kwa kauli yao kuwa wameishiwa madhambi kwa ajili ya damu ya Yesu Kristo na hali wao toka kichwani mpaka miguuni wamezama katika madhambi! Hata hawajui Mungu wao ni nani; bali maisha yao yamechanganyika na mghafiliko, na ulevi wa kinywaji unazunguka katika ubongo wao. Lakini *ladha* tukufu inayoteremka mbinguni hawana habari nayo. Na uzima utokao kwa Mungu na matokeo ya maisha mema wao wamenyimwa.

Basi kumbukeni kuwa hamwezi kuondoka katika maisha ya giza bila yakini, wala hamwezi kukutana na roho mtakatifu.

Naam, wamebarikiwa hao wenye yakini, kwani wao ndio watakaookoka katika madhambi. Mtabarikiwa mtakapopewa hazina ya yakini, kwani baadaye mtaishiwa madhambi. Dhambi na yakini havipatani. Jee! Mnaweza kuingiza mikono yenu katika tundu mnamoona nyoka mkali? Jee! Mnaweza kusimama pahali pale mlima wa volkano unapotupa mawe? Au pahali radi inapoangukia?Au pahali simba mkali anaposhambulia? Au pahali penye Tauni yenye kuangamiza ukoo wa watu wote? Basi mkiwa mna yakini kwa Mungu kama mlivyokuwa na yakini kwa nyoka au radi, au simba mkali au Tauni, haiwezekani kabisa kumwasi Mungu na kufuata njia ya adhabu, au kukataa kufungamana kwa ukweli na kutekeleza kwa Mungu!

Enyi watu mlioitwa kwenye wema na utawa, fahamuni kwa yakini yakuwa, ninyi mtavutwa na Mungu na mtatoharishwa katika doa la madhambi itakapojazwa yakini mioyoni mwenu. Labda mtasema ya kuwa tunayo yakini. Lakini jueni hakika ninyi mnadanganyika. Maana hamna yakini kabisa, sababu mambo yanayotakiwa kwa kupata yakini hayako kwenu, na kwa sababu ninyi hamjiepushi na makosa. Wala ninyi hamnyanyui miguu yenu kwenda mbele ambako inafaa kunyanyua. Wala ninyi hammwogopi yule anayefaa kuogopwa. Fikirini wenyewe, jee, inawezekana mtu kuingiza mkono wake katika shimo anamojua kuwa mna nyoka? Au mtu anaweza kula chakula anachojua kwa yakini kuwa mna sumu? Atakulaje na ataingizaje? Na mwenye kujua kwa yakini kuwa katika pori fulani mna simba elfu wakali atawezaje kunyanyua miguu yake kwenda katika pori hilo bila kuangalia? Basi inawezekanaje mikono yenu na miguu yenu na masikio yenu na macho yenu kufanya madhambi ikiwa mna yakini kwa Mwenyezi Mungu na siku ya malipo? Hasha! Dhambi haishindi yakini! Na kama mkiona moto wenye kuwaka itamkinikaje kujitupa katika moto huo? Hakika kuta za yakini zinafika mpaka mbinguni na haiwezekani Shetani kuzipanda.

Na kila anayetakasika ametakasika kwa yakini tu. Yakini inampa mtu nguvu za kustahamili mashambulio ya dhara. Hata yakini inamwondoa mfalme katika enzi na kumvalisha mavazi ya kimaskini. Yakini inafanya rahisi kuvumilia kila maumivu. Yakini inaonyesha Mungu. Kila *kafara* ni uwongo na kila fidiya ni batili. Na kila utakatifu unakuja katika njia ya yakini. Na kitu chenye kumwondoa mtu katika madhambi na kumfikisha kwa Mwenyezi Mungu na kumfanya mbora hata kuliko Malaika katika ukweli na uthabiti ni yakini. Kila dini isiyokuwa na mambo ila visa vya zamani tu ni dini ya uwongo. Mwenyezi Mungu kama Alivyokuwa zamani ndivyo Alivyo mpaka sasa. Na kama uwezo Wake ulivyokuwa zamani na sasa upo vile vile, na kama Alivyokuwa Anaweza kuonyesha ishara Zake na sasa vile vile Anaweza kuzionyesha. Basi tena kwa nini ninyi mnapenda kufuata visa tu? Imeangamia dini ile ambayo ishara zake na ubashiri wake ni visa tu, na wameangamia watu wale wasioteremkiwa na Mungu,wala hawakutakaswa na mikono ya Mungu kwa njia ya yakini. Kama vile mtu akiona vitu vya ladha za kimwili anavutiwa kwenye vitu hivyo, kadhalika mtu anapopata, kwa njia ya yakini, ladha ya kiroho, anavutwa kwa Mwenyezl Mungu. Na uzuri Wake unamlevya hata anaviona vitu vyote vya dunia kama takataka.

Na mtu huondolewa katika madhambi anapomjua kwa yakini Mwenyezi Mungu na uwezo Wake na malipo Yake. Hakika mzizi wa kila maasi ni ujinga. Mwenye kupata sehemu ya maarifa ya Mungu kwa yakini hawezi kuendelea kumwasi. Mwenye nyumba hawezi kukaa nyumbani mwake akijua kwamba tufani la maji linakuja kwenye welekeo wa nyumba yake; au moto umeizunguka nyumba yake na umeiunguza ila pamebakia pahali padogo tu. Basi huyu hawezi kungojea katika nyumba ile. Kwa nini ninyi mmekaa katika hali yenu yenye hatari baada ya kujidai kuwa mna yakini na malipo ya Mungu? Basi fumbueni macho yenu na tazameni hukumu za Mungu

zilizomo duniani. Na msiwe mapanya waendao chini ya ardhi; bali kuweni njiwa warukao juu na kupenda hewa ya mbinguni. Jihadharini msifanye madhambi baada ya kutubia wala msiwe kama nyoka mwenye kujichubua gamba lake na ni nyoka vile vile. Yakumbukeni mauti siku zote, kwani yanawasogeleeni pole pole, lakini ninyi mmeghafilika nayo. Jitahidini mtakasike, sababu mtu hawezi kumpata Mtakatifu (Mwenyezi Mungu) mpaka ajitakase mwenyewe.

Lakini mnawezaje kupata neema hii? Mwenyezi Mungu Alijibu Mwenyewe kama Anavyosema katika Quran tukufu: *Wastaiinu bisswabri was sswalaat* - yaani, Ombeni msaada kwa Mwenyezi Mungu kwa kusali na kusubiri[49].

Sala ni nini? Sala ni dua inayoombwa kwa Mungu kwa unyenyekevu na kwa tasbihi na kumhimidia na kumtukuza na kumwomba msamaha na kumsalia Mtume Mtakatifu. Kwa hivi ninyi mnaposali sala zenu, msiombe dua zenu kwa maneno ya Kiarabu tu kama watu wenye kughafilika; kwani sala zao na kutubia kwao hakuna maana. Lakini ninyi mnaposali si vibaya kuomba dua zenu kwa unyenyekevu katika lugha zenu isipokuwa Quran ambayo ni maneno ya Mungu na dua zilizobainishwa katika hadithi ambazo ni maneno ya Mtume, amani ya Mungu juu yake, ili alama yakuomba na unyenyekevu iwe katika mioyo yenu.

**Hekima ya kuweka Sala tano.**

Sala tano ni picha ya hali zenu mbalimbali. Maana hali ni tano zenye kufungamana na uzima wenu ziwafikiazo kwenu wakati wa taabu: na matokeo yao ni lazima kwa nafsi zenu.

(1) Hali ya kwanza inaanza mnapoonywa kuwa balaa litawapateni.

49 Sura 2 aya 46

Kama mkiletewa notisi ya mashtaka kutoka Serikalini, basi hiyo ni hali ya kwanza inayobadili furaha yenu, na utulivu wenu unapungua. Hali yenu hii inafanana na wakati wa kupinduka jua kidogo, sababu wakati ule wa kupata notisi furaha yenu inaanza kupinduka. Basi kwa sababu ya kuona hali hii imefaradhiwa sala ya *Adhuhuri* ambayo wakati wake unaanza wakati wa kuanza kupinduka jua.

(2) Na mabadiliko ya pili yanatokea mnaposogezwa karibu sana na pahali pa balaa. Kama mkikamatwa kwa kupatiwa notisi na kupelekwa mbele ya hakimu, huo ndio wakati damu yenu inapokauka kwa sababu ya hofu, na karibu kuiaga nuru yote ya utulivu. Hali yenu hii inafanana na wakati ule nuru ya jua inapopungua na mtu anaweza kulitazama; na inaonekana kuwa bado kidogo litakuchwa. Kwa hivi imefaradhishwa sala ya *Alasiri* kwa kufananisha na hali hii.

(3) Na mabadiliko ya tatu yanawafikieni pale mnapokata tamaa ya kuokoka katika balaa lile. Kama mkihukumiwa kuwa mmekosa, na mashahidi wote wakashuhudia makosa yenu ili mwangamie. Huu ndio wakati akili zenu zinapozunguka na mnafahamu kuwa ninyi mtafungwa. Basi hali yenu hii inafanana na wakati ule jua linapokuchwa na yanakwisha matumaini ya mwangaza wa mchana, kwa hivi imefaradhishwa sala ya *Maghrib* kwa kuifananisha na hali yenu hii.

(4) Na mabadiliko ya nne yanawapateni mnapopata balaa na kuzungukwa na giza la balaa. Kama baada ya ushahidi mnatangaziwa adhabu na kutolewa na askari ili mfungwe. Basi hali hii inafanana na wakati ule usiku unapoingia na kutia giza kabisa. Kwa hiyo imefaradhiswa sala ya *Ishaa* kwa kuifananisha na hali yenu hii.

*(5)* Tena mnapokaa muda katika giza la balaa hili, rehema ya Mungu inatokea na inawaokoeni katika balaa hili, kama Alfajiri inapotokea mara ya pili baada ya giza la usiku na mwangaza kuangaza mara pili. Kwa hivi imefaradhiswa sala ya *Asubuhi* kwa kuifananisha na hali yenu hii ya tano.

Mwenyezi Mungu Amewafaradhishieni sala zenu tano Alipoona hali zenu tano zinazofungamana na hali ya maisha yenu. Katika haya ninyi mnaweza kufahamu kuwa sala hizi hasa ni kwa sababu ya manufaa ya nafsi zenu. Na kama mnataka kusalimika na mabalaa haya, basi msiache sala katika nyakati zake hasa, kwani ni vivuli vya hali zenu za rohoni. Katika sala mna dawa ya kuponyesha ugonjwa wa mabalaa yafikayo. Ninyi hamjui kuwa mchana mpya utaleta kwenu hukumu gani. Basi kabla mchana haujafika, nyenyekeeni mbele ya Mola wenu ili kutokea kwa mchana kuwe kwa heri na baraka kwenu.

**Njia ya Wokofu.**

Enyi wafalme na matajiri na wenye mali!! Ni wachache sana katika ninyi wanaomwogopa Mwenyezi Mungu na washikao utawa katika njia zake zote. Wengi wenu wanapenda vitu vya dunia na ufalme wa dunia, na wanaishi ndani yake wala hawakumbuki mauti. Kila tajiri asiyesali wala hamjali Mwenyezi Mungu, dhambi za watumishi wake zimo shingoni mwake. Na kila tajiri anayekunywa pombe dhambi za wale wanaokunywa pamoja naye zimo shingoni mwake.

Sikilizeni enyi wenye akili, dunia hii si makazi ya siku zote; jihadharini na acheni kila ujeuri. Na acheni kila kitu kinacholevya. Siyo pombe tu peke yake inayomwangamiza mtu, bali pia afyuni, kasumba na bangi na kangara na mnanaa na kila kileweshacho huharibu akili na mwishoni huangamiza. Kwa hivi jiepusheni navyo. Sisi hatuwezi kufahamu kwanini

mnatumia vitu hivi ambavyo madhara yake yanaangamiza[50] maelfu ya walevi kama ninyi kila mwaka. Na juu ya hayo vile vile iko adhabu ya siku ya Kiyama.

Kuweni watu waongofu ili umri wenu uzidi na mpate baraka kwa Mungu. Sikilizeni, kuishi sana katika ladha ya dunia na katika mambo mabaya siku zote ni maisha yaliyolaaniwa. Na kuwa mwenye tabia mbaya sana na kuwa mtu asiye na huruma maisha yake yamelaaniwa. Na kuwa mtu asiyemjali Mungu na viumbe vyake maisha yake yamelaaniwa. Kila tajiri ataulizwa haki ya Mungu na haki ya viumbe vyake kama atakavyoulizwa mtu maskini. Bahati gani mbaya ya yule mwenye kutawakali juu ya uzima huu mchache wa dunia, wala hageuki kwa Mwenyezi Mungu kabisa, na kutumia Alivyoharamisha Mungu kwa ujasiri kama vilivyohalalishwa! Na wakati wa kukasirika[51] anakuwa kama mwenye wazimu, akili yake inamzunguka anamtukana

50 Kinywaji kiliwadhuru Wazungu, ilikuwa sababu yake kuwa Yesu alikuwa akinywa pombe labda kwa ugonjwa au kwa desturi ya zamani. Lakini enyi Waislamu! kwa nini mnakunywa pombe na hali Mtume wenu alikuwa mbali na kila Ulevi na alikuwa mtakatifu kabisa? Baada ya kuitwa Waislamu mnamfuata nani? Quran si kama Injili inayohalalisha pombe. Kwa dalili gani basi mnahalalisha pombe? Je hamtakufa?

51 Anayewakasirikia watu na kuwadhulumu kwa ghadhabu yake, yeye pia anaangamizwa na ghadhabu ya Mungu. Kwa hiyo Mayahudi wameitwa katika Suratul-Fatiha: *Maghdhuwbi ‘alaihim* - “Walioghadhibikiwa”, yanayohakikisha kwamba kila mwenye dhambi ataionja ghadhabu ya Mungu siku ya Kiyama; lakini hapa duniani mtu anayewadhulumu watu na anawakasirikia bila haki, bila shaka yeye ataionja adhabu ya Mungu hapa hapa duniani. Wakristo hawakuonyesha ghadhabu kama walivyoonyesha Mayahudi kwa hivi Wakristo waliitwa katika Suratul-Fatiha: *Addhaalliyna* -”Waliopotea”. Neno hili lina maana mbili.(l) Walioipotea njia ya haki’, na ‘Waliopotezwa na kutoweshwa’; na kwa maana hii ya pili inaonekana kwangu kuwa bishara kwa ajili ya Wakristo, yaani kuna wakati wataokoka katika imani ya uwongo na wataingia katika Uislamu. Na polepole wataacha imani ya ushirikina (yaani kumfanya Yesu Mungu) na mila yao ya ovyo na watakuwa katika hali ya Waislamu washikao umoja wa Mungu. Kwa kifupi, katika tamko la *Addhwaalliyn* lililoko mwisho wa sura ya Alhamdu, kwa kufuata maana ya pili ya neno *dhwalaalah,* yaani kitu kimoja kutoweka ndani ya kingine na kupotezwa au kutoweshwa, imo bishara kwa ajili ya hali ya kidini ya baadaye ya Wakristo.

huyu, anamjeruhi mwingine, na anajiweka tayari kumwua yeyote. Na katika machafuko ya matumaini mabaya ya nafsi yake anapita kiasi katika mambo ya aibu. Basi mtu huyu hawezi kupata bahati nzuri ya kweli na atakufa vivi hivi.

Enyi wapenzi! Mmekuja duniani kwa siku chache tu, na siku nyingi zimekwisha pita. msimkasirishe Mola wenu. Fikirini kama mkikasirikiwa na ufalme wa watu wenye nguvu zaidi kuliko ninyi, unaweza kuwaangamizeni ninyi nyote; basi fahamuni mnawezaje kusalimka katika ghadhabu ya Mwenyezi Mungu Aliye Mfalme wa walimwengu wote? Mkiwa waongofu machoni pa Mwenyezi Mungu, hawezi yeyote kuwaangamizeni. Na Mungu Mwenyewe Atawalindeni, wala yeyote anayewafuateni hataweza kuwakamateni. Na minghairi ya Mungu hapana atakayewalindeni, na ninyi katika hali ya kuogopa maadui na kupata balaa na taabu mtaishi mashakani. Na kwa hiyo mtamaliza umri wenu uliobaki kwa maumivu na makasiriko.

Mwenyezi Mungu Anawalinda wale walio pamoja Naye. Kwa hivi njooni wote kwa Mwenyezi Mungu na acheni kumwasi kwa kila namna. Wala msifanye uvivu katika kutekeleza faradhi zake. Wala msidhulumu viumbe vyake kwa ulimi au kwa mikono. Na ogopeni ghadhabu zake siku zote. Kwani hii ndiyo njia ya kuokoka.

# SURA YA NANE

## Msishike Mwendo wa Mayahudi.

Enyi waalimu wa Kiislamu! msifanye haraka kunikadhibisha, kwani siri ni nyingi ambazo mtu hawezi kuzifahamu upesi. Msiwe tayari kukataa maneno pale mnapoyasikia, sababu hii si njia ya uongofu. Lau kama msingalikuwa na baadhi ya makosa, na msingalikuwa wenye hatia katika kutafsiri baadhi ya hadithi za Mtume, amani ya Mungu juu Yake, ingekuwa ni bure kufika Masihi Aliyeahidiwa kuwa hakimu baina yenu katika mambo ya dini. Tazameni wale waliotangulia! Mayahudi walikazana kama mnavyokazana na waliweka miguu yao pahali mlipoweka ninyi miguu yenu. Yaani walikuwa wakimngojea *Ilyasa* atumwe mara ya pili; ambaye alichukuliwa mbinguni. Na pia walikuwa wakisema ni mwongo mwenye kujidai kuwa yeye ni Masihi kabla *Ilyasa* hajateremka. Wala hawakufahamu haya katika hadithi tu, bali vile vile walikuwa wakithibitisha jambo hili kwa kitabu cha Mungu kiitwacho *Malaki* katika Taurati. Lakini Yesu Kristo alipodai kuwa yeye ndiye Masihi Aliyeahidiwa kwa Mayahudi, *Ilyasa* pia hakuteremka, lililokuwa sharti kwa kudai kwake, basi imebatilika imani yote ya Mayahudi. Na mwishoni ilidhihirika maana ya jambo lile lililokuwa katika imani ya Mayahudi kuwa *Ilyasa* atateremka kutoka mbinguni kwa kiwiliwili chake kuwa atakuja mtu mwingine mwenye kufuatisha desturi za *Ilyasa* na atafanana kwa sifa zake na tabia zake. Na maana hii aliibainisha Nabii Isa mwenyewe, ambaye ninyi mnamtaka ateremke kutoka mbinguni mara ya pili.

Basi kwa nini ninyi mnateleza pale Mayahudi walipoteleza kabla yenu? Katika nchi yenu mna maelfu ya Mayahudi, waulizeni kuamini kwao; si kama vile ninyi mnavyoonyesha sasa? Basi kama Mwenyezi Mungu Hakumteremsha Nabii Ilyasa mara ya pili kwa ajili ya Nabii Isa, kwa hiyo Mungu Akaeleza maana yake kwa namna nyingine, Anawezaje kumteremsha Nabii Isa kwa ajili yenu, ambaye mnataka afike mara ya pili? Kweli

ninyi mnaikataa hukumu yake! Mkiwa na shaka katika haya tuliyoyasema, basi Wakristo wamo katika nchi yenu maelfu na maelfu, na Injili zao vile vile zipo, waulizeni si kweli kuwa Nabii Isa alisema juu ya *Yahya* kuwa huyu ndiye *Ilyasa* Aliyeahidiwa kuja mara nyingine? Na Yesu kwa kauli yake hii akayafanya matumaini yao kuwa upuuzi.

Basi kama ni lazima kwamba Nabii Isa ateremke kutoka mbinguni kwa kiwiliwili chake, yeye hatakuwa tena Nabii wa kweli; kwani lau kama kuteremka kutoka mbinguni na kurudia duniani kungalikuwa ni desturi ya Mungu, kwa nini hakurudishwa Nabii Ilyasa? Na kwa nini Nabii Isa alibainisha tafsiri ya namna nyingine na kusema kuwa Yahya ndiye Ilyasa? Na wafikiri hapa hao wenye akili.

Tena kuamini kwenu kuwa Nabii Isa atateremka kutoka mbinguni na yeye pamoja na Mahdi watapigana na watu kwa kuwasilimisha kwa nguvu, kuamini namna hii, bila shaka, kunaharibu jina la dini ya Kiislamu. Imeandikwa wapi katika Quran kuwa kuwaingiza watu kwa nguvu katika dini kunajuzu? Bali Mwenyezi Mungu Amesema katika Quran takatifu: *Laa ikraha fi-d-din* - yaani hapana karaha katika dini[52]. Basi Nabii lsa atapewa ruhusa au uwezo kuwaingiza watu katika dini kwa nguvu na karaha, hata asikubali jizya (kodi) ila kuua au kusilimu tu? Pahali gani katika Quran na katika juzu gani na katika sura gani yameandikwa mafundisho kama haya?[53]

(i) Quran yote inasema mara kwa mara kuwa hakuna nguvu

52 Sura 2 aya 257

53 Mkisema kuwa ilikuwapo hukumu ya kuwasilimisha Waarabu kwa nguvu na karaha, basi hukumu hii haipatikani katika Quran kabisa. Bali inapatikana katika Quran kuwa Waarabu walimwudhi sana Mtume, Amani ya Mungu juu yake, na waliwaua masahaba Wengi wanaume na wanawake; na waliwatoa masahaba wasiouawa kwa panga zao katika miji yao. Na waliofanya kosa hili, yaani kuua masahaba na kuwasaidia wale waliokuwa wakiwaua masahaba, walistahili kwa Mungu kuuawa. Na kwa hakika kwa sheria ya kisasi hukumu yao ni kuuawa.

na karaha katika dini na inaonyesha wazi wazi kuwa vita vilivyopiganwa wakati wa Mtume, amani ya Mungu juu yake, havikuwa kwa sababu ya kuzagaza dini kwa nguvu. Bali vilikuwa kama namna ya adhabu ya kuwaadhibu wale waliowaua Waislamu wengi na wengine kuwatoa katika nyumba zao, na kuwadhulumu dhuluma kubwa. Kama Anavyosema Mwenyezi Mungu: *Udhina lilladhiyna yukaataluwna bi annahum dhulimuw wainnallaha 'alaa Nasrihim lakadiyr* -Yaani Waislamu walipewa ruhusa kupigana na makafiri wanaowaua Waislamu na kwa sababu ya Waislamu waliodhulumiwa. Na Mungu anao uwezo wa kuwasaidia[54].

(ii) Au vilikuwa kwa sababu ya kujikinga na kujilinda. Yaani walipigana na wale waliokuwa wanaanza kupigana ili kuuangamiza Uislamu na kukataza kwa nguvu na karaha kuzagaza Uislamu.

(iii) Au walikuwa wanapigana kwa sababu ya kusimamisha uungwana katika nchi na uhuru wa dhamiri.

Bila ya sababu hizi tatu Mtume, amani ya Mungu juu yake, hakupigana kabisa wala Makhalifa wake hawakupigana kabisa. Bali Uislamu ulistahamili dhuluma ya mataifa mengine hata haupatikani mfano wake katika mataifa na dini nyingine kabisa. Basi watakuwa wa namna gani hawa Masihi na Mahdi kuja duniani na kuanza kuua mara moja hata wasikubali kodi ya yeyote katika watu wa kitabu (Wakristo na Mayahudi), na kutengua aya hii: *Hattaa yu'tul jizyata 'an-yyadin wahum saaghiruwna - Hata* watoe kodi kwa mkono na watakuwamo katika hali ya uraia[55].

Basi hao watakuwaje walinzi wa Uislamu, hali kwa kufika

54 Sura 22 aya 40
55 Sura 9 aya 29

kwao, watatengua aya za Quran hata watengue aya ambazo hazikutenguka wakati wa Mtume, amani ya Mungu juu yake? Na baada ya kutokea mabadiliko makubwa haya haiji hitilafu katita *Khatm-i-Nubuwwat!!!* Siku hizi, ilipopita miaka elfu moja na mia tatu toka zama za Mtume, amani ya Mungu juu yake, na Uislamu kugawanyika katika vikundi sabini na tatu; inafaa kwa Masihi wa kweli kufanya kazi ya kushinda mioyo kwa dalili si kwa upanga, tena avunje misalaba iliyotengenezwa kwa fedha na dhahabu na shaba na miti. Kama ninyi mkishurutisha basi kushurutisha kwenu kutakuwa dalili kuwa ninyi si wakweli[56]. Kila mjinga na dhalimu, kama hana dalili na akishindwa, huchukua upanga au bunduki. Lakini dini inayoenezwa tu kwa nguvu za upanga, si kwa njia nyingine, haiwezi kuwa dini ya Mungu kabisa. Na kama ninyi hamwezi kujiepusha na

56 Baadhi ya watu wasio na elimu wanabisha kama alivyobisha mtengenezaji wa gazeti liitwalo *Alminar,* kuwa mtu huyu anakaa katika nchi amabayo imo katika ufalme wa Waingereza, kwa hivi anakataza jihadi (kupigana). Lakini hawa wajinga hawajui lau kama nataka kuufurahisha ufalme huu kwa uwongo, kwa nini nimesema mara nyingi kuwa Isa mwana wa Mariamu aliokoka katika msalaba na alikufa kifo cha kawaida katika mji wa Srinagar, Kashmir; wala hakuwa Mungu wala hakuwa mwana wa Mungu. Je, Wazungu wenye kuipenda sana dini yao hawatanichukia kwa ajili ya kauli yangu hii? Basi sikilizeni enyi wajinga! Mimi si mfurahishaji wa udanganyifu wa ufalme wa Waingereza. Bali jambo ni hili ya kuwa ufalme usioingia katika mambo ya dini ya Kiislam wala haukatazi kuzagazaUislamu, wala hautumii panga ili kuzidisha dini yake, wala hautuonyi, basi kupigana na ufalme kama huu imekatazwa katika Quran. Sababu dola pia haipigani kwa ajili ya dini. Na kuushukuru ufalme huu ni lazima kwetu, kwani hatuwezi kutekeleza kazi zetu hata Makka au Madina. Ilikuwa ni hekima ya Mungu kuniumba katika mamlaka yao. Jee, nipunguze heshima ya hekima ya Mungu kwa kuacha kuushukuru ufalme huu? Na kama Anavyosema Mungu katika Quran: *Wa aawainaa humaa ilaa rab watin dhaati karaarin wama'iyn* - Tulipokwisha mwokoa Yesu katika msalaba tulimpa pahali juu ya mlima mrefu pamoja na mama yake. Na pahali pale palikuwa na raha na chemchem zilikuwa zinapita: yaani katika mji wa Srinagar. Vivi hivi Mwenyezi Mungu Amenipa pahali juu ya mlima wa ufalme huu, pahali ambapo mikono ya wafisadi haifiki, na ambapo ni pahali pa raha na katika nchi hii chemehem za elimu za kweli zinatiririka na mashambulio ya maadui hayapo. Basi je, si faradhi juu yetu kushukuru hisani ya ufalme huu?

kupigana kwa namna hii, na kwa ghadhabu yenu mnawaita watawa kuwa makafiri na Dajjali, wenye kuficha ukweli, basi mimi namaliza hotuba yangu kwa maneno mawili: *Kul ya ayyuhal kafiruwnlaa a'budu ma ta'buduwna - Enyi* makafiri! Siabudu mnachokiabudu![57]

Fikirini! Wakati wa hitilafu baina ya Waislamu, ni taifa gani Masihi wenu atakalofutia upanga wake? Jee! Shia (Ithnasharia) hawastahili kupigwa panga na Sunni? Na je, Sunni wao hawastahili kufutwa kwa panga? Ikiwa hali yenu ya nyumbani ni namna hii, yaani mataifa ya Waislamu kwa kuamini kwao wanastahili kuadhibiwa na kufutwa na wengine, basi nani na nani mtakaopigana nao? Lakini jueni kuwa Mwenyezi Mungu hahitaji panga, yeye atazagaza dini Yake kwa ishara za mbinguni, wala hapana yeyote awezaye kumkataza.

Na fahamuni kuwa hatateremka Nabii Isa kabisa. Maana atakiri kwa kauli yake siku ya Kiyama: *Falamma tawaffaitaniy- 'Uliponifisha',* ambayo kauli hii yaonyesha wazi kuwa yeye hatakuja mara ya pili duniani. Na hoja yake siku ya Kiyama itakuwa kwamba hana habari juu ya upotevu wa Wakristo. Na kama yeye atakuja duniani kabla ya siku ya Kiyama, itamkinikaje kwake kujibu kuwa hana habari ya upotevu wa Wakristo? Kwa hivi aya hii inaonyesha kwa wazi wazi kuwa haji duniani mara ya pili. Lau kama yeye atakuja na atakaa duniani miaka arobaini, basi kauli yake mbele ya Mungu kuwa hana habari yoyote ya upotevu wa Wakristo, itakuwa ya uwongo! Bali ilitakiwa aseme kuwa nilipokwenda duniani mara ya pili niliwakuta Wakristo 400,000,000, niliwaona wote, na ninajua sana upotevu wao, na ninastahili kupata zawadi, kwani nimewasilimisha Wakristo wote na nimevunja misalaba yao. Basi uwongo ulioje huu ya kwamba Nabii lsa atasema 'Sina habari ya upotevu wao!'

Kwa neno zima, katika aya hii kumo kukiri kwa Nabii Isa kwa

---

57 Sura 109 aya 2, 3.

wazi wazi kuwa, haji duniani mara ya pili. Na haya ndiyo ya kweli kuwa Nabii Isa amekufa. Na kaburi lake liko katika mtaa uitwao Khanyar[58], mjini Srinagar, Kashmiri. Sikilizeni! Sasa Mwenyezi Mungu Atateremka Mwenyewe na Atapigana na wale wanaopigana na ukweli. Kupigana kwa Mungu si aibu, kwani kupigana kwake ni kwa namna ya ishara. Lakini kupigana kwa mtu kuna aibu, kwani kuko katika namna ya ujabari.

Nawasikitikia Masheikh hawa, lau kama wangalikuwa waaminifu wangetafuta utulivu wao kwa njia ya uongofu. Na hakika Mwenyezi Mungu Aliwapa wenye roho safi utulivu. Lakini hao walioumbwa kwa udongo wa *Abujahal* wanapita njia aliyoipita *Abujahal*. Sheikh mmoja alinipasha habari kwa barua ya "register" kutoka mji wa *Merath* ya kwamba utakuwapo mkutano wa *Nadwatul-Ulama* katika mji wa *Amritsar* na inafaa niende huko kushindana nao. Lakini jueni kwamba, lau kama Masheikh hawa wangalikuwa na nia safi wala wasingalikuwa

58 1. Ushuhuda wa mmoja wa wanazuoni wa Kiisraeli.

Mmojawapo katika Mayahudi vile vile alisadiki kuwa kaburi hili lililoko Srinagar lilijengwa kama makaburi ya Manabii wa Kiyahudi. Tazameni ushuhuda wake ufuatao:

"Mimi nashuhudia kuwa nimeona picha moja kwa Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian. Nina hakika kuwa kaburi hili ni kaburi la mmoja wa Waisraeli. Na tena ni kaburi la mtu mkubwa katika Waisraeli. Na nimeona picha hii leo na nimeandika ushuhuda huu katika mwezi Juni tarehe 12 mwaka 1899".

Sahihi: SULEMAN YUSUF YAS'HAK,
Mfanyaji biashara.

"Suleman Yusuf Yas'hak mfanyaji biashara ameandika ushuhuda huu mbele yangu".

Sahihi: MUFTI MUHAMMAD SADIK,
Mwenyeji wa Bhera.

"Nashuhudia kwa Mungu kuwa maandishi haya ameyaandika Suleman bin Yusuf naye ni mtu miongoni mwa wakubwa wa wana wa Israeli".
Sahihi: SHARIF ABDULLA BAGHDADIY.

na fikara ya kushinda na kushindwa, wasingekuwa na haja ya kukusanyika huku kwa ajili ya kupata utulivu. Sisi hatuoni tofauti baina ya Masheikh wa *Nadwa* na masheikh wa *Amritsar.* Wote wana itikadi moja, jinsi moja na umbo moja. Kila mmoja wao ana hiari kuja Qadian, si kwa ugomvi na ubishi, bali kwa kutaka ukweli na kutafuta haki na kusikia usemi wetu na maneno yetu kwanza. Na kama akiwa bado na shaka, basi aombe kuondolewa shaka kwa adabu na unyenyekevu na atakuwa kwetu kama mgeni muheshimiwa kwa muda wowote atakaokaa Qadian. Hatuna haja na Masheikh wa *Nadwa,* kwani wote ni maadui wa ukweli, ingawa ukweli unazagaa.

Je, hii si ishara katika ishara kubwa za Mungu, kwamba Aliniambia, sasa miaka ishirini imepita, kwa ufunuo wake ambao umeandikwa katika B*arahine-Ahmadiyya,*kuwa *watu watajitahidi jitihada kubwa ili ushindwe, wala usipate kufuzu lakini mwisho wake Mimi Nitawafanyeni jamaat kubwa.* Nilifunuliwa ufunuo huu pale nilipokuwa sina hata mtu mmoja pamoja nami. Na nilipotangaza madai yangu, maadui zangu walijitahidi sana; lakini pamoja na hayo yote, Alivyosema Mungu mwendeleo huu umezagaa, na mpaka tarehe ya leo, Jamaat hii ina watu zaidi ya elfu mia[59] katika India ya Waingereza tu. Na kama Masheikh wa *Nadwa* wakiyakumbuka mauti yao, basi watazame kitabu changu *Barahine-Ahmadiyya* na karatasi za Serikali na baadaye watuambie kama hii ni Ishara ya Mungu au siyo? Na kama imethibitishwa katika Quran na katika Ishara, basi tena sasa mashindano ni ya nini?

Vile vile katika nchi hii Masheikh wa Twarika na watoto wa masharifu wameepukana na dini na wanashughulika katika bidaa zao usiku na mchana hata hawana habari na taabu za

59 Lakini sasa kwa rehema za Mungu hesabu ya Jamaa Ahmadiyya imekuwa karibu laki kumi na tano tena hawa Waahmadiyya wanapatikana katika kila bara la dunia. (Mfasiri).

Uislamu. Ukienda katika mkutano wao utaona, badala ya Quran na vitabu vya hadithi, mazeze na vinanda na vigoma na masiti na vitu vingine vya namna hii. Na juu ya haya wanajidai kuwa ni viongozi wa Waislamu na kujidai kuwa ni wafuasi wa Mtume Mtakatifu. Na baadhi yao wanavaa mavazi ya wanawake na wanapaka hina mikononi, na wanavaa bangili na makoja. Na wanapenda na kusoma mashairi katika mikutano yao badala ya Quran Takatifu. Hii yote ni kutu ya zamani haidhaniwi kuwa itaondoka. Lakini pamoja na haya Mwenyezi Mungu Atatuonyesha uwezo wake na Atakuwa MIinzi wa Uislamu!

# SURA YA TISA

## Maagizo mema Machache kwa Wanawake.

Katika zama zetu, wanawake pia wanaingia na kushughulika katika mambo yaliyo kinyume cha sheria. Wanafahamu kuwa ni vibaya waume zao kuoa wake wengi kana kwamba hawayaamini mafundisho ya Quran. Hawajui ya kuwa katika sheria ya Mwenyezi Mungu imo dawa ya kila namna. Hivyo kama kungekuwa hakuna suala la ndoa za mitala ndani ya Islam, basi kusingekuwa na tiba yoyote ndani ya sheria hii ya hali zile zinazojitokeza kwa mwanaume kuoa mke wa pili. Mathalani mke akipata wazimu, au akipata ukoma, au akipata ugonjwa wenye kumfanya kuchakaa, au hali nyingine inayompata mwanamke hata awe mwenye kustahili kuhurumiwa. Na pia mwanamume naye awe astahiliye kurehemiwa, kwani hawezi kustahamili kukaa pasipo mke. Basi katika hali hii itakuwa dhuluma juu ya mwanamume kama hakupewa nafasi ya kuoa mke mwingine. Kwa hakika sheria ya Mungu ilipoona hali ya namna hii ikawafungulia wanaume njia. Na wakati wa haja wanawake pia wakafunguliwa njia. Yaani mwanamume anapokuwa hafai ni haki kwa wanawake kuomba *khulaa* (talaka)kwa mkono wa hakimu. Na kuomba *khulaa,* kwa mkono wa hakimu ni sawasawa na talaka.

Sheria ya Mungu imefanana na duka la mwuza dawa. Kama katika duka la dawa haipatikani dawa ya kila ugonjwa duka haliwezi kuendelea vizuri. Basi fikirini je si haki kuwa baadhi ya taabu inawapata wanaume na kwa sababu ya, taabu hiyo wanakuwa na haja ya kuoa mke mwingine? Tena faida gani ya sheria isiyokuwa na dawa ya kuondoa kila ugonjwa na kila taabu? Tazameni katika Injili, imeandikwa ya kuwa kutoa talaka

ni kwa sababu ya zinaa tu[60], wala hazikutajwa sababu nyingi zingine ziletazo ugomvi na udhia baina ya mke na mume. Kwa hivi Wakristo hawakuvumilia upungufu wa sheria yao na kwa hiyo katika nchi ya Amerika wakaongeza sheria nyingine wenyewe katika jambo la talaka. Basi sasa kwa sheria hii Injili imetenguka kwa kutenguliwa na Wakristo wenyewe.

Enyi wanawake! Msihuzunike: kwani kitabu kilichotolewa kwenu hakihitaji kubadilishwa na watu. Maana kama haki za wanaume zilihifadhiwa kitabuni, vile vile haki zenu zimehifadhiwa katika kitabu kile kile. Na kama mwanamke haridhii mume wake aoe mke wa pili, basi anaweza kuomba *khulaa* (talaka) kwa mkono wa hakimu. Ilikuwa ni wajibu kwa Mwenyezi Mungu Kutaja katika sheria yake hali zote zinazoweza kuwafikia Waislamu, ili isiwe sheria isiyokamilika, bali iwe sheria kamilifu. Enyi wanawake, msimshtaki Mungu endapo waume zenu wamefunga nia ya kuoa mke wa pili. Bali ombeni ili Mungu Awahifadhini katika msiba na balaa hili. Kweli, ni mdhalimu mkubwa mume yule anayeoa wake wawili naye hafanyi uadilifu baina yao. Lakini ninyi msiwe wenye kukasirikiwa na Mungu, kwa sababu ya kumwasi kwenu. Kila mtu ataulizwa vitendo vyake. Kama ninyi mtakuwa wema mbele ya Mungu, mume wenu atafanywa mwema.

Ingawa sheria imeruhusu kuoa wake wengi kwa sababu ya mahitaji mbalimbali, lakini juu ya hayo, mmefunguliwa kanuni ya kadri ya Mungu. Na kama ninyi hamwezi kubeba kanuni ya sheria, basi jipatieni faida kwa dua katika kanuni ya kudra ya Mungu. Sababu kanuni ya kudra inaishinda kanuni ya sheria. Jihadharini na taweni! Msipende sana dunia na mapambo yake wala msijisifu kwa sababu ya kabila zenu. Wala msimfanyie dharau mwanamke yeyote. Wala msiombe kwa waume zenu

---

60 Mathayo 5:32

maombi wasiyoweza kuyapata. Jitahidini mwingie kaburini na hali mmetakasika na mmetukuka. Msifanye uvivu katika kutekeleza faradhi za Mungu kama Sala na Zaka na nyinginezo. Na tiini waume wenu kwa mapenzi ya roho zenu. Sehemu kubwa ya heshima yao imo mikononi mwenu, basi tekelezeni kazi yenu hii kwa njia nzuri ili mhesabiwe na Mungu katika wanawake wema, wanyenyekevu. Msitumie mali kwa fujo wala msitoe mali za waumfe wenu ovyo, wala msifanye hiana, wala msiibe, wala msisengenyane wala msimsingizie ye yote.

# SURA YA KUMI

## Nasaha ya Mwisho.

Nasaha hii yote tuliyoiandika katika kurasa zilizopita ni kwa ajili ya wanajumuiya wetu ili wazidi kumcha Mwenyezi Mungu, na wawe wenye kustahili kuepuka ghadhabu ya Mungu inayowaka duniani, na walindwe hasa katika siku hizi za Tauni.

Utawa hasa ndio unaomridhisha Mwenyezi Mungu, lakini ah, unapatikana kidogo tu. Na Mwenyezi Mungu Anawalinda katika mabalaa kwa uwezo Wake hasa, wale wenye kumcha kweli kweli. Kila mwenye vitimbi au mpumbavu anajidai ya kuwa yeye anamcha Mungu, lakini mcha Mungu ni yule ambaye kumcha kwake kumethibitika kwa ishara ya Mungu: Kila mtu anaweza kusema ya kuwa mimi nampenda Mungu; lakini ampendaye Mungu ni yule ambaye mapenzi yake yamethibitishwa na ushuhuda wa mbinguni. Na kila mtu anaweza kusema, dini yangu ni dini ya kweli; lakini dini ya kweli ni dini ya yule anayepewa nuru duniani. Na kila mtu anasema ya kuwa nitaokoka, lakini katika kauli hii mkweli ni yule anayeiona nuru ya kuokoka hapa hapa ulimwenguni. Basi jitahidini muwe wapenzi wa Mungu nanyi mtahifadhiwa katika kila msiba.

Mchaji wa kweli atahifadhiwa katika ugonjwa wa Tauni bila shaka, kwani yeye yu katika himaya ya Mungu. Basi mcheni Mungu kweli kweli. Mmekwisha sikia yale Aliyonifunulia Mungu juu ya Tauni. Tauni ni moto wa ghadhabu (ya Mungu) basi lindeni nafsi zenu katika moto huu. Mtu ye yote anayenifuata kweli kweli wala moyoni mwake hana uharibifu au uvivu au uzembe, waIa hachanganyi wema na ubaya, basi huyu

atalindwa bila shaka. Lakini anayeonyesha uvivu kuifuata njia hii wala asiyefuata sawasawa njia za uongofu kama inavyofaa, ameangukia kwenye dunia, basi yeye mwenyewe anaitupa nafsi yake katika mtihani. Mtiini Mungu kwa kila namna.

Na kila anayejifahamu kama yeye ni miongoni mwa wafuasi wangu, sasa inafaa aitumikie silsila hii hata kwa mali yake pia. Na anayeweza kutoa hata pesa moja basi na atoe kila mwezi kwa ajili ya mahitajio ya mwendeleo huu, Na mwenye kuweza kutoa rupia moja basi na atoe kila mwezi. Kwani minghairi ya gharama ya kuwakaribisha wageni, mahitajio mengine ya dini pia ni mengi sana yenye kuhitaji fedha. Mamia ya wageni wanakuja, lakini hawana pahali pa utulivu kwa sababu ya kukosa nafasi na kwa sababu ya kukosa vifaa. Na tena kuna mahitajio ya kupanua msikiti vile vile. Na vile vile kazi ya kuchapisha vitabu na kuvieneza bado ni kazi ndogo kuliko wafanyavyo wahalifu. Yanazagazwa na Wakristo magazeti ya dini yao elfu hamsini lakini sasa hayazagazwi kutoka kwetu hata elfu moja mwezi hata mwezi. Hizi ndizo haja ambazo kwa ajili yake inafaa kwa kila mfuasi atoe msaada kama anavyoweza ili Mwenyezi Mungu Amsaidie yeye pia. Lau kama msaada wao ukitufikia kila mwezi kwa mfululizo hata kama kidogo, hii ni bora kuliko msaada unaotolewa baada ya kusahau kwa muda mrefu. Kila mtu uongofu wake unajulikana kwa kutumika kwake. Enyi wapenzi! huu ni wakati wa kutumikia dini na mahitajio yake. Jikamatieni wakati huu kwa shukrani na isaidieni dini ya Mungu kwani wakati huu hautakuja mikononi tena. Inafaa kwa yule ambaye ni faradhi juu yake kutoa Zaka alete mali ya Zaka yake hapa. Na kila mtu ajiepushe kutoa mali yake ovyo, bali atoe mali yake katika njia hii ya dini na aonyeshe uongofu wake kwa kila namna ili apate zawadi ya fadhili na roho takatifu, kwani zawadi hii imewekwa tayari kwa hao wanaoingia katika mwendeleo huu wa Ahmadiyya.

Roho Mtakatifu kuonekana kwake kwa Mtume wetu, amani ya Mungu juu yake, kulikuwa mkubwa kuliko kuonekana kote. Roho Mtakatifu alionekana kwa Nabii fulani kwa sura ya njiwa, na alionekana kwa Nabii mwingine kwa sura ya ng'ombe na nyakati zingine alionekana kwa baadhi ya Manabii kwa sura ya samaki na mamba. Wala hakuonekana kwa sura ya mwanadamu mpaka alipotumwa mtu kamili yaani Mtume wetu, Amani ya Mungu juu yake. Alipotumwa Mtume mtakatifu, Roho mtakatifu vilevile alionekana kwa sura ya mtu. Na maonyesho yake yalikuwa yenye nguvu sana, yaliyoijaza ardhi mpaka mbinguni, kwa hivi mafundisho ya Quran yanahifadhiwa dhidi ya uharibifu wa ushirikina. Na kwa sababu alikuwa anaonekana kwa Yesu Kristo katika sura dhaifu, yaani sura ya njiwa, ndiyo maana kwa hivi roho mbaya, yaani shetani, ameishinda dini hii, na akaonyesha nguvu zake na ukubwa wake kwa sura ya kutisha mpaka akaishambulia kama joka.

Kwa sababu hii Quran imefahamu upotevu wa Wakristo kuwa ni upotevu mkubwa kushinda upotevu wa dunia yote. Na inasema kuwa karibu mbingu kupasuka na ardhi kuchanika na milima kuanguka kwa sababu ya dhambi yao kubwa: Kumfanya mtu kuwa Mungu na mwana wa Mungu. Na mwanzo wa Quran imetajwa hali ya Wakristo na imebatilishwa imani yao kama inavyoonekana katika aya: *Iyyaka na'budu* –Tunakuabudu wewe tu; na *Addhwaaliyna* - wala katika wale waliopotea[61]. Na mwisho wa Quran vile vile kuna mabatilisho ya Wakristo, kama inavyoonekana katika sura: *Kul huwa llahu ahad Allahu samad lam yalid walam yuwlad walam yakun lahu kufuwan ahad* - Sema Yeye Mungu ni Mmoja, Mungu Anayeendewa. Hakuzaa wala hakuzaliwa, wala hapana aliye sawa Naye hata mmoja[62]. Na katikati ya Quran vile vile imebainishwa fitina ya dini ya

61 Sura 1 aya 4 - 7
62 Sura 112 aya 1 - 5

Wakristo kama inavyojulikana katika aya hii: *Takadusamaawatu yatafattarna minhu*[63] - Karibu mbingu kupasuka. Na ni dhahiri katika Quran kuwa toka mwanzo wa dunia mpaka sasa haikufundishwa kuabudu viumbe na njia za upotovu kama Wakristo wanavyofuata na wanavyofundisha. Kwa sababu hii Wakristo peke yao wameitwa kwenye Mubahala (kuomba kwa Mungu ateremshe laana juu ya waongo), si washirikina wengine.

Lakini kuonekana Roho Mtakatifu katika sura ya ndege na mnyama kabla ya kutumwa Mtume Muhammad, amani ya Mungu juu yake, imo siri gani ndani yake? Atafahamu mwenye akili, lakini hapa tunaeleza kwa uchache. Ilikuwamo ishara katika jambo hili kuwa utu wa Mtume Mtakatifu ulikuwa na cheo kikubwa hata uliivuta roho takatifu kuwa mtu. Basi kwa nini ninyi mnashindwa baada ya kumfuata Mtume kama huyu mtukufu? Onyesheni mfano wa wema wenu hata malaika mbinguni washangae kwa kuona uongofu wenu na utukufu wa roho zenu, na wawasalieni. Kubalini kufa ili mpewe uzima, na ondoeni matumaini mabaya katika roho zenu ili Mwenyezi Mungu Aingie katika roho zenu. Kateni upande mmoja kabisa na fungamaneni upande mwingine kabisa ili Mwenyezi Mungu Awasaidieni.

Na sasa namaliza maneno yangu haya; na ninamuomba Mwenyezi Mungu kwamba mafundisho yangu haya yalete mabadiliko katika roho zenu mpaka muwe nyota za ardhini na ardhi ing'ae kwa nuru ile mtakayopewa na Bwana wenu Mwenyezi Mungu. Amin, tena Amin.

Enyi watumishi wa Mungu mimi nawakumbusheni siku za Mungu na ninawakumbusheni kumcha kwa dhati ya mioyo.

63 Sura 19 aya 91

Hakika kila mwenye kuja mbele ya Mungu, mwenye dhambi, atapata moto ambao hafi ndani yake wala haishi. Wala msiangukie kwenye mapambo ya dunia na uwongo wake. Mcheni Mungu na ombeni msaada kwa kusubiri na kusali.

Hakika Mwenyezi Mungu na Malaika wake wanamsalia Mtume; kwa hiyo, enyi mlioamini, ninyi pia mumsalie na mumsalimie.

*Allahumma swalli'ala Muhammadin wa 'ala ali Muhammadin wabaarik wasallim* (Ee Mola wetu Uteremshe rehema zako juu ya Mtume Muhammad na juu ya wafuasi wa Muhammad na Umbarikie na Umsalimie).

## KIUKENI KUTA HIZI, MWINGIE MWANGU NYUMBANI

Ishara kuzionyesha, bin Adamu hawezi,
Bali mimi naonyesha, kwa nguvu za Mwenye Enzi,
Mola kanithibitisha, kwa jambo hili azizi,
Kiukeni kuta hizi, mwingie mwangu nyumbani.

Bahati yake ni nzuri, yule aliyemaizi,
Akajiweka tayari, kuondoa usingizi,
Aje kwangu jisetiri, saa za simanzi hizi,
Kiukeni kuta hizi, mwingie mwangu nyumbani.

Naapa kwa jina lake, Mola asiye ajizi
Kuwa ni amri yake, mimi nifanye ulinzi
Ubashiri nipeleke, ufunuo huu wazi
Kiukeni kuta hizi, mwingie mwangu nyumbani

Enyi waja wa Manani, jamaa zangu wapenzi
Ishara ikibaini, ushinde haupendezi
Sasa asonibaini, rohoye ina masizi
Kiukeni kuta hizi, mwingie mwangu nyumbani

Miadi ninayotia, enyi watu wachunguzi
Subirini kutimia, mfanye upelelezi
Kama haikutimia,  mnifanye mpuuzi
Kiukeni kuta hizi, mwingie mwangu nyumbani

**MIRZA GHULAM AHMAD,  QADIAN.**

---- Mwisho ----

بســـــم الله الـر َّحـمـن الـر َّحــيـــــم

## MASHARTI YA KUINGIA KATIKA JUMUIYA YA WAISLAMU WAAHMADIYYA

**Yaliandikwa na Sayyidna Ahmad, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu.**

1. Mwenye kutaka kuingia katika Umoja huu uitwao Ahmadiyya ni juu yake kufanya ahadi kwa moyo wote ya kuwa hatamshirikisha Mwenyezi Mungu na chochote mpaka aingie kaburini.

2. Atajitahidi sana kujiepusha kabisa na kusema uwongo, wala hatatazama wanawake wala kufanya ufisadi, ufidhuli, hiyana na uasi, hatavikaribia vitendo vya namna hii, wala hatashindwa na tamaa mbaya za nafsi yake.

3. Atatekeleza Sala tano kwa nyakati zake hasa zilizowekwa kwa amri ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake *s.a.w.* na zaidi ya hayo atajitahidi sawa na uwezo wake kusali sala ya Tahajjud na atamsalia Mtukufu Mtume Muhammad *s.a.w.,* na daima ataomba msamaha wa dhambi zake kwa Mwenyezi Mungu, na kwa shauku ya moyo wake ataikumbuka hisani ya Mwenyezi Mungu, na atamhimidi sana siku zote.

4. Tena hatawadhuru hususa Waislamu na kwa ujumla viumbe wote wa Mwenyezi Mungu kwa sababu ya tamaa mbaya ya nafsi yake, si kwa mkono wake wala kwa ulimi na viungo vyake vingine.

5. Atakuwa radhi juu ya kudra ya Mwenyezi Mungu katika kila hali ya taabu na raha, dhiki na faraja, msiba na neema. Kwa neno zima atakuwa tayari kukubali fedheha na maumivu katika njia ya Mwenyezi Mungu, naye atakapopata msiba wowote hatageuka bali ataendelea mbele kufuata amri yake Mungu.

6. Ataacha kabisa kufuata desturi mbaya ya kutii tamaa ya nafsi yake na kutii mila za watu; bali atakubali amri ya Mwenyezi Mungu na kauli ya Mtume Muhammad *s.a.w.* katika mwenendo wake siku zote.

7. Ataacha kufanya kiburi na majivuno na ataishi kwa tabia njema na huruma na atakaa kwa unyenyekevu, kwa adabu na upole sana.

8. Atafahamu dini na heshima yake na kazi ya Uislamu kuwa ni bora kuliko mali yake na heshima ya nafsi yake na kuliko watoto wake na wapenzi wake wote.

9. Atawahurumia daima viumbe wa Mwenyezi Mungu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu, sawa na uwezo wake; naye atawaneemesha kwa zile neema alizopewa yeye na Mungu.

10. Katika ahadi ya udugu, atakayofungamana nami (Masihi niliyeahidiwa) kwa sharti ya kutii kila amri njema, atatimiza ahadi hii mpaka kufa kwake na katika ahadi hii ya udugu ataonesha utii na unyenyekevu wake kwa imara zaidi kuliko ufungamano wowote, wa damu au wa bwana na mtumishi.

(Tafsiri)

***(“Ishtehar Takmil-e-Tabligh” 12 Januari 89).***

## AHADI YA BAI'AT

أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلٰهَ إِلَّا اللّٰهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيْكَ لَهُ وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُوْلُهُ

أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلٰهَ إِلَّا اللّٰهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيْكَ لَهُ وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُوْلُهُ

Nashuhudia ya kuwa hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu. Yu Mmoja Asiye na mshirika. Na ninashuhudia ya kuwa Muhammad *s.a.w*. ni mtumishi Wake na Mtume wake.

Mimi leo najiunga na Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya kwa mkono wa MASROOR. Nina imani kamili na thabiti kwamba Mtume Muhammad *s.a.w.* ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na ni *Khaatamun Nabiyyiina.*

Mimi nakiri kuwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian ndiye yule yule Imam Mahdi na Masihi Aliyeahidiwa ambaye bishara ya kuja kwake ilitolewa na Mtume Muhammad *s.a.w.*

Mimi naahidi kwamba nitajitahidi kutekeleza masharti kumi ya Bai'at yaliyowekwa na Masihi Aliyeahidiwa *a.s.* Nitatanguliza dini juu ya dunia. Daima nitadumisha uaminifu wangu kwa Khalifa wa Kiahmadiyya na nitajitahidi kutekeleza maamrisho yake yote mema, kwa sababu ya kuwa kwake Khalifa wa Masihi.

أَسْتَغْفِرُ اللّٰهَ رَبِّيْ مِنْ كُلِّ ذَنْبٍ وَّأَتُوْبُ إِلَيْهِ أَسْتَغْفِرُ اللّٰهَ رَبِّيْ مِنْ كُلِّ ذَنْبٍ وَّأَتُوْبُ إِلَيْهِ أَسْتَغْفِرُ اللّٰهَ رَبِّيْ مِنْ كُلِّ ذَنْبٍ وَّأَتُوْبُ إِلَيْهِ

Ninamuomba Allah Mola wangu, msamaha wa dhambi zangu zote na ninatubu / naelekea Kwake.

رَبِّ إِنِّيْ ظَلَمْتُ نَفْسِيْ وَاعْتَرَفْتُ بِذَنْبِيْ فَاغْفِرْ لِيْ ذُنُوْبِيْ فَإِنَّهُ لَا يَغْفِرُ الذُّنُوْبَ إِلَّا أَنْتَ

Ee Mola wangu, hakika mimi nilijidhulumu nafsi yangu na ninakiri dhambi zangu zote.
Nakuomba unisamehe dhambi zangu, kwani hakuna awezaye kusamehe dhambi isipokuwa Wewe. Amin.

---

## MAELEZO KAMILI YA ANAYEJIUNGA

1. Jina ....................................................... Tarehe ya kuzaliwa / umri .....................

Uraia ............................... Anuani ....................................Mob: ..........................

Masomo ............................... Kazi .............................. Saini ..............................

***Pia majina ya watoto walio chini ya umri wa miaka 18 na ambao wako chini ya uangalizi wa anayejiunga, yaorodheshwe.***

1. Jina ............................................................... Umri .................................

2. Jina ............................................................... Umri .................................

## WALIOSAIDIA KWA KUKIPIGISHA CHAPA

## MARA YA KWANZA

Jamaa hawa Waahmadiyya nilipowapelekea habari ya mchango wa kusaidia kupigisha chapa kitabu hiki, waliniletea fedha hiyo kwa furaha hata wakashukuru kwa kuipata nafasi ya kusaidia kazi ya dini. Naandika hapa chini majina yao kwa shukrani na kwa ukumbusho. Ninamwomba Mwenyezi Mungu Awajaze kwa mema duniani na Akhera, Amin.

| | |
|---|---|
| Chaudhri Muhammad Ismail | 100 |
| Bibi Fatima Begum, mkewe Chaudhri Muhammad Ismail | 100 |
| Sayyid Mohammad Sarwar Shah | 100 |
| Bibi Zainab Bibi, mkewe Bwana Sheikh Abdulghani | 107 |
| Bwana Nazir Ahmad Dar | 100 |
| Bwana Muhammad Akram Ghauri | 100 |
| Chaudhri Chiragh Din | 121 |
| (Marehemu) Sayyida Hamida Begum | 100 |
| Chaudhri Pir Muhammad | 100 |
| Sheikh Mubarak Ali | 100 |
| Dr. Sayyid Wilayat Shah | 100 |
| Bwana Abdurrahman Kureshi | 101 |
| Chaudhri Bashir Ahmad | 100 |
| Al Haj Muhammad Ayyub | 100 |
| Seth Uthman Yakub | 100 |
| Seth Daud Uthman | 100 |
| Chaudhri Nisar Ahmad | 100 |
| Dr. L. D. Ahmad | 110 |
| Bibi Salima Sultana Mkewe Mirza Ayyub Beg | 100 |
| Jamaa Ahmadiyya, Tanga | 100 |
| Bibi Safiyya Sultana Butt, mkewe Bwana Abdullah Mustafa | 100 |
| Bwana Abdul Aziz Butt | 100 |
| Hayat Family, Kisumu | 100 |
| Lieutenant Nasir Ahmad Shah | 101 |

Sh. N. H. ANWAR,
NAIROBI